



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI
MHE. ENG. GERSON HOSEA LWENGE (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIPIO YA MAPATO
NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI NA
UMWAGILIAJI KWA
MWAKA 2016/2017**

YALIYOMO

1.	UTANGULIZI.....	1
2.	HALI YA SEKTA ZA MAJI NA UMWAGILIAJI NCHINI ⁵	
2.1.	HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI	6
2.1.1.	RASILIMALI ZA MAJI	6
2.1.2.	HUDUMA YA MAJI VIJIJINI.....	8
2.1.3.	HUDUMA YA MAJI MIJINI.....	9
2.1.4.	KUJENGA UWEZO WA TAASISI	12
2.2.	HALI YA SEKTA YA UMWAGILIAJI NCHINI	13
3.	MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2015/2016.....	13
4.	TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/2016 NA MALENGO YA MWAKA 2016/2017	15
4.1.	USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI.....	15
4.1.1.	Mwenendo wa Rasilimali za Maji	15
4.1.2.	Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji.....	16
4.1.3.	Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji.....	18
4.1.4.	Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji	19
4.1.5.	Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji.....	21

4.1.6. Mipango ya Uendelezaji wa Rasilimali za Maji.....	22
4.1.7. Kuimarisha Bodi za Maji	22
4.1.8. Mradi wa Kufanikisha Uhakika wa Maji Eneo la SAGCOT.....	23
4.1.9. Ukusanyaji wa Maduhuli	24
4.1.10. Udhhibiti wa Migogoro katika Matumizi ya Maji	24
4.1.11. Usimamizi wa Rasilimali za Maji Shirikishi.....	25
4.2. HUDUMA ZA UBORA NA USAFI WA MAJI.....	29
4.2.1. Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani	30
4.2.2. Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda, Umwagiliaji, Ujenzi	31
4.2.3. Kuratibu Mwenendo wa Ubora wa Maji katika Vyanzo	32
4.2.4. Ufuatiliaji na Udhhibiti wa Ugonjwa wa Kipindupindu Nchini	32
4.2.5. Utekelezaji wa Mpango wa Usalama wa Maji (Water Safety Plan) na Mwongozo wa Usalama Mahala pa Kazi.....	33
4.2.6. Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa kwenye Mazingira	34
4.2.7. Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji	35
4.2.8. Uondaji wa Madini ya Fluoride katika Maji ya Kunywa na Kupikia	35

4.2.9. Maabara za Maji kupata Ithibati (Accreditation)	37
4.2.10. Mapitio ya Viwango vya Maji na Majitaka	38
4.2.11. Ujenzi na Ukarabati wa Maabara za Maji	38
4.3. HUDUMA YA MAJI VIJIJINI	40
4.3.1. Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini	41
4.3.2. Uendeshaji na Matengenezo	48
4.3.3. Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini kwa Mwaka 2016/2017	49
4.4. HUDUMA YA MAJI MIJINI	50
4.4.1. Kuboresha Huduma za Maji Mijini	51
4.4.2. Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi	62
4.4.3. Miradi ya Kutoa Maji Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali	63
4.4.4. Miradi katika Jiji la Dar es Salaam	65
4.4.5. Huduma ya Maji katika Baadhi ya Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo	71
4.4.6. Miradi iliyo Kwenye Hatua ya Usanifu na Kuombewa Fedha katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa	74
4.4.7. Miradi ya Maji ya Kitaifa	75
4.4.8. Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini	80

4.5.	HUDUMA YA UMWAGILIAJI	81
4.5.1.	Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP I)	81
4.5.2.	Mradi wa Kuendeleza Sera na Rasilimali Watu (Japan Policy for Human Resources Development - PHRD)83	
4.5.3.	Mradi wa Kuendeleza Zao la Mpunga (Expanded Rice Productivity Project - ERPP)	84
4.5.4.	Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (Small Scale Irrigation Development Project - SSIDP).....	84
4.5.5.	Programu ya Kukabiliana na Changamoto za Uhaba wa Chakula Duniani (Feed the Future)	85
4.6.	TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA.....	85
4.6.1.	Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji	85
4.6.2.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)	88
4.6.3.	Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji	91
4.6.4.	Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)	95
4.6.5.	Bohari Kuu ya Maji	96
4.7.	MASUALA MTAMBUKA	97
4.7.1.	Sheria	97
4.7.2.	Habari, Elimu na Mawasiliano.....	100

4.7.3. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.....	101
4.7.4. Jinsia.....	102
4.7.5. UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) 103	
4.7.6. Maendeleo ya Rasilimali Watu.....	103
4.7.7. Mapambano Dhidi ya Rushwa	104
4.7.8. Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji 105	
5. CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA	109
6. SHUKRANI	114
7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017 ...	117

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI
MHE. ENG. GERSON HOSEA LWENGE (MB) AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA YA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI
KWA MWAKA 2016/2017**

1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Daktari Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang'**, ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji; naomba sasa Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2016/2017.

2. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli** pamoja na Makamu wa Rais **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, kwa kupata ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2015. Ushindi huo ni ishara ya imani kubwa ya wananchi waliyonayo kwa Rais, Makamu wa Rais na kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Vilevile, nakipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa kupata ushindi mkubwa katika uchaguzi wa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani.

3. **Mheshimiwa Spika**, nampongeza pia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Daktari Ali Mohamed Shein**, Makamu wa Rais **Mheshimiwa Balazi Seif Ali Iddi** pamoja na Viongozi wengine kwa ushindi walioupata katika Uchaguzi uliofanyika mwezi Machi, 2016. Ushindi huo ni

ishara ya imani kubwa ya wananchi wa Zanzibar waliyonayo kwa Rais na Chama cha Mapinduzi.

4. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa**, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais, na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu. Kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni ishara tosha ya imani aliyonayo Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wa Tanzania kwa utumishi wake uliotukuka.

5. Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Wizara inayomgusa kila mwananchi. Hakuna njia ya kurudisha imani hiyo kubwa isipokuwa kuahidi kuwatumikia wananchi wa Tanzania kwa uadilifu, haki na bila upendeleo. Naahidi kufanya hivyo kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, kwa ufupi nasema "Hapa Kazi Tu".

6. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani kwa wananchi wa Jimbo la Wanging'ombe kwa imani yao waliyonipa kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kura nyingi za kishindo. Nawaahidi nitawatumikia wote kwa uaminifu, bidii na upendo.

7. Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa wawakilishi wa wananchi kwenye majimbo yao. Nikupongeze sana wewe binafsi, **Mheshimiwa Spika Job Yustino Ndugai (Mb)** kwa kuchaguliwa kwako na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Daktari Tulia Ackson (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vilevile, nawapongeza **Mheshimiwa Andrew John Chenge (Mb)**,

Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb) na **Mheshimiwa Mussa Azan Zungu** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge.

8. Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kabisa kuishukuru **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji** kwa ushirikiano inayoendelea kutoa kwa Wizara yangu. Naishukuru Kamati hiyo pia kwa ushauri, maoni na maelekezo iliyoyotoa wakati nilipowasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2015/2016 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2016/2017. Ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati yamewezesha kuboresha kwa kiwango kikubwa Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2016/2017. Ninaiahidi Kamati hiyo kwamba tutazingatia ushauri, maoni na mapendekezo yake katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii.

9. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu**, kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa bungeni ambayo inatoa dira ya utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba hiyo imeonesha mwelekeo wa uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na utekelezaji wa "Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015 - 2020". Nawapongeza pia, Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na wabunge waliochangia hoja hizo.

10. Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kutoa pole kwa wananchi waliopoteza ndugu, marafiki na mali zao kutokana na matukio ya ajali na maafa mbalimbali yakiwemo mafuriko katika baadhi ya maeneo nchini. Namuomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na moyo wa uvumilivu waathirika wote na azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. **Amin.**

11. Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ambayo inatoa taarifa ya hali ya Sekta za Maji na Umwagiliaji nchini; utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 na malengo ya Sekta kwa mwaka 2016/2017; pamoja na maombi ya fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka 2016/2017. Hotuba yangu imezingatia sera na mikakati ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, sheria na miongozo inayohusiana na Sekta za Maji na Umwagiliaji, pamoja na mgawanyo wa kazi kissekta.

2. HALI YA SEKTA ZA MAJI NA UMWAGILIAJI NCHINI

12. Mheshimiwa Spika, maji ni rasilimali muhimu sana na ya lazima kwa ustawi wa binadamu, wanyama, mimea na mazingira ili kuwezesha maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Wizara inaendelea kutekeleza mipango ya Serikali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 - 2030; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Awamu ya I na II); na ahadi mbalimbali za Serikali. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010; pamoja na Sheria za Maji na Umwagiliaji na Kanuni zake.

13. Mheshimiwa Spika, pamoja na Tanzania kuwa na rasilimali za maji za kutosha, mgawanyo wa rasilimali hizo haupo katika uwiano sawa kwenye maeneo mengi nchini hususan maeneo yaliyo kame. Mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu nchini, ukuaji wa shughuli za uzalishaji mali katika sekta za kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa umeme, uzalishaji viwandani, utalii, uchimbaji madini, ufugaji, uvuvi na wanyama pori. Vilevile, rasilimali za maji hutumika kwa ajili ya kuhifadhi bioanuai. Kupungua au kukauka kwa maji katika vyanzo husababishwa na uharibifu wa mazingira, uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi, na matumizi mabaya ya maji.

14. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara yangu kwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni zilizopo imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji pamoja na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya

Kilimo kwa upande wa Umwagiliaji. Hali ya utekelezaji wa Programu hizo ni kama ifuatavyo:-

2.1. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

15. Mheshimiwa Spika, Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imeendelea kutekelezwa katika programu ndogo nne. Programu ndogo hizo ni Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji, Huduma ya Maji Vijijini (inayojumuisha Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira), Huduma ya Maji Mijini na Kujenga Uwezo wa Taasisi. Hadi sasa, utekelezaji wa Programu hiyo umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

2.1.1. RASILIMALI ZA MAJI

16. Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina kiwango kikubwa cha rasilimali za maji zilizopo juu na chini ya ardhi ambapo upatikanaji wake hutegemea mvua. Aidha, upatikanaji wa maji chini ya ardhi hutegemea pia aina na hali ya miamba. Hata hivyo, mtawanyiko wa rasilimali za maji hauko sawa katika maeneo yote ya nchi kutokana na hali za kijiografia, kijiolojia na hali ya mabadiliko ya tabianchi. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini unatekelezwa na Bodi za Maji za Mabonde.

17. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mvua zilizonyesha katika maeneo mbalimbali nchini kuanzia mwezi Novemba, 2014 hadi Oktoba, 2015 zilikuwa za kiwango cha chini zikilinganishwa na taarifa za mvua kwa mwaka uliopita. Mvua hizo zilichangia kupungua kwa kiasi cha maji katika baadhi ya mito, mabwawa na maziwa. Aidha, mvua za masika zilizoanza kunyesha mwezi Machi 2016 katika maeneo mbalimbali nchini zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani na hivyo kuongeza kiasi cha maji katika mito, mabwawa na maziwa.

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kihaidrolojia (Novemba 2014 – Oktoba 2015), viwango vya mvua katika mabonde yote tisa nchini vilikuwa kama ifuatavyo:- Bonde la Rufiji **milimita 749** ikilinganishwa na wastani wa **milimita 1,271** ya mwaka wa kihaidrolojia uliopita (Novemba 2013 – Oktoba 2014); Bonde la Rukwa **milimita 822** ikilinganishwa na **milimita 900**; Bonde la Ziwa Nyasa **milimita 1,103** ikilinganishwa na **milimita 1,643**; Bonde la Kati **milimita 725** ikilinganishwa na **milimita 774**; Bonde la Ziwa Victoria **milimita 1,017** ikilinganishwa na **milimita 1,450**; Pangani **milimita 698** ikilinganishwa na **milimita 817**; Bonde la Ziwa Tanganyika **milimita 770.37** ikilinganishwa na **milimita 890.45**; Bonde la Wami/Ruvu **milimita 1,150.3** ikilinganishwa na **milimita 2,306**; na katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini wastani wa **milimita 951.73** ikilinganishwa na **milimita 1,016.33** mwaka uliopita.

19. Mheshimiwa Spika, wastani wa kina cha maji kutoka usawa wa bahari kwa Ziwa Tanganyika ulikuwa **mita 774.67** ikilinganishwa na **mita 774.72** mwaka wa kihaidrolojia uliopita na Ziwa Nyasa ilikuwa **mita 473.91** ikilinganishwa na **mita 474.48**. Kwa Ziwa Victoria, kina cha maji kutoka usawa wa bahari kilikuwa **mita 1,133.37** ikilinganishwa na **mita 1,133.22** mwaka uliopita. Kwa upande wa mabwawa, kina cha maji kutoka usawa wa bahari katika baadhi ya mabwawa kilikuwa kama ifuatavyo:- Bwawa la Mindu kina cha maji kilipungua kutoka **mita 507.30** hadi **mita 506.90**; Bwawa la Nyumba ya Mungu kutoka wastani wa **mita 684.81** hadi **mita 683.48**; na Bwawa la Kidatu, kina cha maji kilipungua kutoka **mita 448.87** hadi **mita 443.91** ambapo kina hicho kilikuwa chini ya mita za maji kinachohitajika kuzalisha umeme ambacho ni **mita 450**.

20. Mheshimiwa Spika, kupungua kwa maji kwenye mabwawa hayo kumetokana na mvua kunyesha chini ya wastani kwa mwaka wa kihaidrolojia 2014/2015. Bwawa la Mtera kina kiliongezeka kutoka **mita 691.69** hadi **mita 695.61**, kina hicho kipo juu ya usawa wa mita za uzalishaji umeme ambacho ni **mita**

690. Ongezeko la kina cha maji katika Bwawa la Mtera limetokana na udhibiti wa matumizi ya maji katika ukanda wa juu wa bwawa pamoja na mitambo ya kuzalisha umeme katika bwawa hilo kutofanya kazi kwa muda wa miezi mitano kuanzia mwezi Novemba, 2015 hadi mwezi Machi, 2016.

21. Mheshimiwa Spika, takwimu za kitaifa za rasilimali za maji zilizopo zinaonesha kuwa Tanzania inaelekea kuwa nchi yenye uhaba wa maji endapo hatua madhubuti za utunzaji wa vyanzo vya maji hazitachukuliwa mapema. Kutokana na rasilimali maji zilizopo, kila mwananchi ana uwezo wa kupata **mita za ujazo 1,952** kwa mwaka na kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni **mita za ujazo 1,700**. Iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa, inatarajiwa kuwa ifikapo mwaka 2035, kiwango cha maji kilichopo kinaweza kupungua hadi **mita za ujazo 883** kwa kila mwananchi. Wizara yangu kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa uvunaji wa maji ya mvua ili nchi yetu isifikie kiwango hicho cha uhaba wa maji na kusababisha athari kubwa kwenye maendeleo ya nchi.

2.1.2. HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

22. Mheshimiwa Spika, miradi ya maji vijijini inatekelezwa chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kuzingatia Mpango wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*)”. Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji vijijini imeongezeka kutoka **milioni 15.2** sawa na **asilimia 40** ya wananchi waishio vijijini mwezi Julai, 2013 tulipoanza utekelezaji wa *BRN* na kufikia watu **milioni 21.9** sawa na **asilimia 72** mwezi Machi, 2016. Hayo ni mafanikio makubwa sana katika utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. Lengo ni kufika **asilimia 85** ifikapo mwaka 2020. Kwa mwaka 2016/2017, Wizara yangu imelenga kukamilisha miradi inayoendelea kujengwa, kukarabati miradi ambayo haifanyi kazi, upanuzi wa miradi iliyopo na kujenga miradi mipya ili kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma

ya maji vijijini. Kazi hizo zinafanyika kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Serikali za Mitaa, wananchi, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji.

2.1.3. HUDUMA YA MAJI MIJINI

23. Mheshimiwa Spika, huduma za maji mijini hutolewa kupitia Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwenye Miji Mikuu ya Mikoa **23** pamoja na Dar es Salaam; Miji Mikuu ya Wilaya **99**, Miji Midogo **14**; na miradi **8** ya maji ya Kitaifa. Malengo yaliyopo ni kuboresha huduma hiyo katika Miji Mikuu ya Mikoa kutoka **asilimia 86** hadi kufikia **asilimia 95** mwaka 2020; katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa lengo ni kufikia **asilimia 90** kutoka **asilimia 60** za sasa; na kwa Jiji la Dar es Salaam kutoka **asilimia 72** hadi kufikia **asilimia 95** mwaka 2020. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imepanga kujenga na kupanua miundombinu ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa na kukamilisha Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya Maji Safi na Salama katika Jiji la Dar es Salaam.

(a) Huduma ya Majisafi Mijini

(i) Miji Mikuu ya Mikoa

24. Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji mikuu ya Mikoa zimeendelea kuimarika na kuweza kutoa huduma iliyo bora kwa wananchi wa miji hiyo. Uzalishaji wa majisafi umeongezeka kutoka **lita milioni 385** kwa siku mwezi Aprili 2015 hadi kufikia **lita milioni 470** kwa siku mwezi Machi, 2016. Idadi ya wateja waliounganishiwa huduma ya maji imeongezeka kutoka **362,953** mwezi Aprili, 2015, hadi wateja **405,095** mwezi Machi, 2016 ambapo wateja **392,942** sawa na **asilimia 97** wamefungiwa dira za maji. Lengo ni wateja wote waliounganishiwa huduma ya maji kuwa na dira za maji ili kupunguza upotevu wa maji kufikia wastani wa **asilimia 30** kutoka **asilimia 35** za sasa. Makusanyo ya maduhuli kwa mwezi

yatokanayo na mauzo ya maji yameongezeka kutoka **shilingi bilioni 7.28** mwezi Aprili, 2015 hadi kufikia **Shilingi bilioni 8.50** mwezi Machi 2016 sawa na ongezeko la **asilimia 17**. Wizara inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka hizo ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma iliyo bora na endelevu.

(ii) Jiji la Dar es Salaam

25. Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam linakadiriwa kuwa na wakazi zaidi ya **milioni 4.5**, ambapo mahitaji ya maji kwa ajili ya wakazi hao ni **lita milioni 450** kwa siku. Baada ya kukamilika kwa miradi ya Ruvu Juu na Ruvu Chini, uzalishaji wa maji umefikia **lita milioni 504** kwa siku. Pamoja na uzalishaji huo, bado maeneo mengi yameendelea kupata maji kwa mgao wa wastani wa **saa 8** hadi **20** kwa siku kutokana na kutokukamilika kwa miundombinu ya kusambaza maji. Aidha, idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majisafi wameongezeka kutoka wateja **126,405** mwezi Aprili, 2015 hadi wateja **155,000** mwezi Machi, 2016. Vilevile, wastani wa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na mauzo ya maji kwa mwezi yameongezeka kutoka **Shilingi bilioni 3.31** mwezi Aprili, 2015 hadi **Shilingi bilioni 7.1** mwezi Machi, 2016.

26. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam, **DAWASCO** imeanza kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kampeni ya “**Mama Tua Ndoo ya Maji Kichwani**” ambayo imewezesha kufikisha huduma ya maji katika maeneo mapya **52** yaliyokuwa hayapati huduma hiyo kwa kipindi kirefu. Pamoja na kampeni hiyo, Wizara yangu imeendelea kukabiliana na tatizo la upotevu wa maji ambao umepungua kutoka **asilimia 57** mwezi Aprili, 2015 hadi kufikia **asilimia 47** mwezi Machi, 2016. Lengo ni kupunguza upotevu huo hadi **asilimia 30** ifikapo mwezi Juni, 2017.

(iii) Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

27. Mheshimiwa Spika, mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa ambazo ziko katika daraja 'C' hutegemea ruzuku ya Serikali kwa ajili ya shughuli za uendeshaji. Serikali inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka hizo ili zipande daraja kutoka 'C' hadi madaraja ya 'B' na 'A' na hivyo ziweze kujendesha kibiashara na kupunguza utegemezi kwa Serikali. Mfano ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Kahama ambayo imepanda kutoka daraja 'C' hadi daraja 'A' baada ya kuweza kujendesha kibiashara na kupunguza mzigo wa kuitegemea Serikali Kuu.

28. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ambapo uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka **lita milioni 99.2** kwa siku mwezi Aprili, 2015 hadi **lita milioni 99.5** kwa siku mwezi Machi, 2016. Pamoja na jitihada hizo, upatikanaji wa huduma hiyo haukidhi mahitaji ya sasa ya **lita milioni 247** kwa siku. Aidha, idadi ya wateja waliunganishwa kwenye mtandao imeongezeka kutoka wateja **107,313** mwezi Aprili, 2015 hadi wateja **115,760** mwezi Machi, 2016. Kati ya wateja hao, **asilimia 63** wameunganishiwa dira za maji ikilinganishwa na **asilimia 58** mwezi Aprili, 2015. Hali ya upatikanaji wa maji katika miji hiyo ni wastani wa **saa 9** kwa siku na upotevu wa maji umepungua kutoka **asilimia 45** mwezi Aprili, 2015 hadi **asilimia 41** mwezi Machi, 2016.

29. Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa ni **lita milioni 109** kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa **lita milioni 57.2** za maji kwenye maeneo hayo. Aidha, uzalishaji umeongezeka kutoka **lita milioni 51.6** kwa siku mwezi Aprili, 2015 hadi **lita milioni 57.2** kwa siku mwezi Machi, 2016. Hali ya upatikanaji wa maji imeboreshwa kutoka **saa 9** hadi **saa 16** kwa siku. Vilevile, idadi ya wateja waliunganishwa na huduma ya maji imeongezeka kutoka wateja

16,995 mwezi Aprili, 2015 hadi wateja **18,932** mwezi Machi, 2016 na kati ya wateja hao, **asilimia 75** wamefungiwa dira za maji.

(b) Uondoaji wa Majitaka Mijini

30. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuboresha huduma ya uondoaji wa majitaka katika miji mbalimbali. Hadi sasa, wastani wa upatikanaji wa huduma ya uondoaji majitaka ni **asilimia 20** kwenye miji yenye mtandao wa majitaka ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa. Idadi ya wateja waliunganishwa kwenye mtandao wa majitaka imeongezeka kutoka **24,346** mwezi Aprili, 2015 hadi kufikia wateja **25,361** mwezi Machi, 2016. Pamoja na ongezeko hilo, bado wastani wa huduma ya uondoaji majitaka mijini ni ndogo. Hali hiyo inasababishwa na mwamko mdogo wa wananchi kujiunga kwenye mtandao wa majitaka katika miji hiyo. Vilevile, miundombinu ya majitaka kwa baadhi ya miji ni chakavu na haiwezi kumudu mahitaji ya sasa.

2.1.4. KUJENGA UWEZO WA TAASISI

31. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Wizara inaendelea kujenga uwezo wa taasisi zinazotekeleza Programu za Maendeleo ya Sekta za Maji na Kilimo kwa upande wa Umwagiliaji. Jumla ya wataalam **12,148** wa kada za uhandisi na ufundi sanifu wanahitajika ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Maji na Umwagiliaji. Hadi mwezi Machi 2016, kuna jumla ya wataalam **2,224** katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya; na hivyo, Sekta hizo kukabiliwa na upungufu wa wataalam wapatao **9,924**. Upungufu huo unatokana na watumishi kustaafu, kufariki ama kuacha kazi; Serikali kutoajiri kwa muda mrefu; pamoja na kuongezeka kwa idadi ya Mikoa na Halmashauri. Wizara inaendelea na majadiliano na Mamlaka zinazohusika na ajira serikalini ili kupata ufumbuzi wa kuziba

nafasi za wataalam ambazo ziko wazi. Vilevile, taasisi za utekelezaji zimeendelea kuimarishwa kwa kujengewa ofisi na kupatiwa vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma na utekelezaji wa programu.

2.2. HALI YA SEKTA YA UMWAGILIAJI NCHINI

32. Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina jumla ya eneo la **hekta milioni 29.4** zinazofaa kwa umwagiliaji. Kati ya hizo, **hekta milioni 2.3** zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, **hekta milioni 4.8** zina uwezekano wa kati na **hekta milioni 22.3** zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa. Hadi sasa, eneo linalomwagiliwa ni **hekta 461,326** sawa na **asilimia 1.6** ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na linachangia **asilimia 24** ya mahitaji yote ya chakula nchini kwa sasa.

33. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Sekta ya Umwagiliaji nchini yanasimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupitia ofisi nane za Umwagiliaji za kanda. Lengo lililopo ni kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka **hekta 461,326** hadi kufikia **hekta 1,000,000** katika skimu za wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ifikapo mwaka 2020. Aidha, katika hatua ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, Wizara imepanga kukamilisha ujenzi wa mabwawa **30** na kujenga mabwawa mapya **40** ili kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine ifikapo mwaka 2020.

3. MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2015/2016

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji liliidhinishwa jumla ya **Shilingi 458,900,981,000** na kati ya fedha hizo **Shilingi 31,643,077,000** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi

427,257,904,000 zilikuwa ni fedha za matumizi ya maendeleo. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya **Shilingi 81,424,625,108.77** ya fedha za maendeleo zilipokelewa ikiwa ni sawa na **asilimia 19.06** ya fedha zilizoidhinishwa; na **Shilingi 2,342,922,874** ya fedha za matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 7.40** ya fedha zilizoidhinishwa.

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, kwa upande wa Fungu 5 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji jumla ya **Shilingi 53,826,490,195** ziliidhinishwa na kati ya fedha hizo **Shilingi 232,116,195** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 53,594,374,000** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya **Shilingi 5,131,032,985** ya fedha za maendeleo zilipokelewa ikiwa ni sawa na **asilimia 9.6** ya fedha zilizoidhinishwa; na **Shilingi 97,822,534** ya fedha za matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 42.1** ya fedha zilizoidhinishwa.

4. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/2016 NA MALENGO YA MWAKA 2016/2017

36. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2015/2016 na malengo ya mwaka 2016/2017 kwa Sekta za Maji na Umwagiliaji umejikita katika kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini; kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini; uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji na kutekeleza malengo ya masuala mtambuka. Taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na mpango wa malengo ya utekelezaji kwa mwaka 2016/2017 imechambuliwa kwa undani katika aya zifuatazo.

4.1. USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI

37. Mheshimiwa Spika, wajibu wa Wizara yangu ni kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji kupitia Bodi ya Maji ya Taifa, Bodi za Maji za Mabonde na Maabara za Maji nchini. Usimamizi na uendelezaji huo unahusu kuchunguza, kutathmini na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji, ubora wa maji, pamoja na usimamizi wa rasilimali za majishirikishi (*transboundary water resources*). Wizara inazijengea uwezo na kuziimarisha Bodi ya Maji ya Taifa, Bodi za Maji za Mabonde na Maabara za Maji ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Utekelezaji wa majukumu hayo umeelezwa kwa kina katika aya zifuatazo.

4.1.1. Mwenendo wa Rasilimali za Maji

38. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu huchunguza wingi na ubora wa rasilimali za maji zilizopo juu na chini ya ardhi kwa kutumia mtandao wa vituo vya kupima mwenendo wa rasilimali hizo. Takwimu na taarifa zinazopatikana huchambuliwa na

matokeo yake huiwezesha Serikali kutoa taarifa za hali ya maji nchini; kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya ukame na mafuriko; na kuibua na kusanifu miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

39. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 vituo vya kupima wingi wa maji yaliyopo juu na chini ya ardhi viliendelea kukaguliwa, kujengwa na kukarabatiwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya vituo **24** vilijengwa katika mabonde ya Rufiji (**8**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**6**), Pangani (**5**), Wami/Ruvu (**2**), Ziwa Victoria (**2**) na Ziwa Tanganyika kituo **kimoja (1)**. Vilevile, vituo **139** vilifanyiwa ukarabati katika mabonde ya Pangani (**69**), Ziwa Tanganyika (**35**), Rufiji (**25**), Ziwa Rukwa (**4**), Ziwa Nyasa (**2**), Wami/Ruvu (**2**) na Ziwa Victoria (**2**). Aidha, takwimu za mwenendo wa rasilimali za maji zimekusanywa kupitia vituo **570** katika mabonde yote kwa kupima mwenendo wa maji kwenye vituo **267** vilivyopo kwenye mito, vituo **186** vya kupima mvua, vituo **71** vya hali ya hewa, vituo **26** vya mwenendo wa maji chini ya ardhi na vituo **20** vya kupima kina cha maji kwenye mabwawa na maziwa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji nchini, kukagua na kukarabati vituo vilivyoharibika, kujenga vituo vipya kulingana na mahitaji na kukusanya takwimu za hali ya maji pamoja na kuimarisha kanzidata (*database*) kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

4.1.2. Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji

40. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kutambua vyanzo vinavyotakiwa kuhifadhiwa na hatimaye kutangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji. Katika mwaka 2015/2016, vyanzo vya maji **111** vilitambuliwa na vimepangwa kuwekewa mipaka na kuandaliwa taarifa ili viweze kutangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji. Taarifa kwa ajili ya vyanzo **8** vilivyoko Bonde la Ziwa Rukwa kwa ajili ya matumizi ya

maji katika Jiji la Mbeya imekamilika na taratibu za kutangazwa vyanzo hivyo zinaendelea. Aidha, taarifa za chanzo cha maji cha Mbwinji kinachohudumia Wilaya za Masasi na Nachingwea pamoja na Bwawa la Mindu lililopo Morogoro zimewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kutangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji.

41. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji, madhara ya uharibifu wa vyanzo vya maji, pamoja na sheria na kanuni mbalimbali za usimamizi wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imepanga kutangaza maeneo **18** ya vyanzo vya maji, kuendelea kuyawekea mipaka na kutangaza maeneo yaliyoainishwa ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji na usalama wa vyanzo hivyo.

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuunda na kuimarisha Jumuiya za Watumia Maji ili ziweze kusimamia rasilimali za maji katika ngazi ya chini. Hadi mwezi Machi 2016, Jumuiya **5** ziliundwa katika mabonde ya Ziwa Tanganyika (**1**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**1**), Pangani (**1**), Ziwa Rukwa (**1**) na Ziwa Victoria (**1**); na jumla ya Jumuiya **5** ziliimarishwa katika mabonde ya Rufiji (**3**) na Pangani (**2**) ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, Kamati **4** za mabonde madogo ya maji (*Catchments and Sub-catchment Committees*) katika Bonde la Pangani (**2**) na Wami/Ruvu (**2**) zimeundwa. Taarifa kwa ajili ya maeneo **matano** ya mabonde madogo ya maji ya Wami na Mkondoa katika Bonde la Wami/Ruvu na Mara, Tabora na Somoche katika Bonde la Ziwa Victoria zinaandaliwa kwa ajili ya kutangazwa. Kutangazwa kisheria kwa mabonde hayo kutawezesha kuundwa kwa Kamati za mabonde madogo ambazo zina jukumu la kusimamia rasilimali za maji katika ngazi ya mabonde madogo na kuweza kuzisimamia Jumuiya za Watumia Maji zitakazokuwa chini yao. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaunda Jumuiya za Watumiaji

Maji **33** na Kamati **18** za mabonde madogo na kuendelea kuimarisha jumuiya na kamati zilizopo.

43. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji hususan katika maeneo kame, Serikali imeendelea kutekeleza mipango ya kuhifadhi maji kwa kujenga mabwawa ya kimkakati na kukarabati mabwawa ya ukubwa wa kati. Mabwawa hayo yanatakiwa kuandaliwa taarifa za tathmini za athari za kimazingira na kijamii ili yaweze kujengwa kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira **Na. 20** ya mwaka 2004. Taarifa za tathmini za athari kwa mazingira na jamii kwa ajili ya miradi ya mabwawa ya Farkwa na Ndembera ziliwasilishwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*National Environment Management Council – NEMC*) kwa ajili ya kupata cheti cha mazingira kinachoruhusu ujenzi wa miradi ya maendeleo. Tayari cheti cha mazingira kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Farkwa kimetolewa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaandaa taarifa ya tathmini za athari kwa mazingira na jamii pamoja na usanifu wa mabwawa **16** ya ukubwa wa kati katika mabonde ya Ziwa Victoria mabwawa **manne**, Bonde la Kati (**4**), Ziwa Tanganyika (**3**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**2**), Rufiji (**1**), Wami/Ruvu (**1**) na Pangani bwawa **moja** ili yaweze kukarabatiwa na hivyo kuongeza upatikanaji wa maji katika maeneo hayo.

4.1.3. Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

44. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, jumla ya sampuli **247** za majitaka kutoka viwandani na maeneo ya uchimbaji madini zilichukuliwa na kuchunguzwa katika mabonde ya Wami/Ruvu sampuli **96**, Rufiji (**89**), Ziwa Victoria (**41**), Ziwa Nyasa (**18**) na Bonde la Ziwa Rukwa sampuli **3**. Matokeo ya zoezi hilo yalibaini kuwa majitaka kutoka baadhi ya maeneo hayo hayakidhi viwango vya kuweza kutiririshwa katika vyanzo vya maji. Viwanda na Taasisi zilizobainika kuwa na miundombinu isiyoridhisha, ziliagizwa kufanya marekebisho ili kuondoa kasoro zilizoonekana kwa lengo

la kuhakikisha majitaka yanasafishwa kwa viwango vinavyokubalika kisheria kabla ya kutirishwa kwenye vyanzo vya maji. Vilevile, sampuli **476** kutoka vyanzo mbalimbali vya maji zilichukuliwa na kupimwa kwenye maabara katika mabonde ya Wami/Ruvu sampuli **196**, Rufiji (**95**), Pangani (**71**), Ziwa Rukwa (**44**), Ziwa Nyasa (**31**), Ziwa Tanganyika (**13**), Ziwa Victoria (**11**) na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini sampuli **6**. Uchunguzi huo ulibaini kuwa baadhi ya vyanzo vya maji vimeendelea kuchafuliwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo na kusababisha maji hayo kutokuwa salama. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu itaendelea kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji ili kulinda rasilimali za maji nchini.

45. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kusimamia ujenzi wa mabwawa ya majisafi na mabwawa ya majitaka nchini. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa bwawa linalojengwa na Mgodu wa Shanta kwenye Bonde la Mto Luika katika Wilaya ya Chunya. Bwawa hilo ni kwa ajili ya matumizi ya Mgodu wa *New Luika* na jamii inayozunguka maeneo hayo. Aidha, Wizara imetoa vibali vya ujenzi wa mabwawa mawili ya kuhifadhi majitaka yanayotokana na shughuli za migodi (*Tailings Storage Facilities*) katika migodi ya *CATA Mine Ltd* na *Bulyanhulu Gold Mine*. Vilevile, Wizara imeendelea kukagua ujenzi wa mabwawa ya aina hiyo katika migodi ya Tulawaka, Bulyanhulu, Geita na Buzwagi.

4.1.4. Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji

46. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utafutaji wa vyanzo vipya vya maji katika maeneo yenye uhaba wa maji juu ya ardhi na maeneo yenye ukame. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya maeneo **203** yanayofaa kuchimbwa visima yalitambuliwa katika mabonde ya Pangani maeneo **71**, Ruvuma na Pwani ya Kusini (**42**), Ziwa Tanganyika (**42**), Bonde la Kati (**21**), Wami/Ruvu (**8**), Rufiji (**7**), Ziwa Victoria (**5**), Ziwa Nyasa (**4**) na Ziwa Rukwa maeneo **matatu**. Katika mwaka 2016/2017,

Serikali itaendelea kuvitambua vyanzo vya maji na kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo mengine zaidi ili kuongeza upatikanaji wa maji nchini.

47. Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuongeza upatikanaji wa maji katika **maeneo kame nchini**, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuongeza upatikanaji wa maji. Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Misri imekamilisha uchimbaji wa visima **30** kati ya **70** vilivyopangwa kuchimbwa katika awamu ya pili kwenye Wilaya za Itilima visima **10**, Kiteto **(9)**, Same **(8)**, Bariadi **(2)** na Wilaya ya Mwanga kisima **kimoja**. Kati ya hivyo, visima **21** vimefungwa pampu na vinatumika. Ufungaji wa pampu kwa visima **tisa** vilivyobaki, visima **6** Wilaya ya Itilima, **viwili** Wilaya ya Bariadi na kisima **kimoja** Wilaya ya Kiteto unaendelea. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imepanga kuchimba visima **20** na kukarabati visima **30** vya kuchunguza mwenendo wa maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

48. Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuratibu kampuni za uchimbaji wa visima vya maji ambapo hulazimika kupata leseni kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kabla ya kuanza kazi za uchimbaji. Hatua hii husaidia kuzitambua na kufuatilia utendaji kazi wa kampuni hizo. Katika mwaka 2015/2016, Wizara ilitoa leseni **8** kwa kampuni za uchimbaji visima vya maji na leseni **mbili** kwa kampuni za utafiti wa maji chini ya ardhi. Aidha, jumla ya visima vya maji **1,004** vilichimbwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hivyo, visima **185** vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) na visima **819** vilichimbwa na kampuni binafsi. **Jedwali Na. 1** linaonesha idadi ya visima vilivyochimbwa na makampuni mbalimbali ikiwemo *DDCA*. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kutoa leseni za uchimbaji kwa kampuni zinazokidhi viwango, kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Kanuni zake ili kudhibiti uchimbaji holela wa visima nchini.

49. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara iliendelea kutekeleza miradi ya mabwawa ya kimkakati ya Kidunda, Farkwa na Ndembera. Hadi mwezi Machi 2016, kazi za awali za upembuzi yakinifu, uchunguzi wa kina wa miamba, usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo zimekamilika. Aidha, makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati ya Nkiniziwa na Itobo (Nzega), Lemioni na Enguikment II (Monduli) yamekamilika. Katika mwaka 2016/2017, ujenzi wa mabwawa hayo ya kimkakati na ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati unatarajiwa kuanza.

4.1.5. Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji

50. Mheshimiwa Spika, Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kusimamia matumizi bora ya maji katika maeneo mbalimbali kwa kutoa vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka kwa mujibu wa Sheria **Na. 11** ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Kanuni zake. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya vibali vya kutumia maji **490** vilitolewa katika Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Tanganyika vibali **148**, Rufiji **126**, Nyasa (**62**), Pangani (**42**), Wami/Ruvu (**31**), Ziwa Victoria (**30**), Bonde la Kati (**25**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**15**) na Ziwa Rukwa vibali **11**. Vilevile, vibali **25** vya kutiririsha majitaka vilitolewa katika mabonde ya Ziwa Victoria vibali **10**, Pangani (**9**), Wami/Ruvu (**3**), Ruvuma na Pwani ya Kusini (**2**) na Rufiji kibali **kimoja (1)**. Aidha, ukaguzi ulifanyika katika mabonde ya maji na kubaini kuwa jumla ya watumiaji maji **1,568** wa matumizi mbalimbali hawakuwa na vibali vya kutumia maji. Watumiaji hao walielimishwa kuhusu taratibu za kisheria za matumizi endelevu ya maji na kuagizwa kuomba vibali vya kutumia maji hayo. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imepanga kutoa vibali **600** vya kutumia maji na vibali **43** vya kutiririsha majitaka.

4.1.6. Mipango ya Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

51. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, Mipango Shirikishi ya Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji (*Integrated Water Resources Management and Development Plans – IWRM&D*) katika Bodi za Maji za Mabonde 6 imekamilika. Bodi hizo ni Ruvuma na Pwani ya Kusini, Bonde la Kati, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa na Rufiji. Kwa sasa Tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii (*Strategic Environment and Social Assessment*) imeanza kutekelezwa katika Bonde la Rufiji. Vilevile, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kutayarisha tathmini hiyo kwa mabonde mengine **matano** yaliyokamilisha mipango shirikishi zimekamilika. Aidha, taratibu za kuwapata Wataalam Washauri kwa ajili ya kutayarisha mipango shirikishi ya Bodi za Maji za Mabonde **matatu** ya Pangani, Wami-Ruvu na Ziwa Victoria zimeanza na utayarishaji utakamilika katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea na Tathmini za Kimkakati za Kimazingira na Kijamii kwa mipango iliyokamilika.

4.1.7. Kuimarisha Bodi za Maji

52. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi na kuboresha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini, Wizara imeunda Bodi ya Maji ya Taifa yenye wajibu wa kumshauri Waziri mwenye dhamana ya maji katika masuala mbalimbali yanayohusu rasilimali za maji. Bodi hiyo inajumuisha wajumbe kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Taasisi za Serikali zinazohusiana na Sekta ya Maji; Sekta Binafsi na Asasi zisizo za Kiserikali. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde 9 nchini kwa kujenga ofisi, kuzipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, ujenzi wa Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde uliendelea na umefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Ujenzi wa ofisi katika Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria iliyopo Mwanza na Ofisi ndogo ya Bonde la Rufiji iliyopo Ifakara umekamilika. Ujenzi katika ofisi za bonde la Ziwa Tanganyika umefikia **asilimia 90** na katika Bonde la Kati ujenzi umefikia **asilimia 70**. Ujenzi wa ofisi za Bodi za mabonde ya Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa umeanza katika Miji ya Njombe, Songea, Mbeya, Mtwara, Lindi, Tunduru, Likonde na Sumbawanga. Ofisi hizo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2016/2017. Vilevile, jumla ya watumishi **211** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na semina. Katika mwaka 2016/2017 Wizara yangu itaendelea kujenga uwezo wa taasisi inazozisimamia zikiwemo Bodi za Maji za Mabonde.

4.1.8. Mradi wa Kufanikisha Uhakika wa Maji Eneo la SAGCOT

54. Mheshimiwa Spika, mradi wa kufanikisha uhakika wa maji kwenye eneo la *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* (SAGCOT) unafadhiliwa na **Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Serikali ya Uingereza (Department for International Development - DFID)** na unagharimu **Paundi za Uingereza milioni 5**. Mradi huo unatekelezwa katika Bonde la Maji la Mto Rufiji na unahusu ujenzi wa ofisi, kununua vitendea kazi, kujenga uwezo wa kukusanya, kutunza na kuchambua takwimu, kujenga vituo vya kukusanya takwimu kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa vituo, kuunda taasisi za usimamizi wa rasilimali za maji, kufuatilia hali ya ubora wa maji, kuendesha mafunzo mbalimbali, kutathmini rasilimali za maji chini ya ardhi na kuchimba visima vya kufuatilia hali ya maji chini ya ardhi kwa ajili ya kukusanya takwimu zitakazowezesha kutoa maamuzi ya kutumia rasilimali hiyo kwenye eneo la SAGCOT.

55. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa ofisi ndogo ya Bonde la Rufiji iliyopo Ifakara; ununuzi wa magari **matatu**; ununuzi na ufungaji wa vifaa vya kupima wingi wa maji kwenye mito, pampu **3** za maji, *data logger* (**24**) na jenereta (**1**); na mafunzo kwa watumiaji wa vifaa hivyo yamefanyika. Vilevile, uchimbaji wa visima **vinane (8)** vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi umekamilika. Awamu ya kwanza ya mradi huo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Awamu ya pili ya mradi inatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2016 na itagharimu **Paundi za Uingereza milioni 31.7** kwa kipindi cha miaka mitano. Maandalizi ya awamu hiyo yanaendelea kwa kuandaa kazi zitakazotekelezwa kwa kipindi hicho katika ngazi ya Wizara na katika mabonde ya Rufiji na Pangani. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya **Paundi za Uingereza milioni 1.5** zitatumika katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa.

4.1.9. Ukusanyaji wa Maduhuli

56. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupunguza utegemezi kwa Serikali, Bodi za Maji za Mabonde zina jukumu la kukusanya maduhuli ili kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za maji kwa ufanisi. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya **Shilingi bilioni 2.6** zilikusanywa ambazo ni sawa na **asilimia 86** ya lengo la **Shilingi bilioni 3.02** zilizopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Katika mwaka 2016/2017, Bodi za Maji za Mabonde zimeleaga kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 3.81** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. **Jedwali Na. 2** linaonesha makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, 2015/2016 na makadirio ya makusanyo kutoka Bodi za Maji za Mabonde kwa mwaka 2016/2017.

4.1.10. Udhibiti wa Migogoro katika Matumizi ya Maji

57. Mheshimiwa Spika, migogoro katika matumizi ya maji kwenye maeneo ya vyanzo vya maji imeendelea kujitokeza kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupungua kwa wingi wa

maji kwenye vyanzo pamoja na wananchi kutofuata sheria na kanuni za matumizi bora ya maji. Bodi za Maji za Mabonde zina jukumu la kugawa na kusimamia maji kwa uwiano sahihi kwa watumiaji kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni za rasilimali za maji. Vilevile, Bodi hizo kwa kushirikiana na Jumuiya za Watumiaji Maji zimekuwa zikisuluhisha migogoro hiyo pamoja na kutoa ushauri wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji pale inapostahili. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya migogoro 17 ilijitokeza na kusuluhishwa katika Bodi za Maji za mabonde ya Pangani (11), Ziwa Nyasa (2), Ziwa Rukwa (2), Wami/Ruvu (1) na Rufiji (1). Elimu kuhusu ugawaji na utunzaji wa rasilimali za maji inaendelea kutolewa kwa watumiaji maji ili kupunguza migogoro hiyo.

4.1.11. Usimamizi wa Rasilimali za Maji Shirikishi

58. Mheshimiwa Spika, usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi ni suala la kipaumbele kwa nchi yetu ikizingatiwa kuwa mabonde saba kati ya tisa ya maji ni ya maji shirikishi. Aidha, Tanzania ni sehemu ya Mabonde Makuu matatu katika bara la Afrika, ambayo ni Bonde la Mto Nile, Bonde la Mto Kongo na Bonde la Mto Zambezi. Rasilimali za maji shirikishi za Tanzania ni pamoja na Mito ya Ruvuma, Kagera, Mara, Uмба, Momba na Songwe; na Maziwa ya Chala, Jipe, Victoria, Tanganyika, Nyasa na Natron. Tanzania inashirikiana na nchi nyingine kupitia mikataba au makubaliano ambayo yameanzisha Kamisheni au Taasisi za Kikanda kama vile SADC, Nile Basin Initiative (NBI), Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (Lake Victoria Basin Commission - LVBC), Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, Kamisheni ya pamoja ya Maji ya Mto Ruvuma na Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (ZAMCOM). Aidha, Tanzania ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri wa Maji barani Afrika (AMCOW) ambapo imefaidika na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za pamoja. Utekelezaji wa miradi na programu hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria

59. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda zimeendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Program - LVEMP II*). Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika Ziwa hilo. Kwa upande wa Tanzania, mradi unatekelezwa katika Miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba pamoja na Halmashauri za Wilaya za Maswa, Itilima, Busega, Bariadi, Magu, Meatu, Kwimba, Sengerema, Geita, Chato, Muleba, Karagwe, Kyerwa na Misenyi. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya miradi midogo **341** ya kijamii yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 8.3** iliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji. Kati ya miradi hiyo, utekelezaji wa miradi **173** umekamilika, miradi **140** iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi **28** iliyosalia inatarajiwa kutekelezwa katika mwaka 2016/2017. Vilevile, mradi wa *LVEMP II* kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Taasisi mbalimbali za Serikali, unafadhili utekelezaji wa miradi mikubwa **24** ya kijamii (*Co-Management Interventions*) yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 5.7** ambapo miradi **15** imekamilika, miradi **sita** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi **mitatu** itatekelezwa katika mwaka 2016/2017.

60. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutekeleza *LVEMP II*, usanifu wa miradi ya uunganishaji wa mfumo wa majitaka ya majumbani kwenye mtandao mkuu wa majitaka Jijini Mwanza, na ukarabati wa machinjio na ujenzi wa mfumo wa kusafisha majitaka ya machinjio ya Mwanza (*Constructed Wetland Intergrated with Biogas Plant*) umekamilika. Utekelezaji wa miradi hiyo utanza katika mwaka 2016/2017. Aidha, ukarabati wa Maabara za Maji za Mwanza na Musoma pamoja na ujenzi wa Maabara ya Bukoba umeanza. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016.

61. Mheshimiwa Spika, vilevile, Mradi kwa kushirikiana na Kitengo cha Afya ya Mimea chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi unaendelea kufuatilia, kuondoa na kudhibiti gugumaji katika Ziwa Victoria kwa kutumia njia za kibaiolojia (*introduction of weevils*) pamoja na nyenzo rahisi za mikono. Mradi umefanikiwa kupunguza uwepo wa gugumaji katika Ziwa Victoria kutoka **hekta 518** mwaka 2009 hadi **hekta 104** mwezi Machi, 2016. Kupungua kwa gugumaji kumesaidia kuongeza ubora wa maji na kurahisisha usafirishaji katika Ziwa. Aidha, vifaa vya mawasiliano majini vilinunuliwa na kukabidhiwa kwa Mamlaka ya Usafirishaji Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uokoaji ziwani. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira wa Ziwa Victoria, imeipatia Idara ya Uvuvi boti **3** za doria ambazo zitagawiwa kila moja katika Mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za samaki ziwani.

(b) Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe

62. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi imeendelea kutekeleza awamu ya pili ya programu ya kuendeleza rasilimali za Bonde la Mto Songwe. Awamu hii inahusu usanifu wa kina wa skimu ya umwagiliaji na bwawa **1** kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, kuzuia mafuriko na kuzuia kuhamahama kwa mto. Jumla ya **hekta 3,005** zinatarajiwa kumwagiliwa na megawati **180** za umeme kuzalishwa. Hadi mwezi Machi 2016, rasimu ya makubaliano ya kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Bonde la Mto Songwe (*Convention for Establishment of Songwe River Basin Commission*) imekamilika na kwa sasa Wizara imeanza maandalizi kwa ajili ya Bunge kuridhia makubaliano hayo. Vilevile, Mtaalam Mshauri amekamilisha usanifu wa kina wa bwawa moja (*Lower Songwe dam*); rasimu za tathmini ya athari za mazingira na kijamii (*Draft ESIA*); Mpango Kazi wa kuwahamisha na kulipa fidia waathirika wa mradi (*Resettlement*

Action Plan); Programu ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Development Program*); usanifu wa kuimarisha kingo za Mto Songwe (*River Bank Stabilization*); na Mpango Biashara wa Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Commission Business Plan*). Kazi zote hizo zilikamilika mwezi Septemba, 2015. Aidha, Sekretariati ya Mpito ya Kamisheni tarajiwa imeundwa na makao yake ni Mjini Kyela, Mkoa wa Mbeya.

63. Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya pamoja ya mpito iliyoungwa na nchi za Malawi na Tanzania inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya awali kabla ya kuanzishwa kwa Kamisheni ya Pamoja ya nchi hizo. Hadi mwezi Machi 2016, usanifu wa kina wa miundombinu ya rasilimali za maji na maandalizi ya uwekezaji katika Bonde la Mto Songwe zimekamilika; na utekelezaji wa miradi ya kijamii ya kuhifadhi mazingira unaendelea. Vilevile, Sekretarieti inaendelea na maandalizi ya miradi ya awali ikiwemo mradi wa maji kwa vijiji vilivyopo kwenye Bonde la Mto Songwe utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 1.5** na mradi wa kuandaa Mfumo wa Kuratibu Haidrolojia katika Bonde (*Hydrological Monitoring System*) utakaogharimu **Dola za Marekani 425,000**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itakamilisha taratibu za kuridhia Makubaliano ya kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Bonde la Mto Songwe; pamoja na kushirikiana na Serikali ya Malawi kutafuta wafadhili mbalimbali ili kutekeleza miradi hiyo.

(c) Mamlaka ya Ziwa Tanganyika

64. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Mamlaka ya Bonde la Ziwa Tanganyika ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*), na Zambia katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Tanzania na *DRC* zinamiliki kwa pamoja **asilimia 86** ya Ziwa hilo (*DRC – asilimia 45*; Tanzania – **asilimia 41**; Burundi – **asilimia 8**; Zambia – **asilimia 6**). Kumekuwa na changamoto ya kushuka

kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika hivyo kuathiri miundombinu ya bandari za Kigoma na Kasanga (Tanzania); Kalemie, Uvira na Moba (DRC); Bujumbura na Rumonge (Burundi) na Mpulungu (Zambia) na pia chanzo cha maji kwa Mji wa Kigoma/Ujiji kimeathirika. Kupungua kwa kina cha maji katika ziwa hilo kunahusishwa na kubomoka kwa banio la maji kwenye Mto Lukuga. Jitihada mbalimbali zimefanyika kudhibiti hali hiyo ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa usanifu wa kina wa banio lililobomoka kwenye Mto Lukuga uliofanyika kwa msaada wa COMESA. Mto Lukuga ambao upo nchini DRC ndio pekee unaotoa maji kutoka Ziwa Tanganyika kwenda Mto Congo na hatimaye Bahari ya Atlantic.

65. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza miradi ya kudhibiti kushuka kwa kina cha Ziwa Tanganyika, jumla ya **Dola za Marekani milioni 65** zinahitajika. Mwezi Aprili, 2014 Serikali za Tanzania na DRC zilikubaliana kuwa na mradi wa pamoja wa kuwezesha kina cha maji cha Ziwa Tanganyika kurudi katika hali yake ya kawaida. Mradi huo utahusisha kujengwa kwa banio kwenye Mto Lukuga na uhifadhi wa mazingira kwenye Bonde la Ziwa Tanganyika. Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Serikali hizo ilisainiwa tarehe 7 Mei, 2015. Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zinaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ili kutekeleza mradi huo. Katika mwaka 2016/2017, Tanzania itaendelea kushirikiana na DRC kutekeleza masuala yaliyoainishwa kwenye Hati ya Makubaliano (MoU) ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa banio endapo fedha zitapatikana.

4.2. HUDUMA ZA UBORA NA USAFI WA MAJI

66. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa majukumu ya Wizara ni kuhakiki ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji vijijini na mijini kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira. Katika kutekeleza jukumu hilo,

kwa mwaka 2015/2016 Wizara ilipanga kukusanya na kuchunguza sampuli **10,000** za maji ili kuhakiki ubora wake kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi. Aidha, sampuli **1,500** za majitaka zilipangwa kuhakikiwa ubora wake kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na mfumo wa ikolojia.

67. Mheshimiwa Spika, Wizara ilipanga kuimarisha utendaji kazi wa maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia madawa na vifaa vya uchunguzi pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Katika kutekeleza hayo, Wizara inahakikisha kuwa maabara za maji nchini zinafuatilia na kuchunguza ubora wa maji katika vyanzo na mitandao ya usambazaji maji na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mamlaka za Maji, Vyombo vya Watumiaji Maji, Bodi za Maji za Mabonde, Taasisi pamoja na watu binafsi kuhusu umuhimu wa kuzingatia viwango vinavyokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Takwimu na taarifa zinazopatikana hutumika katika maamuzi mbalimbali ikiwemo utafiti na utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji.

68. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, sampuli **4,520** za maji kati ya sampuli **10,000** zilizopangwa, zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli **3,939** ni za maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani; sampuli **180** kwa matumizi ya viwandani; sampuli **272** ni za kuratibu mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo (mito, chemichemi, maziwa na mabwawa); sampuli **129** kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji, utafiti na ujenzi. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizo na uchambuzi wa hali ya ubora wa maji kwa matumizi mbalimbali ni kama ifuatavyo :-

4.2.1. Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani

69. Mheshimiwa Spika, wananchi wote wa vijijini na mijini wanatakiwa kutumia maji safi na salama ili kulinda afya zao kwa ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Sheria ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009

inavitaka vyombo vinavyohusika na huduma ya usambazaji wa maji nchini kuhakikisha maji yanayosambazwa yana ubora unaokubalika. Hadi mwezi Machi 2016, sampuli **3,939** zilichunguzwa na kati ya hizo sampuli **3,427** sawa na **asilimia 87** zilionesha kuwa maji hayo yalilikidhi viwango vinavyokubalika. Sampuli **512** sawa na **asilimia 13**, maji yake hayakukidhi viwango kutokana na kuwa na kiwango kikubwa cha chumvichumvi maeneo ya Ukanda wa Pwani na *fluoride* katika maeneo ya Igunga, Hai, Rungwe na Isiyu-Shinyanga. Vyanzo vya maji vilivyobainika kuwa na kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride*, wananchi walishauriwa na kuelekezwa namna ya kutumia teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia inayoratibiwa na kituo cha utafiti cha Ngurdoto. Vilevile, ushauri ulitolewa wa kutumia madawa ya kutibu maji yanayokidhi viwango na kukagua mitambo ya kusafisha maji mara kwa mara kwa kuzingatia mabadiliko ya ubora wa maji yanayotokana na vipindi tofauti katika mwaka.

4.2.2. Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda, Umwagiliaji, Ujenzi

70. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ubora wa maji kwa matumizi ya viwandani unazingatiwa, Wizara inaendelea kuhakiki usalama wa maji yanayotumiwa na viwanda vya kusindika vyakula na vinywaji. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya sampuli **180** kutoka viwanda vya samaki katika Miji ya Musoma, Tanga, Bukoba, Mwanza na Dar es Salaam zilifanyiwa uchunguzi wa kimaabara na matokeo ya uchunguzi huo yalionesha maji yanayotumika yanakidhi viwango vinavyokubalika.

71. Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa ubora wa maji ni muhimu pia katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Maji yanayotumika katika shughuli hiyo huhakikiwa ili kubainisha kama yanakidhi viwango vya ubora kwa kuzingatia aina ya udongo na mazao yanayotegemewa kulimwa maeneo husika.

Lengo ni kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao yanayomwagiliwa. Hadi mwezi Machi 2016, sampuli **10** za maji kwa ajili ya umwagiliaji kutoka maeneo ya shamba la Ndolela kijiji cha Mahanje-mkoani Ruvuma zilichunguzwa. Katika uchunguzi huo, sampuli moja haikukidhi ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa kutokana na kiwango kikubwa cha tindikali. Aidha, sampuli **19** za maji yanayotumika katika shughuli za ujenzi zilichunguzwa na kuonesha kuwa kiwango cha madini kilichokuwemo kinakidhi viwango vinavyokubalika. Kwa upande wa utafiti, sampuli **100** za maji zilipokelewa na kuchunguzwa kadri ya hitaji la utafiti husika.

4.2.3. Kuratibu Mwenendo wa Ubora wa Maji katika Vyanzo

72. Mheshimiwa Spika, Sheria Na. **11** ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009 inazielekeza Bodi za Maji za Mabonde kuchunguza na kufuatilia hali ya ubora wa maji katika vyanzo wanavyovisimamia. Hadi mwezi Machi 2016, sampuli za maji **272** kutoka Bodi za Maji za Mabonde zilichunguzwa ili kutoa takwimu zinazotumika katika usimamizi wa rasilimali za maji. Matokeo yalionesha kuwa baadhi ya vyanzo hivyo kuwa vimeathiriwa na uchafuzi na vyanzo vingine vilikuwa na ubora unaokubalika kwa ustawi wa viumbe hai na kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali. Ushauri stahiki ulitolewa kwa Bodi hizo ili kukabiliana na hali hiyo.

4.2.4. Ufuatiliaji na Udhibiti wa Ugonjwa wa Kipindupindu Nchini

73. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu uliotokea mwezi Agosti, 2015 kwenye Mkoa wa Dar es Salaam na kuenea katika mikoa mingine nchini, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na wadau wengine kukagua na kupima uwepo wa vimelea vya vijidudu vya ugonjwa huo katika visima vya maji vinavyotumika kwenye Manispaa za Ilala,

Temeke na Kinondoni. Sampuli za maji zilichukuliwa kutoka visima **108** ambapo kati ya hivyo visima **20** ni vifupi na **88** ni visima virefu. Kwa ujumla visima vingi vilivyopo katika maeneo ya makazi ya watu vimechimbwa bila kufuata Kanuni na Taratibu za uchimbaji wa visima. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha maji ya visima vifupi vyote na visima virefu **46** kutokuwa salama.

74. Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa ubora wa maji kwa maeneo mengine yaliyoathirika na ugonjwa huo uliendelea kufanyika, ambapo vyanzo vya maji katika mikoa ya Mwanza, Mara, Arusha, Manyara, Kagera, Kigoma, Morogoro na Dodoma vilichunguzwa. Jumla ya vyanzo **600** katika Kata **98** kwenye mikoa iliyoathirika vilikaguliwa ambapo matokeo yalionesha kuwa vyanzo ambavyo maji yake ni salama ni chini ya **asilimia 40**. Kutokana na matokeo ya uchunguzi huo, taasisi zinazohusika na usambazaji wa maji zilishauriwa kuimarisha mfumo wa kuratibu ubora wa maji ili kuhakikisha kuwa maji yanayotumiwa na wananchi ni safi na salama. **Jedwali Na. 3** linaonesha vyanzo vya maji vilivyokaguliwa katika mikoa mbalimbali na hali ya ubora wa vyanzo.

4.2.5. Utekelezaji wa Mpango wa Usalama wa Maji (Water Safety Plan) na Mwongozo wa Usalama Mahala pa Kazi

75. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Wizara inayosimamia masuala ya Afya pamoja na **Shirika la Afya Duniani (WHO)** imekamilisha uandaaji wa miongozo ya utekelezaji wa Mpango wa Usalama wa Maji (*Water Safety Plan*) kwa Vyombo vya Watumiaji Maji na Mamlaka za Maji. Miongozo hiyo, inakusudia kuboresha huduma za upatikanaji wa maji safi na salama kwa Mamlaka za Maji na Vyombo vya Watumiaji Maji Vijijini (COWSOs) kuanzia kwenye chanzo cha maji hadi kwa mtumiaji. Kutekelezwa kwa mpango huo, kutaboresha usimamizi wa usalama wa maji katika vyombo hivyo na kuwaepusha wananchi kutumia maji yasiyo salama

pamoja na kupunguza upotevu wa maji katika mifumo ya usambazaji maji. Mpango huo utatekelezwa kwa pamoja na Muongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji (*National Guidelines for Monitoring Drinking Water Quality*).

76. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa miongozo ya usalama wa kufanya kazi nje na ndani ya maabara (*Safety Manual, Safety Policy and Safety Procedure*) ili kukidhi mahitaji ya Sheria ya Afya na Usalama Kazini (*The Occupational Health and Safety Act, 2003*) na *Occupational Health and Safety Assessment Services* (OHSAS 18001:2007). Miongozo hiyo inatumika katika kazi za kila siku za uchunguzi wa ubora wa maji kwenye maabara za Sekta ya Maji nchini kwa lengo la kulinda usalama wa watumishi katika maeneo ya kazi.

4.2.6. Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa kwenye Mazingira

77. Mheshimiwa Spika, majitaka yanayozalishwa viwandani na majumbani na kutiririshwa bila kuzingatia miongozo iliyowekwa ni miongoni mwa visababishi vya uchafuzi wa vyanzo vya maji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, maabara za maji huchunguza viwango vya kemikali ya majitaka hayo na kutoa ushauri kwa mamlaka husika. Hadi mwezi Machi 2016, sampuli **119** za majitaka kutoka Miji ya Morogoro, Mwanza, Iringa, Mbeya na Dodoma; na kutoka viwanda vya samaki, sukari, madawa na tumbaku zilihakikiwa ubora wake. Kati ya hizo sampuli **60** zililenga kuchunguza uwezo wa mifumo ya kusafisha majitaka katika viwanda na miji. Uchunguzi huo ulibaini kuwa sampuli **38** sawa na **asilimia 63** zilizosafishwa na mifumo iliyopo hazikukidhi viwango. Hali hiyo inaashiria umuhimu wa kuongeza jitihada katika ufuatiliaji wa viwango vya ubora wa majitaka yanayotiririshwa kwenye mazingira hususan vyanzo vya maji. Aidha, ushauri wa kitaalam wa kuboresha utendaji wa mabwawa ya majitaka na mitambo ya kusafisha majitaka ulitolewa kwa taasisi husika.

4.2.7. Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji

78. Mheshimiwa Spika, madawa ya kusafisha na kutibu maji yanatakiwa kuwa na ubora unaokubalika kwa kazi zilizokusudiwa. Maabara za maji nchini zimeendelea kuchunguza na kuthibitisha ubora wa madawa hayo. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya sampuli **34** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Mamlaka za Maji za Chalinze, Tanga na Morogoro zilihakikiwa ubora wake. Kati ya sampuli hizo, sampuli za *Polyaluminium Chlorite* (**15**), *Aluminium Sulphate* (**7**), *sodium bicarbonate* (**5**) na *algal Floc* (**2**) ambazo hutumika kusafisha maji; na *Calcium Hypochlorite* sampuli **tano** ambayo hutumika kua vijidudu. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa sampuli zote zilikidhi viwango vinavyokubalika. Aidha, ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi sahihi ya madawa hayo uliendelea kutolewa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuhakiki ubora wa madawa na kukagua ufanisi wa mitambo ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kwa vyombo vinavyotoa huduma ya majisafi vijijini na mijini.

4.2.8. Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika Maji ya Kunywa na Kupikia

79. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mkakati wa usambazaji wa teknolojia ya uondoaji madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kutumia **mkaa wa mifupa ya ng'ombe** (*bone char*) katika ukanda wenye madini hayo. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya mitambo **367** ya ngazi ya kaya imesambazwa katika vijiji vya Engikareet, Oldonyowas, Lemanda, Uwiro na Ngaramtoni katika Mkoa wa Arusha ambapo jumla ya watu **2,202** wamenufaika kwa kupata maji yasiyo na madhara ya madini ya *fluoride*. Vilevile, Kituo cha Utafiti wa Kuondoa Madini ya *Fluoride* cha Ngurdoto kimekamilisha ujenzi wa mtambo wa ngazi ya jamii wa kuondoa madini ya *fluoride* katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya MWEDO. Mtambo

huo umesanifiwa kuhudumia wanafunzi **600** pamoja na watumishi wa shule hiyo na una uwezo wa kuzalisha **lita 4,500** za maji yenye *fluoride* inayokidhi viwango kwa siku.

80. Mheshimiwa Spika, mtambo uliojengwa katika kisima cha maji kinachotumiwa na shule hiyo umeonesha uwezo mkubwa wa kuondoa madini ya *fluoride*. Kiwango cha madini kilichopo kwenye maji ya kisima hicho ni **milligramu 4.2** kwa lita moja na baada ya maji hayo kuchujwa, kiwango cha madini kimefikia **milligramu 0.06** kwa lita moja ya maji. *Bone-char filter media* zilizowekwa kwenye mtambo huo ni **tani 2** ambazo muda wake wa kubadilishwa ni baada ya mwaka mmoja. Vilevile, mtambo huo umewekwa mfumo wa kuuu vimelea vya vijidudu (*UV Disinfection System*) unaotumia nishati ya umeme wa jua au umeme wa kawaida.

81. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa malighafi ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji, vyanzo mbadala vya viambata vinavyotakiwa vimeanza kuchunguzwa ili kubaini wingi na ubora wa viambata hivyo. Maeneo yanayofanyiwa utafiti ni yale yanayosadikiwa kuwa na madini ya *phosphate* yanayotumika kutengeneza kiambata kinachojulikana kama *artificial hydroxyl apatite*. Maeneo ambayo yamefanyiwa utafiti huo ni Mbeya (Mlima Panda), Ileje (Mlima Chamoto), Morogoro (Mlima Wigu) ambapo sampuli zimechukuliwa na kupelekwa *Geological Survey- Dodoma (GST)* kuchunguza viwango vya *phosphate* vilivyomo na uwepo wa madini yenye madhara kwa afya, matokeo yake ndio yatatao uwezekano wa uzalishaji wa *artificial hydroxyl apatite*.

82. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza uelewa na maarifa kwa wananchi juu ya matumizi bora ya teknolojia hiyo, elimu imetolewa kwenye maeneo ya Ngarenanyuki na Uwiro mkoani Arusha. Vilevile, kituo cha utafiti kimetoa elimu kwa kikundi maalumu cha vijana *Mtoshu Ant Fluoride Water Organization*. Kikundi hicho kinashiriki kutoa elimu kwa umma

kuhusiana na madhara ya madini ya *fluoride* na kuhamasisha utumiaji wa *Bone-char filter media* ili kuepuka athari za madini hayo hasa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa kusambaza teknolojia ya *Bone-char filter media* katika maeneo yaliyoathirika na madini ya *fluoride* na kutayarisha ramani (*fluoride map*) ili kutambua maeneo yenye kiwango kikubwa cha *fluoride* katika maji. Taarifa hizo ni muhimu katika kuibua miradi ya maji na aina sahihi ya teknolojia katika uendeshaji.

4.2.9. Maabara za Maji kupata Ithibati (Accreditation)

84. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuziwezesha maabara za maji nyingine kupata ithibati (*accreditation*), Maabara za Maji za Dar es Salaam na Iringa zinaendelea na taratibu za kuziwezesha kupata ithibati katika vipimo vya kemikali (*Chemical analysis to ISO/IEC 17025: 2005*). Katika kutekeleza hayo, maabara hizo zimejengewa uwezo wa kuandaa miongozo ya usimamizi (*Quality Management System*) inayobainisha namna kazi za Maabara zitakavyofanyika ili kukidhi vigezo vya kupata ithibati. Aidha, maabara ikishapata ithibati inapaswa kufanyiwa ukaguzi, hivyo Maabara ya Maji Mwanza ilifanyiwa ukaguzi (*assessment – “TEST-5 0011”*) na SADCAS mwezi Novemba, 2015 na kuidhinishwa kuendelea na ithibati.

85. Mheshimiwa Spika, maabara za maji hushiriki zoezi la kimataifa la kujipima uwezo ambalo huratibiwa na Shirika la Maji la Namibia (*NAM WATER PT Provider-Namibia Water Corporation*) chini ya mpango wa *Southern Africa Development Community Measurement Traceability (SADCMET)*. Katika mwaka 2015/2016, maabara zote **16** zilishiriki zoezi la kujipima uwezo wa utendaji kazi kwa kupima vimelea vya vijidudu (*bacteria*) kwenye maji na maabara **11** (Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya, Arusha, Tanga, Kigoma, Musoma,

Mtwara, Mwanza na Dodoma) zilishiriki kwenye zoezi la kupima viashiria (*parameters*) vya kemikali. Tathmini ya matokeo ya majaribio hayo katika upimaji wa vimelea vya vijidudu kwa maabara hizo ilikuwa ni kati ya **asilimia 60** hadi **asilimia 100** na upande wa kemikali ni **asilimia 60** hadi **asilimia 85**. Matokeo hayo yanaonesha kuwa Maabara zetu zina uwezo mkubwa wa kupima viashiria na vimelea vya vijidudu.

4.2.10. *Mapitio ya Viwango vya Maji na Majitaka*

86. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha viwango vya maji na majitaka vilivyopo ili viendane na mahitaji ya ukuaji wa maendeleo, kuepusha uchafuzi wa vyanzo vya maji na kupunguza athari za uharibifu wa mazingira, Wizara ilifanya mapitio ya viwango hivyo mwezi Oktoba 2015. Viwango ya maji vilivyopitiwa na kuandaliwa rasimu ni kwa ajili ya:- majitaka yanayotirirshwa (*effluents*), vyanzo vya maji vinavyopokea (*receiving waters*), umwagiliaji (*irrigation*), ufugaji wa samaki (*aquaculture*) na ujenzi (*construction*). Rasimu za viwango zimewasilishwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa majumuisho na kupata maoni ya wadau wa Sekta za Maji na Umwagiliaji.

4.2.11. *Ujenzi na Ukarabati wa Maabara za Maji*

87. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na kusogeza huduma ya masuala ya ubora wa maji karibu na wananchi, Wizara inaendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya maabara ili yakidhi viwango vinavyotakiwa ili kukidhi matakwa ya ISO 17025:2005. Hadi mwezi Machi 2016, ujenzi na ukarabati wa majengo hayo yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

- (i) Ujenzi wa maabara za Kigoma, Singida na Shinyanga unaendelea ambapo Kigoma umefikia wastani wa **asilimia**

90, Singida wastani wa **asilimia 60** na ukarabati wa jengo la maabara Shinyanga umefikia wastani wa **asilimia 70**;

- (ii) Ujenzi wa ofisi za Maabara ya Bukoba umekamilika na ujenzi wa majengo ya maabara unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2016;
- (iii) Wakandarasi wa ujenzi wa maabara za Mtwara na Mbeya pamoja na Wakandarasi wa ukarabati wa majengo ya maabara za Songea na Sumbawanga wamekabidhiwa maeneo ya miradi mwezi Desemba, 2015 na kazi hizo zimeanza;
- (iv) Ujenzi wa maabara ya Musoma umefikia **asilimia 70** na kwa maabara ya Mwanza, Mkandarasi amekabidhiwa eneo la mradi na ujenzi umeanza; na
- (v) Ukarabati na upanuzi wa jengo la Maabara Kuu Dar es Saalam ulianza mwezi Julai 2015, ambapo ukarabati wa jengo umefikia **asilimia 45** na upanuzi wa ofisi umefikia **asilimia 55**. Aidha, makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati wa maabara za Morogoro, Dodoma, Tanga na Arusha yanaandaliwa na kazi itaanza mwaka 2016/2017.

88. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi wa Ubora wa Maji na Kudhibiti Uchafuzi kwa kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa ubora wa maji na utekelezaji wa miongozo iliyopo. Katika kutekeleza majukumu hayo, sampuli **10,000** za maji na sampuli **1,500** za majitaka zitakusanywa na kuchunguzwa. Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya maabara ili kuboresha mazingira ya maeneo ya kazi hivyo kulinda afya za watumishi.

4.3. HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

89. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, ambayo inajumuisha Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utekelezaji wa programu hiyo ulianza mwezi Septemba, 2007. Hata hivyo, kutokana na taratibu za ununuzi pamoja na upatikanaji wa vibali vya Benki ya Dunia kuchukua muda mrefu, Wataalam Washauri walipatikana mwezi Desemba, 2009. Wataalam hao walianza usanifu wa miradi na kuandaa makabrasha ya zabuni ambapo ujenzi wa miradi ulianza rasmi mwaka 2012. Katika kipindi ambacho taratibu za kuwapata Wataalam Washauri zilikuwa zikiendelea, Serikali na Washirika wa Maendeleo walikubaliana kutekeleza miradi midogo yenye kuleta matokeo ya haraka (*Quickwins Projects*) ambayo gharama yake haikutakiwa kuzidi **Dola za Marekani 50,000** na isiyohitaji Wataalam Washauri, hivyo kuwatumia wataalam waliopo kwenye Sekta.

90. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini unatumia vyanzo vya visima vifupi, visima virefu, mabwawa na maji mtiririko kwenye maeneo mbalimbali nchini. Katika utekelezaji wa Programu Ndogo ya Maji Vijijini kwa kushirikisha mpango maalum wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa” (*Big Results Now - BRN*), jumla ya miradi **1,160** inayotumia vyanzo vya visima virefu, visima vifupi na miradi ya mtiririko imejengwa katika vijiji **1,556**. Miradi hiyo imeongeza vituo **28,499** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia watu **6,707,506**. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya watu **21,907,506** waishio vijijini wanapata huduma ya majisafi sawa na **asilimia 72** ya wakazi wa vijijini. Aidha, miradi ya maji **424** vijijini inaendelea kujengwa na ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo ikikamilika jumla ya wakazi **3,494,038** waishio vijijini watanufaika na huduma ya maji.

4.3.1. Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini

91. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo hayo. Utekelezaji huo unahusisha ujenzi wa miradi ya kimkakati, miradi yenye kuleta matokeo ya haraka pamoja na ukarabati na ujenzi wa mabwawa. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Miradi ya Kimkakati

(i) Mradi wa Maji Tabora

92. Mheshimiwa Spika, mradi huo unatekelezwa katika Mkoa wa Tabora ambapo Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Japan** inaboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika vijiji **19** kwenye Wilaya zote saba za Mkoa wa Tabora. Mradi huo utatoa huduma kwa kujenga visima **114** vya pampu za mkono na miradi **minne** ya maji yenye mtandao wa kusambaza maji kwenye vituo vya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2016, uchimbaji wa visima umefanyika katika maeneo mbalimbali ambapo visima **84** sawa na **asilimia 74** ya malengo vimepata maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu. Visima **22** vilikuwa na maji yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu.

93. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miradi ya mtandao wa kusambaza maji unaendelea katika Vijiji vya Mabama na Mpumbuli Wilaya ya Uyui, Kijiji cha Kakola Wilaya ya Tabora na Kijiji cha Isanga Wilaya ya Nzega. Ujenzi wa Mradi katika Kijiji cha Mabama (Wilaya ya Uyui) umefikia **asilimia 96.5** na Kijiji cha Kakola (Manispaa ya Tabora) **asilimia 95.9** ambapo kazi iliyobaki ni kufunga pampu. Utekelezaji katika Kijiji cha Isanga ni **asilimia 54.9** na Kijiji cha Mpumbuli ni **asilimia 85.2**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016 na utawanufaisha zaidi ya wakazi **40,352** wa Wilaya hizo.

(ii) Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe

94. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe utakuwa na uwezo wa kuhudumia watu **456,931** katika Wilaya za Same (watu **264,793**), Mwanga (watu **177,085**) na watu **15,053** katika Wilaya ya Korogwe. Idadi hiyo inahusisha wakazi wa miji ya Same, Mwanga pamoja na vijiji **38** kwenye Wilaya za Same vijiji **16**, Mwanga (**17**) na Korogwe vijiji (**5**). Awamu ya kwanza ya Mradi wa Same-Mwanga-Korogwe inakadiriwa kugharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 41.36** ambapo mchango wa **BADEA (Arab Bank for Economic Development in Africa)** ni **Dola za Marekani milioni 10**, **OFID Dola za Marekani milioni 12** na Serikali **Dola za Marekani milioni 19.36**. Fedha hizo zitatumika kujenga sehemu ya mradi kutoka kwenye chanzo katika bwawa la Nyumba ya Mungu, mtambo wa kutibu maji eneo la Njia Panda na kulaza mabomba makubwa yenye urefu wa **kilomita 12.7** kutoka kwenye chanzo hadi matanki ya kituo cha kusukuma maji.

95. **Mheshimiwa Spika**, awamu ya kwanza ya mradi huo unatekelezwa katika vipande vinne (*4 Lots*). **Kipande cha kwanza (Lot 1)** cha mradi kinajumuisha ujenzi wa chanzo cha maji; chujio la maji katika Kijiji cha Njia Panda; tanki la maji eneo la Kisangara; pamoja na kununua na kulaza bomba kutoka chanzo cha maji kupitia chujio la maji hadi Kijiji cha Kisangara. Katika utekelezaji wa kipande cha kwanza cha mradi, ujenzi wa kambi na ofisi (*Mobilization and Temporary Facilities*) umefikia **asilimia 90** na ujenzi wa miundombinu ya maji (*Permanent Structures*) kwa **asilimia 9**. **Kipande cha Pili (Lot 2)** cha mradi huo kinahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji **9** vya awali. Vijiji hivyo ni Ruvu Mferejini, Ruvu Jiungeni, Handeni, Kiti cha Mungu, Langata Bora, Langata Kangongo, Nyabinda, Kiryana Njia Panda. Kazi za ujenzi wa Kipande hicho bado hazijaanza.

96. Mheshimiwa Spika, kipande cha tatu (Lot 3) cha mradi huo kinahusisha ujenzi wa kituo cha kusukuma maji katika Kijiji cha Kisangara, kulaza bomba toka Kisangara hadi Mwanga mjini kwa kupitia Kiverenge, ujenzi wa tanki la maji na mtandao wa mabomba katika Mji wa Mwanga. Zabuni ya kutafuta Mkandarasi wa ujenzi wa kipande hicho imekamilika na taratibu za kusaini mkataba wa kazi zinaendelea. **Kipande cha nne (Lot 4)** kinahusisha ujenzi wa tanki kuu la Kiverenge, kununua na kulaza mabomba toka Kiverenge hadi Same, ujenzi wa matanki **matatu (3)** pamoja na kulaza mabomba ya kusambaza maji Mjini Same. Zabuni ya kutafuta Mkandarasi wa ujenzi wa kipande hicho imekamilika na taratibu za kusaini mkataba wa kazi zinaendelea.

97. Mheshimiwa Spika, aidha, baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi, Serikali itanza kutekeleza awamu ya pili ya mradi huo itakayohusisha vijiji 29 vilivyobaki vikiwemo vijiji 14 vya Wilaya ya Same; vijiji 10 vya Wilaya ya Mwanga; na vijiji vitano (5) vya Bwiko, Mkomazi, Manga Mtindiro, Manga Mikochei pamoja na Nanyogie katika Wilaya ya Korogwe.

(iii) Mradi wa Maji Masoko - Rungwe

98. Mheshimiwa Spika, mradi wa Masoko ambao ulianza mwezi Septemba 2010, unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Halmashauri ilisitisha mkataba na Mkandarasi kwa kushindwa kutekeleza kazi kulingana na viwango vya usanifu. Kwa sasa Halmashauri imepata mkandarasi mwingine na ujenzi wa kidakio cha maji, ulazaji wa bomba na ujenzi wa matanki mawili yenye mita za ujazo 90 kila moja unaendelea. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 30. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imetenga jumla ya Shilingi milioni 650 kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobaki na kuharakisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Masoko.

(iv) Mradi wa Maji Mkoani Kigoma

99. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ubelgiji** inatekeleza mradi wa maji mkoani Kigoma katika Halmashauri zote za Mkoa. Mradi huo unategemewa kugharimu kiasi cha **Euro milioni 8.8** kati ya fedha hizo **Euro milioni 8** zitatolewa na **Serikali ya Ubelgiji** na fedha inayobaki itatolewa na Serikali ya Tanzania. Mradi utakapokamilika wananchi wapatao **200,000** wanatarajiwa kunufaika na huduma ya maji. Jumla ya vijiji **26** vya kipaumbele vimeainishwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 5.28** zikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

(b) Miradi yenye Kuleta Matokeo ya Haraka (*quickwins*)

(i) Mradi wa Maji kwa Vijiji 100 Vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama-Shinyanga

100. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa vijiji **100** vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga. Mradi huo unahusu uboreshaji wa huduma ya upatikanaji wa maji kwenye vijiji **40** vya awali vilivyotambuliwa katika Halmashauri za Misungwi, Kwimba, Shinyanga na Msalala. Utekelezaji wa mradi umeanza kwa kupima na kufanya usanifu wa miradi katika vijiji **31** kwenye Halmashauri za Msalala na Shinyanga ambapo gharama yake imekadiriwa kufikia **Shilingi bilioni 2.59**. Hadi mwezi Machi 2016, ujenzi wa miradi ya maji umekamilika katika vijiji **11** vya Nyashimbi, Magobeko, Kakulu, Butegwa, Ng'homango, Jimondoli, Kadoto, Lyabusalu, Mwajiji, Ichongo na Bukamna ambapo wananchi wanapata huduma ya maji. Ujenzi unaendelea katika vijiji vya Mwakatola na Mwasekagi katika Halmashauri ya Shinyanga. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi katika Halmashauri za

Wilaya za Msalala na Shinyanga, na kuanza usanifu wa miradi kwenye Halmashauri za Misungwi na Kwimba. Jumla ya **Shilingi milioni 760.67** zimetengwa kwa kazi hizo.

(ii) Mradi wa Maji wa Ntomoko

101. Mheshimiwa Spika, mradi wa Ntomoko unahusisha Halmashauri mbili za Wilaya za Chemba na Kondoa ambapo hapo awali ilipangwa kuvipatia vijiji **18** huduma ya maji ambavyo vinakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji. Hata hivyo kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wakazi katika vijiji vinavyokusudiwa ikilinganishwa na uwezo wa chanzo cha maji kilichopo, ilibainika kuwa vijiji **10** tu vitaweza kupata huduma ya maji kwa ukarabati miundombinu ya maji, matanki ya kuhifadhia maji pamoja na ujenzi wa chujio la maji. Vijiji hivyo ni Makirinya, Kirere cha Ng'ombe, Lusangi, Hamai, Songolo, Madaha, Churuku, Kinkima, Jinjo na Jangalo. Vijiji vilivyobaki vya Jenjeluse, Goima, Mtakuja, Mlongia, Igunga, Itolwa, Mapango na Chandama vilitafutiwa vyanzo vya maji kwa kuchimba visima virefu.

102. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, ukarabati wa chanzo, ujenzi wa chujio la maji na ujenzi wa tanki lenye **mita za ujazo 100** umekamilika. Kazi ya ukarabati wa bomba kuu na mtandao wa mabomba ya kusambaza maji inaendelea ambapo ulazaji wa bomba kuu umefikia **kilomita 16.81** kati ya **kilomita 21** na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umefikia **kilomita 31.45** ikilinganishwa na **kilomita 90** zilizokusudiwa. Vilevile, ukarabati wa matanki **matatu** umekamilika na ukarabati wa tanki **1** unaendelea. Aidha, miradi ya maji ya kusukuma kwa pampu katika vijiji vya Jenjeluse, Goima, Mtakuja na Mlongia imekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji. Uchimbaji wa visima **viwili** katika vijiji vya Mapango na Chandama umekamilika na usanifu ukikamilika, vijiji hivyo vitajengewa miundombinu ya maji.

(iii) Mradi wa Maji Chiwambo, Masasi

103. Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Chiwambo unahusisha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kata **saba (7)** za Lulindi, Lupumbulu, Namalenga, Chiungutwa, Sindano, Mchauru na Mbuyuni katika Wilaya ya Masasi. Mradi huo unalenga kuwanufaisha wananchi wapatao **84,082**. Hadi mwezi Machi 2016, kazi zilizotekelezwa katika Kijiji cha Nagaga kilichopo Kata ya Lulindi ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 5.2**; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa kusambaza maji umbali wa **kilomita 1.3**; ujenzi wa vituo **17** vya kuchotea maji ambao umefikia **asilimia 80**; ujenzi wa tanki kuu la maji la **lita 50,000** ambao umefikia **asilimia 70**; ukarabati wa *sump* ambao umefikia **asilimia 20**; na ukarabati wa nyumba ya pampu ambao umefikia **asilimia 30**. Katika Kijiji cha Milewe kilichopo Kata ya Lulindi, ukarabati wa matanki **mawili** yenye ujazo wa **lita 25,000** na ujenzi wa bomba kuu la maji umbali wa **kilomita 13** umekamilika.

104. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kata ya Chiungutwa ujenzi na ukarabati umeendelea katika Kijiji cha Mpeti ambapo ulazaji wa bomba kuu la maji umbali wa **kilomita 10.5** kati ya **kilomita 23.5** zilizopangwa umekamilika; ukarabati wa tanki la maji **lita 25,000** na ujenzi wa uzio umefikia **asilimia 70**; ujenzi wa vituo **13** vya kuchotea maji umefikia **asilimia 80** na ukarabati wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji umefikia **asilimia 50**. Utekelezaji wa mradi umeendelea katika Kijiji cha Chiungutwa ambapo ujenzi wa vituo **13** vya kuchotea maji umefikia **asilimia 70** na ujenzi wa tanki la maji umefikia **asilimia 45**. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imetenga jumla ya **shilingi bilioni 1** kuendelea kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri ya Masasi.

(c) Ukarabati na Ujenzi wa Mabwawa

105. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uhaba wa maji hususan **maeneo kame** na kwenye vyanzo vyenye uwezo mdogo wa kutoa maji, Wizara imejenga na kuratibu ujenzi wa mabwawa **20** maeneo ya vijijini kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2006/2007 hadi 2015/2016. Kati ya mabwawa hayo, ujenzi wa mabwawa **14** umekamilika na yanatumika. Kazi ya ujenzi wa mabwawa **6** inaendelea na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali.

106. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mabwawa yanayoendelea kujengwa ni Bwawa la Kidete lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Lengo la ujenzi wa bwawa hilo ni kudhibiti mafuriko ya Mto Mkondoa, kilimo cha umwagiliaji na kutoa huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Ujenzi wa bwawa hilo umechukua muda mrefu kukamilika kutokana na matatizo ya kimkataba na kiufundi kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na Mkandarasi. Hatua zinazoendelea kuchukuliwa ni kuandaa mkakati wa muda mfupi na muda mrefu wa kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo.

(d) Uvunaji wa Maji ya Mvua

107. Mheshimiwa Spika, **uvunaji wa maji ya mvua** ni muhimu sana kwa nchi yetu kutokana na hali duni ya upatikanaji wa maji hasa maeneo kame ya vijijini. Uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya majengo ndio njia rahisi ambayo wananchi waishio vijijini wanaweza kuimudu. Serikali imetoa miongozo kwa kila Halmashauri kutunga Sheria ndogo zenye kuzitaka Taasisi za kijamii, Asasi na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya matanki **29,029** yenye ujazo kati ya **lita 1,000** hadi **5,000** yamejengwa kwenye shule, zahanati na taasisi za kijamii katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua.

108. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa mabwawa **6** na ukarabati wa mabwawa **matano**. Aidha, Serikali inaziagiza Halmashauri za Wilaya kuanza kuandaa mpango wa ujenzi wa mabwawa kuanzia ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya zao kwa kujenga bwawa moja au zaidi kila mwaka ili kuvuna maji ya mvua.

4.3.2. Uendeshaji na Matengenezo

109. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha miradi ya maji vijijini inayojengwa inakuwa endelevu katika kutoa huduma kwa wananchi, Serikali imeweka Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wake. Kuundwa kwa Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs) ambavyo vitasimamia miradi hiyo ni mojawapo ya hatua za Serikali katika kutimiza azma hiyo. Wizara imetoa miongozo mbalimbali kwa ajili ya usajili wa vyombo hivyo ikiwemo uteuzi wa Wasajili katika Halmashauri na namna vyombo vitakavyoendeshwa; kuongeza idadi ya wataalam kwenye miradi; na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa skimu za miradi. Wizara imeandaa Mkakati wa Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini (*National Rural Water Supply Sustainability Strategy*) ambao unatekelezwa katika Halmashauri zote kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa miradi hiyo.

110. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, idadi ya vyombo vya watumiaji maji vilivyosajiliwa kisheria imefikia **913**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyombo hivyo, kuhimiza uundwaji zaidi wa vyombo vya watumiaji maji na kusisitiza wasajili kuongeza kasi ya usajili kwa miradi iliyopo na mingine itakayojengwa.

111. Mheshimiwa Spika, katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Serikali imepanga kujenga miradi mipya ya maji vijijini katika vijiji **2,052** itakayokuwa na vituo vya kuchotea maji **38,549**; kukarabati miradi ya maji katika vijiji **1,107** yenye vituo vya kuchotea maji **19,889**; pamoja na kupanua

miundombinu ya maji katika vijiji **946** itakayokuwa na vituo vya kuchotea maji **17,852**. Jumla ya wananchi wapatao **19,080,000** waishio vijijini wanatarajiwa kupata huduma ya maji. Lengo la Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwezi Juni, 2020 **asilimia 85** ya watu waishio vijijini wanapata huduma ya maji.

112. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini unatumia fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:- Mfuko wa Pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Basket Fund*), Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji pamoja na wahisani mbalimbali. Katika mwaka 2015/2016, kiasi cha **Shilingi bilioni 207.8** kilikasimiwa kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili kutekeleza miradi ya maji pamoja na uhamasishaji wa usafi wa mazingira vijijini. Aidha, kiasi kingine cha **Shilingi bilioni 101.7** kilikasimiwa kupitia mafungu ya mikoa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016, **Shilingi bilioni 80.2** zimetumwa katika Halmashauri na Sekretarieti za mikoa kwa ajili ya kuwalipa Wakandarasi na Wataalam Washauri pamoja na gharama za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji.

4.3.3. Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini kwa Mwaka 2016/2017

113. Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi huduma bora ya maji vijijini, Wizara itaendelea na ujenzi wa miradi ambayo haijakamilika, kujenga miradi mipya, kupanua miradi, kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa pamoja na kusimamia na kufuatilia mara kwa mara utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha kuwa inakidhi viwango na ubora kulingana na usanifu na mikataba. Katika mwaka 2016/2017, kiasi cha **Shilingi bilioni 463.30** zimepangwa kutumika kutekeleza miradi ya maji katika vijiji **786** ambapo vituo **14,031** vya kuchotea maji vitajengwa na wakazi wapatao **3,520,250** waishio vijijini watanufaika na huduma ya maji.

114. Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa za matumizi ya nishati ya umeme, jenereta na dizeli katika mitambo ya kusukuma maji, Serikali inahamasisha matumizi ya nishati ya nguvu ya jua pamoja na kurahisisha upatikanaji wa vipuri vinavyotumika katika miradi ya maji. Lengo ni kuwapunguzia wananchi mzigo wa gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi. Vilevile, kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji kwa gharama nafuu na miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu.

115. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 463.30** fedha za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 373.34** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 89.96** ni fedha za nje. **Jedwali Na. 4 (a), (b) na (c)** yanaonesha orodha ya Halmashauri, Mikoa na Miradi iliyotengewa fedha za maendeleo kutekeleza miradi ya maji vijijini katika mwaka 2016/2017.

4.4. HUDUMA YA MAJI MIJINI

116. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kujenga miradi, kukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Wilaya, Miji Midogo, Miradi ya Kitaifa na Jiji la Dar es Salaam. Utekelezaji wa miradi hiyo umeziwezesha Mamlaka hizo kutoa huduma ya majisafi na salama iliyo bora na endelevu, hivyo kuweza kupunguza kero ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi waishio mijini. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

4.4.1. Kuboresha Huduma za Maji Mijini

(a) Miradi ya Maji katika Miji Saba

117. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali kwa kushirikiana na **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD)**, **Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW)** na **Umoja wa Ulaya** imetekeleza miradi katika miji **saba** ya Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Mtwara na Babati. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Manispaa za Bukoba na Musoma

118. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD)**, inatekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika Manispaa za Bukoba na Musoma. Kazi zinazotekelezwa katika miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa mitambo ya kusafisha na kusukuma maji na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji.

119. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Bukoba umekamilika mwezi Februari, 2016 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 31**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 8.82** hadi **lita milioni 18** kwa siku zinazokidhi mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Bukoba. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na **AFD** na **European Investment Bank (EIB)** imekamilisha usanifu wa mradi wa miundombinu ya majitaka kwa Manispaa hiyo. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017, ambapo kwa sasa taratibu za kupata Wakandarasi zinaendelea.

120. Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Musoma unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 40.62**. Hadi

mwezi Machi 2016, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 82** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 10.14** kwa siku kwa sasa hadi **lita milioni 36** ambazo zitakidhi mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Musoma hadi mwaka 2025. Vilevile, usanifu wa mradi wa miundombinu ya majitaka umekamilika, taratibu za kupata mkandarasi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017.

(ii) Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga

121. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya** inatekeleza miradi katika Miji ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga yenye gharama ya **Euro milioni 62.59**. Utekelezaji wa miradi hiyo unahusu uchimbaji wa visima, ujenzi wa mabanio, ujenzi wa matanki, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji, ujenzi wa chujo na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

122. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi wa maji katika Manispaa ya Lindi unatekelezwa kwa gharama ya **Euro Milioni 11.91**. Mradi huo unahusu uchimbaji wa visima virefu **10**; ujenzi wa chujo la maji lenye uwezo wa kusafisha maji **lita milioni 7.5** kwa siku; ujenzi wa matanki **mawili** ya maji ya ujazo wa **lita milioni 3** na **milioni 2**; ulazaji wa bomba kuu la maji umbali wa **kilomita 11.5**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 27**; ujenzi wa **vituo 85** vya kuchota maji; ujenzi wa mabwawa **mawili** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la huduma ya uondoaji majitaka. Hadi mwezi Machi 2016, uchimbaji wa visima **10** vyenye uwezo wa kuzalisha maji **lita milioni 7.5** kwa siku umekamilika. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2016/2017 ambapo utawanufaisha wakazi wapatao **81,343** wa Mji wa Lindi.

123. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Manispaa ya Kigoma, mradi wa majisafi na usafi wa mazingira unatekelezwa kwa gharama ya **Euro Milioni 15.16**. Mradi huo unahusu ujenzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 2**; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji chenye pampu **9**; ujenzi wa matanki **matano** yenye ujazo wa **lita milioni 2** kila moja na tanki moja la **lita 500,000**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 122.8**; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 16.9**; ujenzi wa vituo **200** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la huduma ya uondoaji majitaka. Hadi mwezi Aprili 2016, utekelezaji umefikia **asilimia 54** na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2016. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 65** za sasa hadi **asilimia 95**.

124. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Sumbawanga unatekelezwa kwa gharama ya **Euro milioni 14.99**. Kazi zinazotekelezwa ni uchimbaji wa visima virefu **14**; ujenzi wa *sump* ya ujazo wa **lita milioni 1**; upanuzi wa chujo la maji; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 68** na bomba kuu umbali wa **kilomita 16**; ujenzi wa matanki **6** ya maji yenye jumla ya ujazo wa **lita milioni 7**; ujenzi wa vituo **56** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili** ya kutibu majitaka na ununuzi wa magari **matatu** ya uondoaji wa majitaka. Uchimbaji wa visima vyenye uwezo wa kuzalisha **lita milioni 13** kwa siku umekamilika. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 78** na unatarajiwa kukamilika mwezi **Julai, 2016**. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 62** za sasa hadi **asilimia 100**.

(iii) Manispaa za Mtwara na Babati

125. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ujerumani** kupitia **KfW** itatekeleza miradi katika miji ya

Mtwara na Babati itakayogharimu jumla ya **Euro milioni 18.9**. Kazi zitakazotekelezwa ni ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi; kujenga mabwawa ya kutibu majitaka; kununua magari mawili ya kutoa huduma ya uondoaji wa majitaka (moja kwa kila mji); na ujenzi wa vyoo vya mfano katika baadhi ya shule. Hatua za kutafuta Wakandarasi zimeanza na mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka 2016/2017.

(b) Miradi ya Maji ya Kukidhi Mahitaji ya Muda Mrefu

(i) Mradi wa Maji Tabora

126. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati na upanuzi wa chujo la maji katika kituo cha Igombe Mjini Tabora uliogharimu **Dola za Marekani Milioni 4.74**, umetekelezwa na Serikali kupitia **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji**. Mradi huo ulihusu ujenzi wa chujo la maji, matanki ya maji, ulazaji wa bomba kuu na ufungaji wa pampu. Kwa sasa mradi umekamilika na upo katika kipindi cha matazamiao (*Defect liability period*). Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 15** hadi **lita milioni 30** kwa siku na kukidhi mahitaji ya maji katika Mji wa Tabora ambayo ni **lita milioni 24.5** kwa siku na kuwanufaisha wakazi **247,000**.

(ii) Mradi wa Maji Mjini Dodoma

127. Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Chuo Kikuu cha Dodoma unagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 27.7** na unahusisha kazi zifuatazo:- ujenzi wa matanki makubwa **matatu** yenye jumla ya **lita milioni 12**; ulazaji wa mabomba makubwa ya kusafirisha maji umbali wa **kilomita 12.2** na mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 9.6** kwenye maeneo ya Chuo (Vyuo vya Sayansi ya Jamii, *Informatics*, Elimu na Afya); ujenzi wa kituo cha kusukuma maji (*pumping station*) katika eneo la Makulu pamoja na uwekaji wa umeme; ujenzi wa mtandao wa mabomba makubwa ya kusafirisha majitaka (*main*

trunk sewer) umbali wa **kilomita 18.5**; mabomba madogo ya kukusanyia majitaka (*lateral sewers*) umbali wa **kilomita 8**; na ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka. Ujenzi umekamilika na kwa sasa mradi huo upo katika hatua ya majaribio. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao **100,000** wa eneo la Chuo.

128. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya **Korea Kusini** imekamilisha mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Mji wa Dodoma kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 49.62**. Utekelezaji wa mradi huo ulihusisha ukarabati wa visima **17** na uchimbaji wa visima vipya **viwili** katika eneo la Mzakwe; ulazaji wa bomba la kusafirishia maji kutoka Mzakwe hadi Dodoma Mjini umbali wa **kilomita 47.98**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 32.88** kwenye maeneo ya Nzuguni, Kikuyu na Chidachi; kujenga mfumo mpya wa uendeshaji wa pampu kwenye visima na vituo vya kusukuma maji; ujenzi wa matanki **mawili** katika kituo cha Mailimbili ya ujazo wa **lita 790,000** kila moja; ujenzi wa matanki **mawili** yenye jumla ya ujazo wa **lita milioni 12** katika maeneo ya Imagi na Itega; ujenzi wa maabara ya kisasa ya kupima ubora wa majisafi na majitaka; na ujenzi wa vituo vipya vya kusukuma maji katika maeneo ya Mzakwe na Kilimani. Mradi huo umekamilika mwezi Agosti, 2015 na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 32** hadi **milioni 61.5** kwa siku na kuongeza muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka wastani wa saa **12** hadi **20** kwa siku na kuwanufaisha wakazi wapatao **360,000**.

(iii) Mradi wa Maji Jijini Arusha

129. Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru utagharimu **Dola za Marekani milioni 233.915**. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imefanikiwa kupata mkopo nafuu wa **Dola za Marekani milioni 210.962** kutoka **Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)** na **Dola**

za Marekani milioni 22.953 zilizobaki zitachangiwa na Serikali kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Kazi zitakazotekelezwa ni uchimbaji wa visima; ujenzi wa matanki; ulazaji wa mtandao wa mabomba ya majisafi; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; ujenzi wa mabwawa mapya ya majitaka; ujenzi wa ofisi kuu ya Mamlaka; na ununuzi wa vitendea kazi. Hatua za kuwapata Wataalam Washauri wa kupitia nyaraka za usanifu zimeanza na zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2016. Ujenzi wa mradi huo utanza mwaka 2016/2017 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2019 ambapo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 200** kwa siku. Vilevile, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi utaongezeka kutoka **saa 12** za sasa hadi **saa 24** kwa siku. Aidha, huduma ya uondoaji wa majitaka itaongezeka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**.

(iv) Mradi wa Maji Morogoro Mjini

130. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ufaransa** kupitia **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD)** itatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya majisafi ili kuongeza upatikanaji wa maji utakaokidhi mahitaji ya Mji wa Morogoro. Mradi huo utahusu kuongeza urefu wa tuta la Bwawa la Mindu kwa **mita 2.5** ili kuongeza ujazo wa maji kutoka **lita bilioni 12** hadi kufikia **lita bilioni 20**; upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji ili kuwafikia wakazi wote wa Manispaa ya Morogoro; ujenzi wa chujio la maji lenye uwezo wa kuzalisha **lita milioni 54** kwa siku; na ujenzi wa miundombinu ya majitaka. Taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri wa kupitia usanifu uliofanyika awali na kuandaa gharama mpya za mradi na makabrasha ya zabuni zinaendelea. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017.

(v) Mradi wa Maji Songea Mjini

131. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mradi wa kukarabati chanzo cha Mto Ruhila kilichopo Mjini Songea kwa kujenga banio la maji kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.6**. Kwa sasa mradi upo katika kipindi cha matazamia. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 2.3** hadi **lita milioni 9.6** kwa siku na kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika Kata za Mji wa Songea pamoja na Vijiji vya Mshangano, Mletele na Ruhuwiko ambapo inakadiriwa wakazi **188,422** wananufaika na mradi huo.

(vi) Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma Kupeleka Mtwara-Mikindani

132. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mtwara-Mikindani na vijiji **26** pamoja na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu. Mradi huo utatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka **Serikali ya China** kupitia **China Exim Bank** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 189.9**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo kutoka Mto Ruvuma; chujio la kutibu maji; nyumba ya mtambo wa kusukuma maji; matanki **26**; tanki kuu la ujazo wa **lita milioni 30** ambalo litajengwa eneo la Mangamba; vituo vya kuchotea maji **234**; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 63**. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9** hadi **lita milioni 120** kwa siku na kutosheleza mahitaji ya watu na viwanda mbalimbali vinavyoendelea kujengwa vikiwemo vya saruji na gesi. Kwa sasa, majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na **Serikali ya China** kuhusu mkataba wa maridhiano wa kupata mkopo huo yanaendelea. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017.

(c) Mradi wa Kutoa Maji Kutoka Mto Malagarasi Kwenda Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka

133. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeanza kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Malagarasi kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa miji ya Urambo, Kaliua, Nguruka, Ussoke pamoja na vijiji **68** vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa mitambo ya kutibu majisafi; ujenzi wa matanki ya majisafi; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mto Malagarasi hadi miji ya Urambo na Kaliua; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji kwenye miji hiyo. Mtaalam Mshauri anatarajiwa kukamilisha usanifu wa mradi mwezi Juni, 2016. Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo (AFD) ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo unaotarajiwa kuanza mwaka 2016/2017 na utawanufaisha wakazi wapatao **607,086**.

(d) Mradi wa Maji katika Miji ya Sengerema, Nansio na Geita

134. Mheshimiwa Spika, mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LV-WATSAN II*) katika Miji ya Sengerema, Nansio na Geita unatekelezwa kwa ufadhili wa **Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)** pamoja na Serikali ya Tanzania. Jumla ya gharama za utekelezaji wa mradi huo ni **Dola za Marekani milioni 30.4** ambapo kati ya fedha hizo **AfDB** inatoa **Dola za Marekani milioni 25.8** na Serikali ya Tanzania **Dola za Marekani milioni 4.6**. Mradi huo umelenga kupunguza uchafuzi wa Ziwa Victoria kwa kujenga na kuboresha miundombinu endelevu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji husika. Utekelezaji wa mradi katika Miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mji wa Sengerema

135. Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Sengerema unakadiriwa kugharimu **Shilingi bilioni 20.06**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa kidakio cha maji cha Nyamazugo katika Ziwa Victoria; ujenzi wa matanki **matano** ya kuhifadhi maji yenye jumla ya **lita milioni 2.6**; na kulaza mabomba yenye umbali wa **kilomita 71.3**. Kwa upande wa mradi wa usafi wa mazingira, kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la lyogelo; kujenga vyoo kwenye shule **tatu** za msingi za Ibondo, Ngweli na Mwabaluhi pamoja na kujenga dampo la kisasa kwa ajili ya kutupa taka ngumu eneo la Ibondo. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 70**. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi **138,017** wa Mji wa Sengerema.

(ii) Mji wa Nansio

136. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kujenga miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Nansio unaogharimu **Shilingi bilioni 10.9**. Mradi unahusu ujenzi wa chanzo kipya cha maji; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; ujenzi wa matanki makubwa **mawili**; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 12.6** na mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 46**. Aidha, uboreshaji wa huduma za usafi wa mazingira unahusu ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la Bukongo yenye uwezo wa **lita 50,000**; vyoo **viwili** kwenye shule za msingi za Nansio na Nakoza; na dampo la kisasa la kutupia taka ngumu eneo la Bukongo. Ujenzi wa mradi wa majisafi umefikia **asilimia 80** na ujenzi wa mradi wa usafi wa mazingira umefikia **asilimia 70**. Miradi hiyo itakapokamilika itawanufaisha wakazi **108,653** wa Mji wa Nansio.

(iii) Mji wa Geita

137. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kujenga miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Geita. Mradi huo unagharimu kiasi cha **Shilingi bilioni 6.67**. Kazi zinazotekelezwa ni uchimbaji wa visima virefu **vitatu**; kununua na kufunga mitambo ya kusukuma maji kwenye visima **8**; ujenzi wa matanki **manne** ya maji yenye jumla ya ujazo wa **lita 815,000**; kununua dira za maji **3,608**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 34.62**. Aidha, kwa upande wa kuboresha huduma za usafi wa mazingira mradi unahusu ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la Usindakwe yenye uwezo wa **lita 50,000**, vyoo **viwili** kwenye Shule za Msingi za Mbugani na Nyankumbu, na dampo la kisasa la kutupa taka ngumu eneo la Usindakwe. Mradi huo umefikia **asilimia 50** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2016/2017, na utanufaisha wakazi **135,359** wa Mji wa Geita.

(e) Mradi wa Maji Geita kutoka Ziwa Victoria: Uwekezaji wa Serikali na Mgodzi wa Dhahabu wa Geita (GGML)

138. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Mji wa Geita kwa kushirikiana na Mgodzi wa Madini wa Geita (*Geita Gold Mining Limited – GGML*) imetekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji mjini Geita kwa gharama za **Dola za Marekani milioni 1.4**. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa tanki lenye **lita milioni 1.2**; ulazaji wa bomba umbali wa **kilomita 35.36**; ujenzi wa magati **manne**; na vituo **viwili** vya kujazia maji kwenye magari. Mradi huo umezinduliwa rasmi na **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** tarehe 05 Januari, 2016. Mradi huo umeongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 12.5** hadi **asilimia 36.4**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 2** ili kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Geita. Vilevile, upembuzi

yakinifu na usanifu utafanyika katika Miji ya Mkoa wa Geita ikiwemo Miji ya Geita, Chato na Ushiroambo.

(f) Miradi Mipya katika Eneo la Ziwa Victoria

139. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kwa miji iliyopo eneo la Ziwa Victoria, Wizara inatekeleza miradi mbalimbali ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Mwanza, Bukoba, Musoma, Magu, Misungwi na Lamadi. Miradi hiyo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank-EIB)** na **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (French Development Agency-AFD)** kwa gharama ya **Euro milioni 104.5**. Mchango wa Serikali ni **Euro milioni 14.5**, **EIB** na **AFD** watachangia **Euro milioni 45** kila mmoja. Kwa upande wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi, Mtaalam Mshauri amekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaji wa makabrasha ya zabuni. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017.

(g) Mradi wa Maji Kigoma

140. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **AfDB** inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Kigoma kwa gharama ya **Euro 170,000**. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa tanki la ujazo wa **lita 150,000**; ununuzi wa dira za maji **692**; na ufungaji wa kifaa cha kudhibiti matumizi ya umeme (*power factor correction*). Kukamilika kwa kazi hizo kumeborisha upatikanaji wa huduma ya maji katika eneo la Buronge na kupunguza gharama za umeme. Hadi mwezi Aprili 2016, ulazaji wa bomba kuu umefikia umbali wa **kilomita 6.4** na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umefikia **kilomita 114.7** ambapo ujenzi wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 54**. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2016. Mradi huo utakapokamilika, wakazi wapatao **10,000** wataunganishwa kwenye huduma ya maji safi na salama.

4.4.2. Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi

141. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi ambayo ina uhaba mkubwa wa maji. Utekelezaji wa mradi katika Miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mji wa Mpanda

142. Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Mpanda unaendelea ambapo usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni utakamilika mwezi Juni, 2016. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika majadiliano yanayoendelea na **Serikali ya Austria** ili kupata kiasi cha **Euro milioni 5** za kutekeleza mradi huo. Kazi zitakazotekelezwa ni ujenzi wa vyanzo vya maji, mtambo wa kutibu na kusafisha maji, matanki ya kuhifadhi maji, vituo vya kuchotea maji, na ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **60,000** na kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 38** hadi kufikia **asilimia 72**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **shilingi bilioni 2** ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mpanda.

(b) Mji wa Njombe

143. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha mradi wa maji katika Mji wa Njombe. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa kidakio cha maji na matanki **matatu** ya **lita 135,000** kila moja, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 16.6** na bomba kuu umbali wa **kilomita 14.3**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 3.7** hadi **lita milioni 5.8** kwa siku na kuongeza idadi

ya wakazi wanaopata huduma ya maji kutoka **asilimia 55** hadi **asilimia 79**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuendeleza upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Njombe.

(c) Mji wa Bariadi

144. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Bariadi. Hadi mwezi Machi 2016, kazi zilizotekelezwa ni kuunganisha visima vipya **vitano** kwenye mtandao wa maji; kujenga matanki **mawili** ya maji yenye ujazo wa **lita 135,000** katika eneo la Somanda na **lita 680,000** eneo la Sima; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 11.2** katika maeneo ya Sima, Malambo na Somanda; kujenga nyumba ya mtambo wa kusukuma maji na kulaza bomba kuu la kupandisha maji kwenye matanki; ujenzi wa kituo cha kuchotea maji; na kufunga dira za maji kwa wateja **400**. Mradi huo umefikia **asilimia 75** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Kukamilika kwa mradi huo, kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 30** kufikia **asilimia 75**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2.5** kwa ajili ya kuendeleza upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Bariadi.

4.4.3. Miradi ya Kutoa Maji Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali

(a) Miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi

145. Mheshimiwa Spika, mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Mkoa wa Simiyu unalenga Miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa, Mwanhuzi pamoja na vijiji vipatavyo **253** vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu. Usanifu wa mradi huo utakamilika mwezi Juni, 2016.

Katika mwaka 2016/2017, Wizara itanza ujenzi wa mradi huo utakaogharimu kiasi cha **Euro milioni 313** kwa kutekeleza kazi zifuatazo:- kujenga kidakio cha maji, mitambo ya kutibu majisafi, na tanki lenye ujazo wa **lita milioni 30** eneo la Ngasamo; na ulazaji wa bomba kuu kutoka Ziwa Victoria hadi miji husika pamoja na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji kwenye miji hiyo. Mradi huo utatekelezwa kwa awamu mbili.

146. Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza inalenga kufikisha maji katika Miji ya Busega, Bariadi na Lagangabilili kwa gharama ya **Euro milioni 105**. Kati ya fedha hizo, **Benki ya KfW** ya **Ujerumani** itachangia **Euro milioni 25** na **Euro Milioni 80** zitatolewa na **Green Climate Fund (GCF)**. Taratibu za kuajiri Mtaalamu Mshauri kwa ajili ya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kwa awamu hiyo zinaendelea. Aidha, awamu ya pili inalenga kufikisha maji katika miji ya Mwanhuzi na Maswa kwa gharama ya **Euro milioni 208**, fedha ambazo zitatolewa na **GCF**. Awamu zote za mradi zikamilika zitawanufaisha wakazi wapatao **834,204** wa miji hiyo.

(b) Miji ya Isaka, Kagongwa na Tinde

147. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha usanifu, uandaaji wa makabrasha ya zabuni na uandaaji wa gharama za ujenzi wa mfumo wa usafirishaji na usambazaji maji katika Miji ya Isaka, Kagongwa na Tinde. Kazi hizo zimetetelezwa na wataalam wa **Mamlaka ya Maji KASHWASA** kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Halmashauri za Wilaya husika. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kutumia Wataalam wa ndani itatekeleza ujenzi wa mradi huo kwa kutumia chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria kupitia bomba kuu la **KASHWASA**. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi **183,838** wanaoishi katika miji hiyo pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu.

(c) Miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo

148. Mheshimiwa Spika, mradi huo unatekelezwa na Wataalam wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, *KASHWASA*, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Manispaa ya Shinyanga, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Shinyanga (*SHUWASA*) na kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga. Hadi mwezi Machi 2016, ulazaji wa bomba la kusambaza maji kuanzia Old Shinyanga hadi Maganzo pamoja na Mgodi wa Almasi wa Mwadui umekamilika; na ulazaji wa bomba la kusambaza maji kuanzia Kijiji cha Ikonongo hadi Mji wa Kishapu umeanza ambapo mabomba yamelazwa kwa umbali wa **kilomita 6** kati ya **kilomita 36.5**. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itakamilisha mradi huo ambao utawanufaisha wakazi wapatao **58,155** wa miji hiyo na wakazi wa maeneo yaliyo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu.

(d) Miji ya Tabora, Igunga, Nzega, Sikonge na Wilaya ya Uyui

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha uchambuzi wa awali (*prequalification*) wa Wakandarasi watakaopewa zabuni ya kujenga mradi huo. Mradi huo unahusu upanuzi wa bomba kuu la *KASHWASA* kutoka Kijiji cha Solwa; ulazaji wa mabomba; na ukarabati wa mitandao ya kusambaza maji katika miji ya Tabora, Igunga, Nzega, Sikonge na Uyui; pamoja na kusambaza maji katika vijiji **89** vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2016/2017 ambapo **Serikali ya India** kupitia **Benki ya Exim** itatoa kiasi cha **Dola za Marekani milioni 268.35**.

4.4.4. Miradi katika Jiji la Dar es Salaam

150. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ili kuongeza upatikanaji wa huduma

ya majisafi katika Jiji hilo pamoja na miji ya Kibaha na Bagamoyo. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

151. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili kuhakikisha maji katika Mto Ruvu yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka na kuzalisha umeme wa **megawati 20**. Mradi huo pia unahusu ujenzi wa barabara yenye urefu wa **kilomita 75** kutoka eneo la bwawa la Kidunda hadi Ngerengere na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka bwawa la Kidunda hadi Chalinze. Usanifu wa kazi hizo umekamilika. Gharama ya ujenzi wa mradi inakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 215**. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo zaidi vya fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo. Ili kufanikisha ujenzi wa mradi huo, wananchi walilipwa fidia na kuhamishwa kupisha ujenzi huo na kupelekwa kwenye makazi mapya.

152. Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia makazi kwa waathirika waliopisha ujenzi wa bwawa, Wizara kupitia **DAWASA** iliingia makubaliano na Ofisi ya Mkurugenzi ya Halmashauri ya Morogoro ili kuandaa viwanja **1,000** pamoja na ujenzi wa barabara kwenda katika makazi mapya kwa ajili ya waathirika hao. Gharama ya kazi hiyo ni **Shilingi bilioni 1.31** ambapo malipo ya awali ya **Shilingi milioni 241** kwa ajili ya upimaji viwanja vya makazi mapya yamefanyika. Kwa sasa, Halmashauri inaendelea kuandaa hati ili kuwamilikisha wananchi viwanja hivyo. Kazi ya ugawaji wa viwanja imefikia **asilimia 81** na ujenzi wa barabara kwa ajili ya makazi mapya ya wananchi umefikia **asilimia 90**. Kazi zote zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Aidha, Wizara kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (**DDCA**) imekamilisha uchimbaji wa visima **vitatu (3)** kwenye makazi hayo na sasa **DAWASA** inaendelea na taratibu za kupata *solar pump* ili visima hivyo viweze kutumika. Vilevile, Wizara imeajiri Mkandarasi wa kujenga majengo ya shule,

zahanati na ofisi ya kijiji. Kazi hiyo imefikia **asilimia 72** na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016.

153. Mheshimiwa Spika, ulipaji wa fidia kwa ajili ya watakaohamishwa kupisha ujenzi wa bwawa la Kidunda na njia ya umeme ulikamilika mwezi Septemba 2014. Hata hivyo, wakazi **2,045** kati ya wakazi **2,603** walilalamikia viwango vya fidia waliyopata. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, uhakiki ulifanyika na kubaini kuwa fidia kwa wakazi **1,830** zilikuwa na kasoro na kufanyiwa marekebisho. Baada ya uchambuzi huo, jumla ya fedha inayohitajika kulipa fidia kwa sasa ni **Shilingi 4,026,761,989** na katika mwaka 2016/2017, malipo ya fidia kwa waathirika hao yatafanyika.

(b) Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera

154. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara inaendelea na kazi ya uchimbaji wa visima virefu **20** katika maeneo ya Kimbiji na Mpera ambavyo vinatarajiwa kuzalisha maji **lita milioni 260** kwa siku. Hadi mwezi Machi 2016, Mkandarasi amekamilisha uchimbaji wa visima **tisa** na anaendelea kuchimba visima **vitano**. Kazi ya uchimbaji wa visima vyote **20** itakamilika mwezi Agosti, 2016. Visima hivyo vitahudumia wakazi wa maeneo ya Mkuranga, Kongowe, Chanika, Ukonga, Pugu, Kinyerezi, Mbagala, Kigamboni, Kurasini, Mtoni na Kisarawe.

155. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imekamilisha mradi wa uchimbaji wa visima **saba** vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi katika mwamba wa Kimbiji na Mpera. Visima hivyo vimechimbwa katika maeneo ya Mwasonga, Mkuranga, Kibada, Buyuni, Changani, Chanika na Nzasa-Chanika. Mradi huo umegharimu **Shilingi bilioni 7.54**. Hivi sasa Mtalaamu Mshauri anatomia matokeo ya uchimbaji kutayarisha taarifa ya uchunguzi. Taarifa itakamilika mwezi Juni, 2016 na inatarajiwa kutoa majibu kuhusu

wingi wa maji na mpango wa matumizi endelevu ya chanzo hicho muhimu cha maji chini ya ardhi.

(c) Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu na Ulazaji wa Bomba Kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara

156. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India inatekeleza mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, ulazaji wa bomba kuu la kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tanki jipya la Kibamba. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu uliogharimu **Dola za Marekani milioni 39.7** umekamilika na mtambo upo katika hatua za majaribio. Mradi huo umeongeza uwezo wa mtambo wa kuzalisha maji kutoka **lita milioni 82** hadi **lita milioni 196** kwa siku.

157. Mheshimiwa Spika, kazi za ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tanki jipya la maji la Kibamba kwa ujumla zimegharimu **Dola za Marekani milioni 59**. Ujenzi wa mradi umekamilika mwezi Aprili, 2016 na kwa sasa Mkandarasi anafanya majaribio ya mradi. Kukamilika kwa mradi huo kumepunguza kero ya uhaba wa maji katika Miji ya Mlandizi na Kibaha pamoja na maeneo ya Kiluvya, Kibamba, Changanyikeni, Mbezi, Kimara, Kibangu, Kinyerezi, Makuburi, Tabata, Segerea, Vingunguti, Airport, Ukonga na Kipawa katika Jiji la Dar es Salaam.

(d) Upanuzi wa Mradi wa Maji Ruvu Chini na Ujenzi wa Bomba Kuu la Kusafirisha Maji Kutoka Ruvu Chini kuelekea Matanki ya Chuo Kikuu Ardhi

158. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Shirika la Kimarekani la Millenium Challenge Co-operation (MCC)** imekamilisha upanuzi wa chanzo cha maji cha Ruvu Chini na upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji. Kukamilika kwa upanuzi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 180** hadi

lita milioni 270 kwa siku. Mradi huo umegharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 36.8**. Vilevile, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha mradi wa ulazaji wa bomba la kusafirisha maji umbali wa **kilomita 55.3** kutoka mtambo wa Ruvu Chini hadi matanki ya Chuo Kikuu Ardhi. Mradi huo umegharimu **Shilingi bilioni 141** ambazo ni fedha za ndani na kupunguza kero ya uhaba wa maji kwa wakazi wa maeneo ya Bagamoyo na vitongoji vyake, Bunju, Mabwepande, Boko, Tegeta, Kunduchi, Mbezi Beach, Mbezi Juu, Salasala, Kawe, Makongo, Chuo Kikuu, Mikocheni, Msasani, Masaki, Mwananyamala, Kinondoni, Magomeni, Sinza, Manzese, Ubungo, Mabibo, Kigogo, Buguruni, Ilala, maeneo yote ya katikati ya jiji la Dar es Salaam, Kurasini na Bandarini.

159. Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi hiyo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini tayari baadhi ya maeneo kama vile Segerea, Kimara, Kibangu na Kinyerezi yenye mabomba ya kusambaza maji, maarufu kama “**Mabomba ya mchina**” ambayo yalikuwa hayapati maji, yameanza kupata maji.

(e) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi

160. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi katika Jiji la Dar es Salaam unaohusisha maeneo ya Tegeta hadi Mpiji, Mpiji hadi Bagamoyo na Mbezi hadi Kiluvya kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 32.93**. Hadi mwezi Machi 2016, Mkandarasi amekabidhiwa eneo la mradi na ameanza usanifu wa njia za bomba na matanki. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha Mji wa Bagamoyo na vitongoji vyake, eneo la uwekezaji la Bagamoyo (EPZ), Mpiji, Bunju, Mabwepande, Boko, Mbweni, Tegeta, Ununio, Wazo, Salasala, Kinzudi, Matosa, Mbezi Juu, Goba, Changanyikeni, Makongo, Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Msakuzi, Makabe, Malamba mawili na Msigani.

(f) Mfumo Mpya wa Kusambaza Maji Katika Maeneo Yasiyokuwa na Mtandao wa Mabomba

161. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kulaza mabomba ya kusambaza maji kwenye maeneo yenye uhaba wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo. Usanifu wa mradi umeanza na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2016. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2016/2017 na Wizara imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 44** kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi katika maeneo ya Mkuranga, Chamazi, Msongola, Chanika, Gongo la Mboto, Pugu, Kitunda, Uwanja wa Ndege, Kinyerezi, Vituka, Kiwalani na Vingunguti. Maeneo mengine yatakatunufaiika ni pamoja na Kimbiji, Kibada, Kigamboni, Tuangoma, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Temeke na Bandarini.

(g) Kuboresha Miundombinu ya Uondoaji Majitaka

162. Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mradi wa uondoaji majitaka katika Jiji la Dar es Salaam ili kuongeza wastani wa huduma ya uondoaji majitaka kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 30** ifikapo mwaka 2017. Usanifu na utayarishaji wa vitabu vya zabuni utakamilika mwezi Juni, 2016. Serikali ikishirikiana na **Serikali ya Korea Kusini** itatekeleza ujenzi wa mradi huo kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 89**. Mradi huo utahusu upanuzi wa miundombinu ya majitaka kwenye maeneo ya katikati ya Jiji, ujenzi wa miundombinu mipya katika maeneo ya Ilala, Magomeni hadi Ubungo, Sinza, Kinondoni, Mwananyamala, Oysterbay, Masaki, Msasani, Kawe, Mbezi Beach, Kurasini, Keko, Chang'ombe na Temeke. Vilevile, mradi huo utahusisha ujenzi wa mitambo mitatu ya kisasa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Jangwani, Kurasini na Mbezi Beach. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Korea Kusini** pamoja na **Benki ya Dunia** itatekeleza mradi wa huduma ya

uondoaji majitaka na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uondoaji wa maji ya mvua katika Jiji la Dar es Salaam.

(h) Miradi Mingine ya Maji Jijini Dar es Salaam

163. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wananchi wasiopata huduma ya maji kutoka mtandao wa maji wa *DAWASCO* wanapata maji, Wizara inatekeleza mradi wa visima katika maeneo mbalimbali ya Jiji. Hadi mwezi Machi 2016, visima **52** vimechimbwa na kati ya hivyo visima **32** vinatumika kutoa huduma ya maji. Maeneo yaliyonufaika ni Mavurunza A, Kilungule A, Kilungule B, King'ongo I, King'ongo III, Sandali, Mpogo, Mwemberadu, Mburahati, Kipunguni, FFU Ukonga, Mongo la Ndege, Segerea, Chanika, Yombo, Saranga I, Saranga II, Chang'ombe A, Unubini, Chang'ombe Toroli, Keko Magurumbasi na Keko Mwangi. Utekelezaji wa mradi huo unaendelea katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji hadi miradi ya ujenzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji yatakapofika katika maeneo hayo.

4.4.5. Huduma ya Maji katika Baadhi ya Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo

(a) Miji ya Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo

164. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji midogo ya Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo. Kazi zinazotekelezwa katika miradi hiyo ni uchimbaji wa visima, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji, ufungaji wa umeme kwenye nyumba za mitambo, ujenzi wa matanki na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Utekelezaji wa miradi katika Miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

165. Mheshimiwa Spika, mradi wa maji katika Mji wa Kilosa unaogharimu **Shilingi bilioni 2.57** unaendelea na ukikamilika utawanufaisha wakazi wapatao **32,120**. Hadi mwezi Machi 2016,

ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Kwa Mji wa Turiani, ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 77** na unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.82**. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwaka 2016/2017. Aidha, Wizara imechukua hatua ya dharura ya kujenga vituo vya kuchotea maji ambapo kwa sasa wananchi wananufaika na huduma hiyo wakisubiri mradi mkubwa kukamilika. Mradi huo ukamilika utawanufaisha wakazi **48,113** wa Mji wa Turiani.

166. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa maji katika Mji wa Mvomero unaogharimu **Shilingi bilioni 2.02** unaendelea na ukamilika utawanufaisha wakazi **15,795** wa mji huo. Hadi mwezi Machi 2016, ujenzi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2016/2017. Kwa upande wa Mji wa Gairo, mradi wa maji unaoendelea kujengwa unagharimu **Shilingi bilioni 6.67**. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2016 na kuwanufaisha wakazi **27,180**. Aidha, Serikali imechukua hatua ya dharura ya kupunguza kero ya maji katika Mji wa Gairo kwa kujenga vituo **nane** vya kuchotea maji na kuchimba visima **vitatu** vyenye kuzalisha maji **lita 36,600** kwa saa katika maeneo ya Polisi, Shuleni na Mnadani.

(b) Mji wa Bunda

167. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi wa kuboresha hali ya huduma ya maji katika Mji wa Bunda kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.45**. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa kidakio cha maji; kulaza bomba kuu umbali wa **kilomita 25.4**; ukarabati wa matanki **matatu** yenye ujazo wa lita **225,000** kila moja; na ufungaji wa pampu. Kukamilika kwa awamu hiyo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 1.26** hadi **lita milioni 8** kwa siku na kwa sasa wakazi wa Mji wa Bunda pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ya eneo la bomba kuu wanapata huduma ya maji. Aidha, Mkandarasi anaendelea na

awamu ya pili ya mradi kwa kujenga mtandao wa kusambaza maji pamoja na vituo vya kuchotea maji na utekelezaji umefikia **asilimia 78**. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016 na kunufaisha wakazi wapatao **23,632** wa mji huo. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaanza ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji ili kuhakikisha wakazi wa Mji wa Bunda wanapata maji safi na salama.

(c) Mji wa Mugumu

168. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea na ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji katika Mji wa Mugumu unaogharimu **Shilingi bilioni 1.6**. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 55** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2016/2017. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao **25,000** kwa kupata huduma ya majisafi na salama.

(d) Mji wa Tarime

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na uchimbaji na ukarabati wa visima vya maji pamoja na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Mji wa Tarime kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.2**. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 75** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2016/2017. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao **46,500** kwa kupata huduma ya maji safi na salama. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea na upembuzi na usanifu wa kupeleka maji katika Mji huo kutoka chanzo cha Ziwa Victoria. Aidha, Wizara imetenga **Shilingi milioni 300** katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za upatikanaji wa maji katika Mji wa Tarime.

(e) **Mji wa Orkesumet**

169. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (BADEA)** na **OPEC Fund for International Development (OFID)** inatarajia kujenga mradi wa majisafi utakaohudumia Mji wa Orkesumet. Mradi huo utagarimu **Dola za Marekani milioni 18.4** ambapo BADEA watatoa **Dola za Marekani milioni 8**, OFID watatoa **Dola za Marekani milioni 8** na mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani milioni 2.4**. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2016/2017 na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji katika Mto Pangani eneo la Ruvu; ujenzi wa mtambo wa kutibu na kusafisha maji; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 44**; ujenzi wa matanki **manne** yenye uwezo wa **lita milioni 1.6, lita 150,000, lita 225,000** na **lita 50,000**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 52**; ujenzi wa magati **10** na vituo **nane** vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi huo umepangwa katika vipande viwili (*2 Lots*). Kipande cha kwanza kitahusu ujenzi wa kidakio cha maji na mtambo wa kutibu na kusafisha maji. Kipande cha pili kitahusu ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2017 na utawanufaisha wakazi wapatao **52,000**.

4.4.6. Miradi iliyo Kwenye Hatua ya Usanifu na Kuombewa Fedha katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

170. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa miradi ya maji katika miji mbalimbali. Juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi hiyo zinaendelea. Mchanganuo wa fedha zinazohitajika kutekeleza ujenzi wa miradi husika umeainishwa katika **Jedwali Na 5**. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya India ili kupata kiasi cha **Dola za Marekani milioni**

500 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji katika miradi ya kitaifa na miji mbalimbali. Miradi ya kitaifa itakayonufaika ni Wanging'ombe, *HTM* na Makonde na Miji iliyojumuishwa kwenye ufadhili huo ni Muheza, Kayanga (Karagwe), Makambako, Njombe, Manyoni, Songea, Sikonge, Chunya, Kasulu, Kilwa Masoko, Rujewa, Mugumu (Serengeti), Geita na Zanzibar ambapo wakazi wapatao **3,183,964** watapata huduma ya maji baada ya miradi hiyo kukamilika. **Jedwali Na. 6** linaonesha mchanganuo wa fedha kwa Miji itakayonufaika na ufadhili wa **Dola za Marekani milioni 500** kutoka **Serikali ya India**.

171. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo kwa kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi katika miji hiyo. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 17.4** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. **Jedwali Na. 7** linaonesha mgawanyo wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Miji mingine iliyobaki itatengewa fedha katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

4.4.7. Miradi ya Maji ya Kitaifa

172. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji ya kitaifa ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya miradi hiyo. Kuna jumla ya miradi nane ya maji kitaifa ambayo ni Chalinze uliopo Mkoa wa Pwani, Mugango-Kiabakari (Mara), Makonde (Mtwara), *HTM* (Tanga), Wanging'ombe (Njombe), Maswa (Simiyu), Masasi-Nachingwea (Mtwara/Lindi) na *KASHWASA* (Shinyanga). Kati ya miradi hiyo, miradi ya Masasi-Nachingwea na *KASHWASA* imekamilika. Kazi zinazoendelea kwa miradi iliyobaki zimeainishwa kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Maji Chalinze

173. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha awamu ya pili ya mradi wa maji Chalinze ambao unatoa huduma ya majisafi katika vijiji **47** vilivyopo katika Mkoa wa Pwani (vijiji **42**) na vijiji **vitano** katika Mkoa wa Morogoro. Mradi huo ulitekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na **BADEA** na **Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 53.7** na kuwanufaisha wakazi **197,648** wa wilaya tatu za Morogoro Vijijini, Bagamoyo na Kibaha. Mradi umegawanyika katika vipande **9** na vijiji vinavyonufaika katika kila kipande ni kama ifuatavyo:-

- (i) **Kipande A**, vijiji vya Mihuga, Masimbani, Kweikonje, Mandamazingara na Mkange;
- (ii) **Kipande B**, vijiji vya Masuguru/Mwetemo, Kiwangwa/Mwavi, Fukayosi, Kidomole, Mkenge, Msinune, Pongwe Msungura, Madesa na Makurunge;
- (iii) **Kipande C**, vijiji vya Kinzagu, Makombe, Talawanda, Malivundo, Msigi, Kisanga, Mindukeni, Msanga na Magulumatali;
- (iv) **Kipande D**, vijiji vya Mbala, Chamakweza, Vigwaza, Buyuni na Visezi;
- (v) **Kipande E**, vijiji vya Chahua, Gwata, Gumba, Magindu na Lukenge;
- (vi) **Kipande G**, vijiji vya Kwan'gandu, Pongwe Kiona, Kifuleta na Kwaruhombo; na
- (vii) **Kipande J**, vijiji vya Kidugalo, Ngerengere, Sinyaulime, Bwawani, Gwata, Kinonko pamoja na Kambi za Jeshi za Sangasanga, Kizuka na Kinonko.

Aidha, ujenzi wa **Kipande F&H** unaohusu vijiji vya Msolwa, Mdaula, Matuli, Ubenazomozi, Mwidu, Visakazi, Tukamisasa na Lulenge umekamilika mwezi Aprili, 2016 na upo katika kipindi cha majaribio.

174. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara inaendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa maji Chalinze ulioanza mwezi Julai, 2015 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 41.3**. Kazi zinazotekelezwa ni upanuzi wa kidakio katika chanzo; kujenga matanki ya kuhifadhi maji katika vijiji **20**; kulaza bomba kuu na upanuzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji; kujenga tanki kubwa la kuhifadhi maji katika Mlima Mazizi; na kujenga vituo vya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na huduma ya maji wakati wa ujenzi wa awamu ya I na II. Hadi mwezi Machi 2016, ujenzi wa mantanki umeanza katika vijiji vya Kihangaiko, Pingo, Pera, Bwilingu, Msoga na Mboga. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2017 na utaongeza uzalishaji maji kutoka **lita milioni 7.2** hadi **lita milioni 11** kwa siku. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 3.5** kukamilisha mradi huo.

(b) Mradi wa Mugango - Kiabakari

175. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA)** na **Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (Saudi Fund for Development - SFD)** inatekeleza mradi wa maji wa Mugango-Kiabakari-Butiama kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Hadi mwezi Machi 2016, Mtaalamu Mshauri anaendelea na usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2016/2017 na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; ujenzi wa matanki **matatu**; kulaza bomba kuu kutoka Mugango, Kiabakari hadi Butiama umbali wa **kilomita 32**; kukarabati mitambo ya kusukuma maji ya Kiabakari; na kulaza mabomba ya mtandao wa kusambaza maji kutoka Butiama hadi Bisarye. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapatao **80,000** waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 20** ili kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji

katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa Mugango-Kiabakari.

(c) Mradi wa Makonde

176. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali kwa kushirikiana na **DFID** imekamilisha ukarabati wa visima virefu **sita** eneo la Mitema na kufunga pampu katika visima hivyo. Kukamilika kwa kazi hizo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 7.4** hadi **lita milioni 14.8** kwa siku, hivyo kuboresha huduma ya maji katika baadhi ya maeneo yanayohudumiwa na mradi huo. Aidha, Wizara inaendelea na majadiliano na wadau mbalimbali ambao wameonesha nia ya kuendelea kuboresha huduma ya maji katika Mradi wa Kitaifa wa Makonde. Gharama za kutekeleza kazi hiyo zinakadiriwa kuwa **Euro milioni 89**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa mradi.

(d) Mradi wa Handeni Trunk Main (HTM)

177. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Uholanzi** inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi kwa maeneo yanayohudumiwa na mradi wa kitaifa **HTM**. Mtaalam Mshauri anakamilisha mapitio ya usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni ya mradi kwa gharama ya **Euro 30,000** zilizotolewa na **Serikali ya Uholanzi**. Aidha, Wizara inaandaa taarifa ya athari za kimazingira na kijamii ili iwasilishwe **NEMC** kwa ajili ya kupata kibali cha ujenzi.

178. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi utanza katika mwaka 2016/2017 kwa gharama ya **Euro milioni 60** ambazo zitatolewa na **Serikali ya Uholanzi** ili kutekeleza mradi huo. Kazi zitakazotekelezwa ni ukarabati na upanuzi wa kidakio cha maji kilichopo Mto Pangani; ujenzi wa mitambo ya kusafisha maji; ukarabati wa bomba kuu na matanki; ujenzi wa matanki mapya ya kuhifadhi maji; pamoja na ukarabati na ulazaji wa mtandao wa

mabomba ya kusambaza maji. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 44** ya sasa hadi **asilimia 80**. Vilevile, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kupunguza kero ya uhaba wa maji kwa maeneo yanayohudumiwa na mradi wa *HTM*.

(e) Mradi wa Wanging'ombe

179. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya India** itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika eneo linalopata huduma hiyo kutoka mradi wa kitaifa wa Wanging'ombe pamoja na Mji wa Igwachanya. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 48.99** na unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka 2016/2017. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ukarabati wa chanzo cha Mbukwa na Mtitafu; kulaza bomba kuu kutoka chanzo cha Mbukwa umbali wa **kilomita 112**; ukarabati wa matanki **59**; kulaza bomba kuu kutoka chanzo cha Mtitafu umbali wa **kilomita 15**; ujenzi wa tanki la ujazo wa **lita 200,000** katika eneo la Igwachanya; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya **Shilingi bilioni 3** zimetengwa ili kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa Wanging'ombe kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi mpya.

(f) Mradi wa Maswa

180. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa chujo la maji litakalohudumia miji ya Maswa na Vijiji vya Zanzui, Malita, Bayubi, Dodoma, Hinduki, Mwasita, Mwabayanda, Ng'wigwa na Mwabujiku. Gharama ya ujenzi wa mradi ni **Shilingi bilioni 3.35**. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 32** na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2016. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5.9** hadi **lita milioni 10.37** na kupunguza magonjwa yatokanayo na maji

yasiyo salama. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa kitaifa wa Maswa.

4.4.8. Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini

(a) Ujenzi wa Ofisi za Mamlaka

181. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati. Kukamilika kwa jengo hilo kumeiwezesha Mamlaka hiyo kuhamia kwenye jengo lake na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuokoa kiasi cha **Shilingi milioni 6** kila mwaka ambazo zilikuwa ni kodi ya jengo la Halmashauri ya Mji wa Babati. Aidha, ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Tunduma umefikia **asilimia 70** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2016. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 2.4** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ofisi za Mamlaka za Maji Mijini, zikiwemo Mamlaka za Maji za Geita na Mpanda ambazo zimekamilisha taratibu zote za kuanza kwa ujenzi wa ofisi.

182. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji Mijini ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka hizo, hatimaye Mamlaka ziweze kujijendesha kibiashara pamoja na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

183. Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka 2016/2017 Wizara imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 392.4** fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi ya maji mijini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 240** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 152.4**

ni fedha za nje. Orodha ya miradi itakayotekelezwa mijini kupitia fedha hizo za maendeleo imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 8**.

4.5. HUDUMA YA UMWAGILIAJI

184. Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji unatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme - ASDP*); Mradi wa Kuendeleza Sera na Rasilimali Watu (*Japan Policy for Human Resource Development*); na Mradi wa Kuendeleza Skimu Ndogo za Umwagiliaji (*Small Scale Irrigation Development Project - SSIDP*). Miradi hiyo inatekelezwa kwa njia shirikishi baina ya Wizara kupitia **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Mamlaka za Serikali za Mitaa**.

185. Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya *ASDP* ilikamilika mwezi Juni, 2013 na kwa sasa maandalizi ya awamu ya pili ya programu hiyo yamefikia hatua za mwisho. Katika kipindi cha mpito cha maandalizi ya awamu ya pili ya programu, Serikali kwa makubaliano na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutekeleza miradi ya umwagiliaji na miradi hiyo imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

4.5.1. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (ASDP I)

186. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ambapo ujenzi wa skimu **15** zenye jumla ya hekta **16,048** ambazo zitawanufaisha wananchi **80,240** unatekelezwa. Skimu hizo ni; Ipatagwa, Mbuyuni-Kimani, Kapyo, Chang'ombe, Motombaya, Kongolo-Mswiswi, Gwiri, Mwendamtitu zilizopo Wilayani Mbarali; Cherehani-Mkoga, Idodi, Mapogoro na Pawaga-Mlenge Wilayani Iringa; na Ugala, Karema na Mwamkulu katika Wilaya ya Mpanda. Ujenzi wa skimu hizo umefikia **asilimia 71** na malipo ya

Wakandarasi yamefanyika kwa **asilimia 45**. Aidha, ujenzi wa maghala **8** katika skimu za umwagiliaji za Ngana na Makwale (Wilayani Kyela); Magozi na Tungamalenga (Wilayani Iringa); na Mbuyuni-Kimani, Ipatagwa, Kongolo-Mswiswi na Motombaya (Wilayani Mbarali) unaendelea. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu **103** na maghala **53** pamoja na kuendelea kujenga skimu **37** ambazo ujenzi wake haujakamilika. **Jedwali Na. 9 (a)** linaonesha skimu zitakazofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu na **Jedwali Na. 9 (b)** linaonesha orodha ya skimu zitakazoendelezwa.

187. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi zinazohusiana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha, ukame na mafuriko, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Nishati na Madini; Sekretarieti za Mikoa; Halmashauri za Wilaya; Wakulima; Wafugaji; na Washirika wa Maendeleo itaendelea kujenga **mabwawa ya kuvuna maji ya mvua** kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine kama hatua muhimu ya kukabiliana na changamoto hizo. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa mabwawa **7** ya Itagata Wilayani Manyoni, Dongobesh na Tlawi Wilayani Mbulu, Mitumbati Wilayani Nachingwea, Kasoli Wilayani Bariadi, Kongogo Wilayani Bahi na Lwanyo Wilayani Mbarali ambayo ujenzi wake haujakamilika. Vilevile, upembuzi yakinifu utafanyika kwa maeneo **39** yaliyotambuliwa kuwa na uwezekano wa kujengwa mabwawa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10**.

188. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara itafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 (*The National Irrigation Master Plan, 2002*) ili kuhakiki maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ikizingatiwa kuwa ni takriban miaka 14 imepita tangu zoezi hilo lifanyike. Aidha, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kuongeza vitendea kazi na watumishi,

kwa kuzingatia muundo ulioidhinishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma mnamo mwezi Desemba 2014. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kuwajengea uwezo wakulima na wataalam kuhusu usimamizi na uendeshaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Katika hatua hiyo, Wizara itaanzisha daftari la usajili ambapo kwa mwaka 2016/2017, vyama vipya **100** vya wamwagiliaji katika skimu za wakulima wadogo vitasajiliwa na vyama **442** vilivyopo vitaimarishwa. Aidha, wataalam **294** watapewa mafunzo ya usimamizi wa ujenzi, uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji.

189. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara itafanya utafiti ili kubaini teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi zaidi katika matumizi ya maji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija ya mazao. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imepanga kuanzisha kituo cha mafunzo na utafiti wa teknolojia mbalimbali za umwagiliaji.

4.5.2. Mradi wa Kuendeleza Sera na Rasilimali Watu (Japan Policy for Human Resources Development - PHRD)

190. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji** na kwa kushirikiana na **Serikali ya Japan** iliendelea kutekeleza mradi wa **PHRD** kwa kujenga maghala **6** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.78** ili kuhifadhi mpunga kwa lengo la kuongeza thamani katika skimu mbalimbali. Skimu hizo ni Lekitatu iliyopo Wilaya ya Arumeru, Uturo (Mbarali), Mombo (Korogwe), Bagamoyo BIDP (Bagamoyo), Mkindo (Mvomero) na Mkula Wilayani Kilombero. Ujenzi ulianza mwezi Agosti, 2015 na hadi mwezi Aprili 2016, utekelezaji ulifikia **asilimia 40**. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa maghala hayo.

Vilevile, mafunzo kuhusu Kilimo Shadidi cha Mpunga (*Systems of Rice Intensification – SRI*); usimamizi na uendeshaji wa maghala; upatikanaji wa masoko; mikopo kutoka taasisi za kifedha; na uendeshaji wa vyama vya wamwagiliaji yalitolewa. Mafunzo hayo yaliwahusisha viongozi wa skimu na wakulima viongozi **454** pamoja na wakulima wadogo **1,410** kutoka katika skimu **20** za umwagiliaji na Maafisa Ugani **65**.

4.5.3. Mradi wa Kuendeleza Zao la Mpunga (Expanded Rice Productivity Project - ERPP)

191. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na **Benki ya Dunia** itatekeleza mradi wa **ERPP** unaolenga kuongeza uzalishaji na tija kwa zao la mpunga katika skimu **6** za umwagiliaji zenye jumla ya **hekta 2,249** na kunufaisha wakulima **11,245**. Mradi huo utagharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 4.66** na utatekelezwa katika Mkoa wa Morogoro katika skimu za Kigugu na Mbogo Wilayani Mvomero; Msolwa Ujamaa na Njage (Kilombero); na skimu za Mvumi na Kilangali Wilayani Kilosa. Katika kutekeleza mradi huo kazi zitakazofanyika ni pamoja na mapitio ya usanifu, ukarabati wa skimu na kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu kilimo shadidi cha mpunga (*SRI*).

4.5.4. Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (Small Scale Irrigation Development Project - SSIDP)

192. Mheshimiwa Spika, Serikali iliingia makubaliano ya kupata mkopo wa masharti nafuu kutoka **Serikali ya Japan** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu **119** za wakulima wadogo katika Halmashauri za Wilaya **68** nchini. Utaratibu wa utoaji wa fedha unafuata mfumo wa Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund - DIDF*) ambapo fedha za ujenzi hupelekwa katika Halmashauri husika. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya **32** imeendelea

kusimamia ukarabati wa skimu **45** za umwagiliaji za awamu ya kwanza zenye jumla ya **hekta 13,722** katika Halmashauri hizo. Hadi mwezi Machi 2016, utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 94** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa skimu **63** zitakazopewa fedha katika awamu ya pili ya mradi huo.

4.5.5. Programu ya Kukabiliana na Changamoto za Uhaba wa Chakula Duniani (Feed the Future)

193. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Marekani** inatekeleza Programu ya *Feed the Future* inayolenga kukabiliana na changamoto za uhaba wa chakula duniani kwa kuongeza uzalishaji na tija, kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chakula na kuimarisha huduma za masoko ili kuinua kipato kwa wananchi wa vijijini. Programu hiyo, imelenga kuendeleza miradi ya umwagiliaji na barabara za kuunganisha masoko katika Mkoa wa Morogoro ambapo ukarabati wa mradi wa Dakawa wenye jumla ya **hekta 2,000** umeanza. Vilevile, upembuzi yakinifu, usanifu na tathmini ya athari za kimazingira kwa mradi wa Mgongola wenye jumla ya **hekta 680** umekamilika.

4.6. TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

4.6.1. Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji

194. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji (*National Water Investment Fund - NWIF*) umeanzishwa chini ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 (Kifungu 44(1)). Mfuko huo ni Taasisi yenye jukumu la kukusanya mapato, kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi yake. Lengo kuu la Mfuko ni kuwekeza (*Provisions of "investment support"*) kwenye miradi ya huduma ya maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidakio vya maji, kipaumbele ikiwa ni kwenye maeneo yenye uhaba

mkubwa wa huduma ya maji hususan maji vijijini. Mfuko utasaidia kuwekeza katika ujenzi wa **miradi ya maji vijijini**; upanuzi wa **miradi ya maji mijini**; pamoja na usimamizi na uendelezaji wa **vyanzo vya maji** ili kuboresha upatikanaji wa huduma endelevu ya maji nchini. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Mfuko utajikita zaidi katika kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

195. Mheshimiwa Spika, Mfuko huo unasimamiwa na Bodi ya Wadamini inayoteuliwa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Bodi hiyo inajumuisha Wajumbe wa Bodi wanne akiwemo Mwenyekiti; na Mwakilishi kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji, OR-TAMISEMI, na Wizara ya Fedha na Mipango. Majukumu ya Bodi ni kuteua Afisa Mtendaji Mkuu (CEO) pamoja na Sekretarieti kwa ajili ya usimamizi wa kazi za kila siku za Mfuko; kuidhinisha fedha za miradi ya maji na kuhakikisha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kulingana na vigezo na mwongozo wa utoaji fedha; kutoa ushauri kwa Wizara na Wadau wa Mfuko kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa miradi; kuchukua hatua stahiki kwa wakiukaji wa masharti ya misaada ya fedha iliyotolewa; na kuwasilisha kwa Waziri taarifa za Hesabu za mwaka za Mfuko kwa ajili ya kuziwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu (Kifungu 46 cha Sheria **Na. 12** ya mwaka 2009).

196. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria **Na. 12** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, vyanzo vya mapato vya Mfuko ni fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Hadi sasa, chanzo pekee cha mapato ya Mfuko ni tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya petroli. Mapato hayo yametokana na Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 kuifanyia marekebisho Sheria ya Mafuta na Tozo za Barabara, Sura ya 220 inayoelekeza tozo hiyo iwekwe kwenye Mfuko huo. Makadirio kutokana na chanzo hicho yanaonesha kuwa Mfuko utakuwa unapokea kiasi cha **Shilingi bilioni 99** kwa mwaka.

197. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, Mfuko umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 107.3** kutoka tozo ya mafuta na kuzielekeza fedha hizo kwenye utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, madeni ya Wakandarasi wanaoendelea na ujenzi wa miradi ya maji vijijini ni **Shilingi bilioni 373** na wastani wa mahitaji ya fedha za uwekezaji wa miradi mipya ya maji vijijini kwa mwaka ni **Shilingi bilioni 354**. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita 2012/2013 - 2014/2015, mahitaji ya fedha kwa ajili ya miradi ya maji vijijini pekee ilikuwa ni **Shilingi trilioni 1.577** ambapo fedha zilizoidhinishwa ni **Shilingi bilioni 593** na fedha zilizotolewa ni **Shilingi bilioni 306**. Hivyo, kumekuwa na upungufu wa **Shilingi trilioni 1.271** kwa ajili ya miradi ya maji vijijini iliyopangwa kutekelezwa katika kipindi hicho.

198. Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato bado havikidhi mahitaji yaliyopo ya uwekezaji kwenye miradi ya maji. Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa kuwa na vyanzo vya ziada vya mapato ili kuboresha huduma ya maji nchini. Kwa sasa Wizara inaendelea na majadiliano na Mamlaka husika ili kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato vya Mfuko. Endapo Serikali itaridhia mapendekezo yaliyowasilishwa ya vyanzo vya ziada vya mapato ya Mfuko, zaidi ya **Shilingi bilioni 304** zinatarajiwa kupatikana katika mwaka 2016/2017 na kuwezesha utekelezaji wa miradi mingi zaidi ya maji vijijini. Miradi hiyo itatoa huduma ya majisafi na salama kwa wakazi wengi zaidi vijijini na mijini. Hivyo, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji utawezesha utekelezaji wa miradi mingi ya maji na kunufaisha watu wengi zaidi waishio vijijini na mijini. Kwa mantiki hiyo, Serikali itaongeza kasi ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama na kufikia lengo la **asilimia 85** ya watu wanaoishi vijijini na **asilimia 95** kwa wakazi wa mijini ifikapo mwaka 2020.

4.6.2. Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

199. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ina majukumu ya kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao. Kwa mujibu wa Sheria **Na. 11** ya *EWURA* ya mwaka 2001, inaitaka *EWURA* kudhibiti utoaji wa huduma kwenye Sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na usafi wa mazingira nchini. Kwa upande wa Sekta ya Maji, *EWURA* inadhhibiti huduma za upatikanaji wa maji na uondoaji majitaka katika Mamlaka **130** za majisafi na usafi wa mazingira nchini. Kati ya hizo, Mamlaka **23** ni za Miji Mikuu ya Mikoa; Mamlaka **97** za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo; *DAWASA*; *DAWASCO*; na Mamlaka za Miradi **nane** ya maji ya Kitaifa.

200. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, *EWURA* ilipokea maombi ya kubadilisha bei za majisafi na majitaka kutoka Mamlaka **23** za Majisafi na Usafi wa Mazingira na ilitathmini na kuidhinisha bei za Mamlaka **17** za Arusha, Babati, Bukoba, Chalinze, *DAWASA*, Moshi, Mpwapwa, Iringa, Kahama, Kiomboi, *KASHWASA*, Mbinga, Mwanza, Ngudu, Njombe, Kongwa na Shinyanga. Tathmini ya maombi ya bei za maji inaendelea kwa Mamlaka **6** za Dodoma, Igunga, Kilwa Masoko, Kisarawe, Morogoro na Singida. Vilevile, *EWURA* ilikagua miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na majitaka katika Mamlaka **43** za maji mijini ili kuhakiki viwango vya huduma vinavyotolewa na Mamlaka hizo, kupima ubora wa maji, kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kibiashara na utekelezaji wa maagizo ya *EWURA*. Mamlaka za maji hujulishwa kuhusu matokeo ya ukaguzi huo ili waweze kuzifanyia kazi kasoro zilizojitokeza na kuongeza ufanisi. Matokeo ya ukaguzi pia hujumuishwa katika ripoti ya utendaji kazi wa Mamlaka kwa ajili ya ufuatiliaji wa *EWURA*, Wizara ya Maji na Umwagiliaji na OR-TAMISEMI.

201. Mheshimiwa Spika, EWURA imechapisha matokeo ya ufuatiliaji wa utendaji wa mamlaka kwa mwaka 2014/2015 kwenye ripoti maalum za huduma ya majisafi na usafi wa mazingira. Ripoti hizo ni za aina mbili ambazo ni; Ripoti ya Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa na Miradi ya Kitaifa; na Ripoti ya Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo. Ripoti hizo husaidia mamlaka za maji kulinganisha utendaji wake na mamlaka nyingine na kutambua mapungufu yake; kuifahamisha Serikali kuhusu utendaji wa mamlaka ili ichukue hatua stahiki; na kuwafahamisha wateja na wananchi kwa ujumla kuhusu utendaji wa Mamlaka zinazowahudumia. Taarifa ya utendaji wa Mamlaka kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, inaonesha kuwa ufanisi wa mamlaka umeongezeka katika kufunga dira za maji, uwezo wa kumudu gharama za uendeshaji, kuongezeka kwa idadi ya wateja wa majisafi na majitaka, kuongezeka kwa wastani wa saa za upatikanaji wa huduma ya maji na ukusanyaji wa maduhuli. Changamoto bado zipo kwenye vyanzo vya maji visivyotosheleza mahitaji ya sasa na ya baadae na upotevu wa maji. Vilevile, *EWURA* ilipokea jumla ya malalamiko **7** yaliyohusu ankara za majisafi na majitaka zilizokosewa, ukosefu wa maji, kukatiwa huduma ya maji kimakosa na huduma hafifu kwa wateja. Kati ya malalamiko hayo, **6** yamepatiwa ufumbuzi na **moja** lililobaki liko katika hatua ya utatuzi.

202. Mheshimiwa Spika, EWURA kwa kushirikiana na Umoja wa Wadhibiti wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika "*Eastern and Southern Africa Water and Sanitation Regulators Association (ESAWAS)* imetayarisha ripoti ya kwanza inayolinganisha hali ya utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya nchi za Kenya, Rwanda, Zambia, Msumbiji, Lesotho na Tanzania ambapo Shirika la Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam - *DAWASCO* lilishirikishwa. Kwenye ripoti hiyo, upotevu wa maji umeonekana kuwa ni changamoto kubwa kwenye Mamlaka za Maji za nchi hizo.

203. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta za Umeme, Petroli na Gesi Asilia, *EWURA* imeendelea kusimamia Sekta hizo ili kuhakikisha uwepo, ubora na usalama wa huduma hizo kwa kuandaa kanuni na taratibu zinazovutia uwekezaji. *EWURA* imetoa leseni **5** kwa wawekezaji wa miradi midogo ya umeme isiyozidi Megawati **10** ambazo ni Uzia *Small Hydro Power* (1.12MW) ya Uzia – Sumbawanga; Ulaya *Hydro and Windmill Technology Ltd*/Kalumbaleza *Small Hydro Power* (1.2MW) ya Kalumbaleza – Sumbawanga; *TEXPOL Development Co. Ltd* (6.2MW) ya Dar es Salaam; *EA-Power Ltd* (10MW) ya Kiwira – Mbeya; na *Tangulf Express Ltd* (10MW) ya Songea - Ruvuma.

204. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, *EWURA* imetoa leseni **96** kwa vituo vipya vya mafuta, leseni za biashara ya kuagiza kwa jumla mafuta ya petroli kwa kampuni mpya **8**; leseni **4** za uagizaji na usambazaji wa jumla wa vilainishi (*Lubricants*); leseni **moja** kwa kiwanda chenye miundombinu ya mafuta kwa ajili ya matumizi binafsi (*Consumer Installation Licence*); na vibali **15** vya kuruhusu ujenzi wa miundombinu mipya ya petroli (*construction approvals for new petroleum handling infrastructures*). Vilevile, Mamlaka imehuisha jumla ya leseni **138** baada ya kujiridhisha kuwa wamiliki wa leseni hizo wametimiza masharti ya leseni zao ikiwemo kuboresha vituo vya mafuta kufikia viwango stahiki. Aidha, *EWURA* imeendelea kupanga bei kikomo za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayouzwa kwenye vituo vya mafuta na kupima ubora wa mafuta hayo. Lengo ni kuhakikisha kuwa mtumiaji anauziwa mafuta yaliyo bora na kwa bei ambayo si zaidi ya bei kikomo. Vilevile, *EWURA* imeendelea kukagua miundombinu ya kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia ili kubaini kuwa ni salama kwa matumizi na mazingira.

205. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, *EWURA* iliendelea kutunga kanuni na miongozo ya kuimarisha uelewa kwa watoa huduma na umma kuhusu nyenzo za udhibiti ikiwemo ubora wa huduma inayotakiwa kutolewa na taratibu mbalimbali

zinazotumika kwenye udhibiti ili kuimarisha utawala bora. Kanuni na miongozo iliyotungwa ni pamoja na Mwongozo wa Kukagua Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (*Inspection Manual for Water Utilities*); Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Biashara (*Revised Business Planning Guidelines*); na Mwongozo wa Kufuatilia Ubora wa Maji na Uondoaji wa Majitaka katika Mamlaka (*Water and Wastewater Quality Monitoring Guidelines for Water Utilities*).

206. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, *EWURA* imelenga kuimarisha udhibiti wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira nchini kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: kushamirisha uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta za Nishati na Maji; kutekeleza ujenzi wa ofisi ya *EWURA*; kuanzisha ofisi za kanda ya kaskazini (Arusha) na nyanda za juu kusini (Mbeya); kufuatilia utendaji wa Mamlaka za Maji Mijini kwa kuchambua na kuhakiki taarifa za utendaji kazi wa Mamlaka hizo; kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kibiashara (*Business Plans*) ya mamlaka kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na *EWURA*; na kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kiudhibiti, haki na wajibu wa watumiaji wa huduma zinazotolewa na Mamlaka.

207. Mheshimiwa Spika, *EWURA* ni Mamlaka ya udhibiti wa Sekta kuu mbili za Nishati na Maji. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, nimeagiza *EWURA* iendeleze ushirikiano wa karibu kwa kupokea na kutekeleza miongozo inayotolewa na Wizara zinazosimamia Sekta hizo kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

4.6.3. Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji

208. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji hapo awali kilijulikana kama Chuo cha Maji cha Rwegarulila na kilianzishwa mwaka 1974. Chuo hicho kilikuwa kikiendeshwa kwa kutegemea ruzuku ya Serikali kupitia Wizara

ya Maji na Umwagiliaji ambapo kuanzia tarehe 22 Agosti 2008, Chuo kimebadilishwa kuwa Wakala wa Serikali ili kuweza kujiendesha na kujitegemea. Mabadiliko hayo yalitokana na maboresho kwenye Sekta ya Utumishi wa Umma ambayo yalilenga kuboresha utoaji wa huduma bora na kupunguza utegemezi kwa Serikali. Majukumu ya Chuo ni kuendeleza na kutoa wataalamu wanaohitajika katika Sekta ya Maji na Umwagiliaji kwa njia ya mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa kuzingatia Sera na Miongozo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi (NACTE).

209. Mheshimiwa Spika, Chuo kinaongozwa na Mkuu wa Chuo na kusimamiwa na Bodi ya Ushauri ya Wizara (*Ministerial Advisory Board*) ambayo ina majukumu ya kutoa ushauri kwa Waziri kuhusu uendelezaji na usimamizi wa Sera; kuandaa mpango mkakati na biashara wa Chuo na bajeti yake; kuweka vipaumbele na kutoa malengo ya utendaji ya kila mwaka; kupokea taarifa za utendaji za kila mwaka na taarifa za mapato na matumizi ya Chuo; kutoa tathmini ya utendaji wa Chuo; kuidhinisha mishahara na stahili mbalimbali za watumishi; na kutoa ushauri kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Wakala **Na. 30** ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake.

210. Mheshimiwa Spika, Chuo kinatoa mafunzo katika fani **tano** kwa ngazi ya Stashahada na fani **moja** katika ngazi ya Shahada. Fani zitolewazo katika ngazi ya Stashahada ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*); Haidrolojia na Hali ya hewa (*Hydrology and Meteorology*); Haidrojiolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*); Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*); pamoja na Teknolojia ya Maabara na Uboru wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation Engineering*) hutolewa. Vilevile, Chuo kinatoa mafunzo

ya muda mfupi kulingana na mahitaji ya wadau kwenye Sekta ya Maji. Udahili wa wanafunzi umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 11**.

211. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Chuo kilidahili wanafunzi **394** wa stashahada na wanafunzi **193** wa shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji na hivyo kufikia jumla ya wanafunzi **1,472** waliopo Chuoni. Kati ya hao, wanafunzi **1,099** wako katika mafunzo ya ngazi ya Stashahada na wanafunzi **373** ni wa ngazi ya Shahada. Aidha, jumla ya wanafunzi **8** wa Cheti na **280** wa Stashahada katika fani mbalimbali walihitimu mafunzo yao mwezi Novemba 2015.

212. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kwenye masomo ya sayansi, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*), kwa mwaka 2015/2016 ilifadhili wanafunzi wa kike **80** katika mafunzo ya awali ya kuwawezesha kujiunga na masomo ya Stashahada (*pre-entry course*) ikilinganishwa na wanafunzi **41** mwaka 2014/2015. Ufadhili huo umechangia kuongezeka kwa wanafunzi wa kike katika ngazi za Stashahada na Shahada kutoka wanafunzi **226** mwaka 2014/2015 hadi **342** mwaka 2015/2016, sawa na **asilimia 23** ya wanafunzi wote. Aidha, Mfuko wa Mafundi Sanifu (*Water Technicians Fund*) umefadhili jumla ya wanafunzi **306** mwaka 2015/2016 ikilinganishwa na wanafunzi **212** waliofadhiliwa mwaka 2014/2015.

213. Mheshimiwa Spika, ili Chuo kiweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi kimechukua hatua mahsusi za kuboresha mazingira ya ufundishaji kwa programu zilizopo. Kipaumbele kikubwa kimekuwa katika kukarabati miundombinu iliyopo, kuweka vifaa katika maabara, na kutilia mkazo utafiti pamoja na utoaji wa ushauri wa kitaalamu. Msaada mkubwa katika utekelezaji wa azma hii umetokana na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Kwanza chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

214. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Chuo kimefanya maboresho ya miundombinu mbalimbali ikiwemo ukarabati wa majengo ya Maabara ya Udongo, *Plumbing and Pumps workshop*, *Land Survey* na maabara ya Ubora wa Maji. Kazi ya usanifu wa jengo la ghorofa sita lenye madarasa, maabara, kumbi za mihadhara, ofisi na maktaba; na usanifu wa ukarabati wa majengo ya chuo na nyumba za waalimu umekamilika. Ukarabati wa vyumba **vitano** vya maabara na kantini ya wanafunzi umefanyika. Ununuzi na ufungaji wa vifaa kwenye maabara na viyoyozi katika maktaba umefanyika. Katika kuboresha matumizi ya TEHAMA Chuo kimeunganishwa na mkongo wa Taifa (*Government Fibre Optic network*). Vilevile, Chuo kilipokea na kuzifanyia uchunguzi sampuli za maji **172** na kutoa ushauri kwa wahusika. Aidha, Chuo kilifanya utafiti wa Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini mkoani Dodoma (*Sustainability of Rural Water Supply Services*).

215. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Chuo kinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, kimeendelea kuajiri ambapo hadi mwezi Machi 2016, Chuo kina jumla ya watumishi **92**. Kati ya hao **59** ni wakufunzi na **33** ni watumishi katika utawala. Kwa sasa, uwiano kati ya wakufunzi na wanafunzi ni **1:25** ambao ni sawa na kiwango kinachopendekezwa na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi. Vilevile, katika mwaka 2015/2016, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi ambapo jumla ya watumishi **21** wanaendelea na masomo ya muda mrefu. Kati ya hao, watumishi **7** wako katika masomo ya shahada ya uzamivu (*PhD*); watumishi **11** kwenye masomo ya shahada ya uzamili (*Masters*); **wawili** ngazi ya shahada na mtumishi **mmoja** ngazi ya stashahada.

216. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, lengo la Chuo ni kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka **587** hadi **800**. Vilevile, kimepanga kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa sita; kukarabati majengo; kuongeza vifaa vya kufundishia katika maabara; ununuzi wa vitabu; pamoja na kufanya utafiti katika

masuala ya upotevu wa maji kwenye Mamlaka za Maji na uendelevu wa miradi ya maji vijijini.

4.6.4. Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)

217. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) iliendelea kuchimba visima na kujenga mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Machi 2016, Wakala umechimba jumla ya visima virefu **185** na kufanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **129** kwa ajili ya uchimbaji wa visima. **Jedwali Na. 12** linaonesha orodha ya visima vilivyochimbwa na DDCA hadi mwezi Machi 2016.

218. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wakala umekamilisha mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika jengo la Ikulu ndogo ya Chamwino Dodoma, na ujenzi na ukarabati wa Bwawa la Olyapasei kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo lililopo Wilaya ya Kiteto Mkoa wa Manyara. Vilevile, Wakala uliendelea na ujenzi na ukarabati wa Bwawa la Tuliila lililopo Wilaya ya Mbinga Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kufua umeme ambalo limefikia **asilimia 99**; Bwawa la Lipokela (Songea - Mkoa wa Ruvuma) kwa ajili ya umwagiliaji ambalo limefikia **asilimia 95**; Bwawa la Matwiga (Chunya - Mkoa wa Mbeya) kwa ajili ya matumizi ya binadamu ambalo limefikia **asilimia 90**; na Bwawa la Kwamaligwa lililopo Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo ambalo limefikia **asilimia 90**. Aidha, upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Mfili katika Halmashauri ya Mlele (Katavi) na ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji katika Wilaya ya Musoma Vijijini (Mara) umefanyika. Ujenzi wa mabwawa mengine **matatu** ya Habiya lililopo Wilaya ya Itilima Mkoa wa Simiyu, Sekeididi (Kishapu - Mkoa wa Shinyanga) na Mbangala lililopo Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya utanza mwezi Juni, 2016 baada ya kipindi cha mvua kumalizika.

219. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa umepanga kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **200** nchini, kuchimba visima **400**, kukarabati visima **50**, kufunga pampu za maji **30**, kujenga na kukarabati mabwawa ya ujazo wa kati **matano**, usanifu wa udongo maeneo **matano** na kujenga mifumo midogo ya usambazaji maji maeneo **matano**. Wakala unatarajia kukusanya **Shilingi bilioni 10.75** zitakazotokana na mapato ya utekelezaji wa miradi hiyo.

4.6.5. Bohari Kuu ya Maji

220. Mheshimiwa Spika, Bohari Kuu ya Maji imeendelea kutekeleza majukumu ya kuhakiki na kusimamia ubora wa vifaa na nyenzo kwa watekelezaji wa miradi ya maji nchini; na kusambaza mabomba na viungio vyake kwenye miradi mbalimbali ya maji nchini. Katika mwaka 2015/2016, mabomba yalisambazwa kwenye Mamlaka za Maji za Singida, Babati, Wanging'ombe, Chalinze, Chamwino, Tanga, Mtwara, Dodoma, Kondo, Namanyere, Makonde, Igunga, Kigoma, **KASHWASA**, Morogoro, Kilindi, Lindi, Njombe, Karatu, Maswa, Kibiti, Bukoba, Mugumu, Iringa, **DAWASA** na **DAWASCO** na kwenye Halmashauri za Wilaya hapa nchini. Vilevile, Bohari iliwasiliana na wadau mbalimbali wanaotengeneza na kuuza vifaa vya maji ndani na nje ya nchi ili kuweza kujihakikishia kuwa vifaa bora vinapatikana kwa ajili ya miradi ya maji nchini. Lengo likiwa ni kununua vifaa vya maji kwa wingi (*bulk procurement*) vyenye ubora na gharama nafuu.

221. Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi 2016, upatikanaji wa vifaa na nyenzo za maji ulikuwa wa kuridhisha ambapo Bohari ilisambaza vifaa vya kutekeleza miradi ya maji kwenye Mamlaka mbalimbali ikiwemo mabomba yenye jumla ya **kilomita 150,000**, viungio mbalimbali vya miundombinu ya maji na dira za maji **70,000**. Mchango huo wa Bohari katika kutekeleza miradi ya maji umeongeza ufanisi kwenye utoaji wa huduma ya maji kwa

wananchi. Vilevile, Bohari imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka Sekta Binafsi katika kutekeleza Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*) kwa lengo la kuboresha upatikanaji na usambazaji wa vifaa ili kuimarisha Bohari na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

222. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeanza ujenzi wa maghala na Ofisi za Bohari Kuu ya Maji katika eneo la Boko baada ya kuhamishiwa eneo hilo kutoka Kurasini ili kupisha uwekezaji katika Bandari. Ujenzi wa uzio na ukarabati wa ghala **moja** umekamilika. Mtaalamu Mshauri wa kuandaa usanifu na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati wa maghala mengine mawili na ujenzi wa ofisi amepatikana na ujenzi utianza katika mwaka 2016/2017.

4.7. MASUALA MTAMBUKA

4.7.1. Sheria

223. Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam **Na. 20** ya mwaka 2001, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, **Na.11** ya mwaka 2009, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, **Na. 12** ya mwaka 2009, na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji **Na. 5** ya mwaka 2013, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sheria hizo. Elimu hiyo ilitolewa kwa Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji na Wadau wengine wa Sekta za Maji na Umwagiliaji pamoja na jamii kwa ujumla kupitia warsha, mikutano, semina, mafunzo, makongamano na vyombo vya habari. Vilevile, Wizara inaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa Sheria hizo na hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wake. Sheria hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Bunge (www.parliament.go.tz) na kanuni za Sheria za Maji zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji (www.maji.go.tz).

224. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imekamilisha kuandaa notisi **moja (1)** ya kuipandisha daraja Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama kuwa daraja A na kuiwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio (*vetting*) na notisi hiyo ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali **Na. 337** la tarehe 21/08/2015. Vilevile, notisi **moja** ya *Water Supply and Sanitation (Moshi Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area) Notice, 2016* imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa.

225. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha kuandaa kanuni **5** na kuziwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio (*vetting*) kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kanuni hizo ni Notisi ya kutangaza vyanzo vya maji vya Mbwinji na Mwena (*The Water Resources Management (Mbwinji and Mwena Springs Protected Zones) Notice, 2016*); Notisi ya kutangaza chanzo cha maji cha Bwawa la Mindu (*Water Resources Management (Mindu Dam Protected Zones) Notice, 2016*); Oda ya kutangaza chanzo cha maji cha Mto Mara (*Water Resources Management (Designation and Declaration of Mara River Water Catchment) Order, 2016*); Oda ya kutangaza chanzo cha maji cha Somoche (*Water Resources Management (Designation and Declaration of Somoche Water Sub Catchment) Order, 2016*); na Oda ya kutangaza chanzo cha maji cha Tobora (*Water Resources Management (Designation and Declaration of Tobora Water Sub Catchment) Order, 2016*).

226. Mheshimiwa Spika, vilevile, maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusu Kanuni **sita (6)** za *The Water Resources Management (Transfer of water use, discharge and groundwater permits) Regulations 2016*; *The Water Resources Management (Control and Management of Storm Water) Regulations 2016*; *The Water Supply and Sanitation (Provision and Management of Sewage and Waste Water Services) Regulations 2016*; *Water Supply and Sanitation (Water Bowsers)*

Regulations 2016; Water Supply and Sanitation (Licensing Board) Regulations, 2016; na DAWASA (Water Bowers) Regulations, 2016 yamekusanywa na kufanyiwa kazi na rasimu zimekamili kwa ajili ya hatua ya kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili zitangazwe.

227. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeendelea kukusanya maoni na kuboresha rasimu za marekebisha ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na.11** ya mwaka 2009, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 na Sheria ya **DAWASA Na. 20** ya mwaka 2001. Maboresho hayo ni pamoja na mapendekezo ya vyanzo vya ziada vya fedha za Mfuko wa Maji unaokabiliwa na mahitaji makubwa ya fedha za kuwekeza kwenye miradi ya maji. Wizara imeandaa andiko kwa ajili ya kupendekeza vyanzo vya ziada vya fedha za Mfuko na kulijadili katika vikao vya wataalam vilivyofanyika katika mwezi Desemba, 2015 na mwezi Machi, 2016. Andiko hilo limewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kujumuisha maoni, ushauri na mapendekezo ya wataalam hao.

228. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara imeendelea kupitia na kutoa ushauri wa kisheria kwenye Mikataba na Randama za Makubaliano ambayo Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni sehemu (*party*) ya mikataba ya makubaliano hayo. Mikataba na Randama za Makubaliano **92** zimepitwa na kutolewa ushauri na baadae kuwasilishwa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio (*vetting*). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefuatilia na kusimamia mashauri **17** yaliyopo mahakamani ambayo yapo katika hatua tofauti na kati ya hayo, mashauri **mawili** yametolewa uamuzi.

229. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea na utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji kutegemeana na

mahitaji ya Sheria. Vilevile, Wizara itaendelea kukamilisha mapendekezo ya kurekebisha Sheria za Maji na kutoa ushauri wa kisheria kwa wadau wa Sekta za Maji na Umwagiliaji pale inapohitajika.

4.7.2. Habari, Elimu na Mawasiliano

230. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea kutoa elimu na taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta za Maji na Umwagiliaji kutokana na umuhimu wake kwa jamii kama njia mojawapo ya kuelimisha masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na uendelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji nchini. Aidha, Wizara ilishiriki Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kitaifa mkoani Dar es Salaam mwaka 2015. Katika maonesho hayo, Wizara ilipata tuzo **mbili** na kutunukiwa vyeti ambapo ilikuwa mshindi wa kwanza katika kutekeleza masuala ya UKIMWI mahala pa kazi, na kuwa mshindi wa pili katika kutekeleza masuala ya jinsia pamoja na cheti cha banda bora.

231. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara ilishiriki katika maonesho ya Nanenane ambayo yalifanyika Kitaifa Mkoani Lindi mwezi Agosti, 2015 na kufanikiwa kuwa mshindi wa pili katika kuelimisha umma. Maadhimisho hayo hutumika na wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji kuelimisha umma kuhusu kazi zinazotekelezwa na Sekta. Aidha, Wizara iliandaa vipindi **15** vya mahojiano kwenye luninga vya ana kwa ana (*Live talk shows*), makala **8** za luninga na vipindi **5** vya redio vilivyolenga kufafanua masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Maji, na machapisho mbalimbali ya rasilimali za maji, ubora wa maji na utunzaji wa vyanzo vya maji. Vilevile, rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano (*Draft Communication Strategy*) kuhusu Sekta ya Maji ambao utatumika kama mwongozo wa shughuli zote za habari na mawasiliano Wizarani imeandaliwa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itakamilisha Mkakati wa Mawasiliano na kuendelea kuelimisha wananchi kuhusu Sekta za Maji na Umwagiliaji kupitia

makala, vipindi kwenye luninga na redio pamoja na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta.

4.7.3. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

232. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea na juhudi za utekelezaji wa Serikali Mtandao ili kuboresha utoaji wa huduma. Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA, Wizara imekamilisha rasimu ya mpango mkakati na miongozo ya matumizi ya TEHAMA; imeboresha Mfumo wa Kielektroniki katika ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi, na utayarishaji wa ramani za vituo vya kuchotea maji vijijini (*Water Point Mapping System*). Vilevile, majaribio ya matumizi ya ujumbe mfupi kwa simu za viganjani katika kuboresha upatikanaji wa taarifa za miradi ya maji vijijini yamefanyika Wilayani Bunda na kuonesha mafanikio na yataendelezwa kwenye Halmashauri zote nchini. Aidha, Wizara imeimarisha mfumo wa kielektroniki wa Menejimenti ya Takwimu na Taarifa (*Water Sector Management Information System*) ili kusaidia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na miradi kwenye Sekta ya Maji.

233. Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara imeanza kutumia huduma za mawasiliano kwa njia ya ujumbe mfupi kupitia simu za viganjani (*GovSMS*) iliyosanifiwa na Wakala wa Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma; mawasiliano ya simu yaliyounganishwa kwenye miundombinu ya mtandao wa intaneti (*IP Telephony*) ili kupunguza gharama za matumizi; na barua pepe ya Serikali katika mawasiliano ya kiofisi yaani '*Government Mailing System*'. Vilevile, Wizara imeshiriki katika kutekeleza Mpango wa '*Open Data*' ili kuwezesha utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Maji kwa uwazi; na jumla ya watumishi **641** kutoka taasisi zinazotekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji nchini walipata mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kielektroniki.

234. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa habari na mawasiliano kwa kuunganisha Ofisi za Wizara Makao Makuu na Taasisi zake kupitia miundombinu ya mtandao wa Serikali; kutumia teknolojia ya ujumbe mfupi wa simu za viganjani katika kupata taarifa za vituo vya maji vijijini; kukamilisha usanifu wa mfumo wa kielektroniki wenye lengo la kuoanisha mifumo ya kielektroniki inayotekelezwa ndani ya Sekta ya Maji (*Integrated Information Management System for the Water Sector*); kuandaa miongozo ya TEHAMA kwa ajili ya Sekta ya Maji ili taasisi zote zilizo chini ya Wizara ziwe na mifumo au miradi ya TEHAMA; kutekeleza Mpango wa 'Open Data' kwa ajili ya utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Maji; na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi katika matumizi ya TEHAMA. Vilevile, Wizara itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa utunzaji na ufuatiliaji wa mafaili na majalada ili kuboresha huduma na kupunguza gharama za uendeshaji.

4.7.4. Jinsia

235. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo imeendelea kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume. Uwiano huo unazingatiwa kwenye maeneo ya vyombo vya maamuzi katika usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa miradi nchini. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imeshiriki katika Kongamano la Siku ya Wanawake Duniani lililofanyika kitaifa tarehe 08/03/2016 mkoani Dar es Salaam. Vilevile, Wizara inazingatia suala la kurithishana madaraka (*succession plan*) kwa kuangalia sifa za miundo na kuweka kipaumbele hususan kwa wanawake wenye sifa, elimu na weledi na imeendelea kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili kufikia uwiano wa hamsini kwa hamsini ifikapo mwaka 2030.

4.7.5. UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY)

236. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi mbalimbali za kukabiliana na janga la ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) mahala pa kazi. Juhudi hizo ni pamoja na kusambaza mwongozo wa UKIMWI na MSY uliotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Waraka unaoweka wazi huduma zinazotakiwa kwa watumishi wanaoishi na VVU kwa kuzingatia kiwango cha fedha kwa ajili ya lische bora. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imetoa mafunzo kwa Menejimenti kuhusu tafsiri ya mwongozo na waraka unaohusu UKIMWI na MSY, pamoja na elimu kuhusu magonjwa sugu kama vile Kisukari, Kiarusi, Shinikizo la damu, Uzito uliozidi na Kansa. Vilevile, mafunzo kwa waelimishaji rika **25** yalitolewa kwa kada mbalimbali na kuwapatia Jarida la kufundishia watumishi wengine (*Training Manual*) kama mojawapo ya vitendea kazi.

4.7.6. Maendeleo ya Rasilimali Watu

237. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukabiliana na upungufu wa wataalam wa Sekta ya Maji. Katika mwaka 2014/2015, Wizara ilipata kibali cha kuajiri wataalam **475** wa Sekta ya Maji ambapo hadi mwezi Aprili 2016, wataalam **395** (Wahandisi **132** na mafundi sanifu **263**) wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi. Kati ya wataalam hao, **282** walipangiwa Ofisi za Mikoa na Halmashauri; na **113** walipelekwa katika Bodi za Maji za Mabonde, Miradi ya Kitaifa, Mamlaka za Maji na wengine kubaki Makao Makuu ya Wizara. Katika kibali hicho, Wizara bado inasubiri kupata watumishi **80** kutoka Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Aidha, kutokana na upungufu mkubwa wa wataalam hususan katika kada ya mafundi sanifu, Wizara imeomba kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi na Utawala Bora ili iweze kuajiri wataalam wa Sekta ya Maji kutoka vyuoni hasa Chuo cha Maji bila kupitia Sekretarieti ya Ajira.

(a) Kuwajengea Uwezo Watumishi

238. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa Watumishi wa miaka mitatu (2014/2015 hadi 2016/2017), Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya Watumishi **249** wamegharamiwa mafunzo mbalimbali yakiwemo ngazi ya Stashahada watumishi **watatu**, Shahada (**12**), Uzamili (**28**), Uzamivu (**3**) pamoja na watumishi **203** wa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili kuongeza ufanisi wa kutekeleza majukumu yao.

(b) Ujenzi wa Ofisi za Wizara

239. Mheshimiwa Spika, majengo ya ofisi za Wizara kwa sasa yapo katika eneo la hifadhi ya Barabara ya Morogoro ambapo Wizara inatakiwa kupisha upanuzi wa barabara hiyo. Upanuzi huo utasababisha **asilimia 60** ya majengo yanayotumika kwa sasa kubomolewa. Katika kukabiliana na hali hiyo, mwezi Aprili 2015, Wizara ilianza mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara la ghorofa **14** ambalo lipo katika makutano ya Barabara za Sam Nujoma na Chuo Kikuu. Ujenzi wa jengo hilo unagharimu **Shilingi bilioni 37.5** (bila VAT). Hadi mwezi Aprili 2016, ujenzi umefikia ghorofa ya **nne** na utakamilika mwezi Aprili, 2017.

4.7.7. Mapambano Dhidi ya Rushwa

240. Mheshimiwa Spika, Wizara imetekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaloelekeza kila Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali kuwa na simu za kupokea hoja za wananchi na kuzijibu papo kwa papo. Wizara imeanzisha simu za moja kwa moja (*helpline* - **+255 22 2452068; +255 22 2450699**) ambazo hazitozi malipo na kuboresha tovuti kwa ajili ya kupokea malalamiko ya wateja. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imeendelea na

harakati za kupambana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Katika kutekeleza harakati hizo, malalamiko mbalimbali yalipokelewa kwenye Dawati la Malalamiko ambapo **matatu** yalipatiwa ufumbuzi. Vilevile, mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja, yamewasilishwa kwa wadau wa ndani ili kupata maoni yao kabla ya kuanza kutumika. Mkataba huo umezingatia hali halisi ya mahitaji ya sasa katika kutoa huduma na kupunguza mianya ya rushwa.

4.7.8. Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

241. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya maji na usafi wa mazingira na rasilimali za maji zinakuwa endelevu, Serikali ya Awamu ya Tano kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutekeleza miradi ya maji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*). Utekelezaji wa Programu hiyo unazingatia dhana ya ushirikishwaji wa wadau katika uibuaji, usanifu, upangaji, ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji kwa lengo la kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Wadau hao ni pamoja na Halmashauri za Wilaya nchini; Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji; OR-TAMISEMI; Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundu; Taasisi zisizo za Kiserikali; na Washirika wa Maendeleo. Wizara inaratibu utekelezaji wa Programu kwa kuzingatia makubaliano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

242. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa Programu unaleta tija iliyokusudiwa, Wizara inafuatilia kwa karibu utekelezaji wake kwa kutembelea miradi na kuendesha vikao vya ngazi mbalimbali vya kujadili hali ya utekelezaji wa miradi na kutoa ufumbuzi wa changamoto zilizojitokeza. Katika mwaka 2015/2016, ukaguzi wa pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo umetekelezwa kwa miradi iliyopo kwenye Halmashauri mbalimbali na jumla ya vikao **16** vimefanyika

vinavyohusisha wataalam kutoka taasisi zote zinazotekeza Programu. Ili kuhakikisha kuwa viwango na kasi ya utekelezaji wa Programu vinazingatia thamani ya fedha iliyowekezwa (*value for money*), miongozo na ushauri kwa watekelezaji wa Programu ilitolewa kwa wakati. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kuratibu Awamu ya Pili ya Programu pamoja na kutoa taarifa mbalimbali za utekelezaji wake.

(a) Mapitio ya Awamu ya Kwanza ya Utekelezaji wa Programu

243. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji umepangwa kufanyika katika **miaka 20** kutoka mwaka 2006 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025. Awamu ya kwanza ilikamilika rasmi Desemba, 2015 baada ya kumalizika kwa muda wa nyongeza (*additional financing period*) uliokubalika na wadau wote wa programu kwa lengo la kukamilisha miradi ambayo utekelezaji wake ulichelewa. Baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa awamu hiyo ni pamoja na kuanzishwa kwa Bodi ya Taifa ya Maji ambayo inatekeleza majukumu yake ya kumshauri Waziri katika masulala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa rasilimali za maji; na kuandaliwa kwa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa mabonde **6** ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Rufiji, Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Bonde la Kati.

244. Mheshimiwa Spika, vilevile, katika awamu ya kwanza ya Programu vituo **28,499** vya kuchotea maji vimejengwa katika vijiji **1,556** na kuongeza idadi ya watu **6,707,506** wanaoishi vijijini kupata huduma ya maji. Ongezeko hilo limewezesha jumla ya watu **21,910,562** wanaoishi vijijini kunufaika na huduma ya maji safi na kufanya huduma ya maji vijijini kufikia **asilimia 68**. Kwa upande wa Miji Mikuu ya Mikoa, upatikanaji wa huduma ya maji uliongezeka kutoka **asilimia 80** mwaka 2007 hadi **asilimia 86** mwaka 2015; **asilimia 55** hadi **asilimia 72** kwa Jiji la Dar es Salaam; na **asilimia 41** hadi **asilimia 60** kwa Miji Mikuu ya

Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Kampeni ya Kuhamasisha Usafi wa Mazingira (*National Sanitation Campaign*) imetekelezwa katika Vijiji **6,184** ambapo Vitongoji **17,220** vimesaini makubaliano ya **kuachana na tabia ya kujisaidia katika mapori** na maeneo ya wazi na kuanza kutumia vyoou.

245. Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yametokana na taasisi zinazotekeleza Programu kujengewa uwezo kwa kupatiwa wataalam; kujengewa ofisi na kukarabati zilizopo; kupatiwa vifaa na vitendea kazi; pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi. Ni dhahiri kuwa mafanikio makubwa yamepatikana katika awamu ya kwanza na tunatarajia mafanikio makubwa zaidi wakati wa utekelezaji wa awamu ya pili.

(b) Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)

246. Mheshimiwa Spika, Serikali na Wadau wa Maendeleo wamekubaliana kuendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2015/2016 - 2019/2020) ambayo imeanza kutekelezwa mwezi Januari, 2016. Inakadiriwa kuwa, jumla ya **Dola za Marekani bilioni 3.3** zinahitajika kufanikisha utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu. Maandalizi ya awamu hiyo yamezingatia mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza pamoja na miongozo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza awamu ya pili.

247. Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira, Wadau wa Sekta wamekubaliana kuwa katika Awamu ya Pili ya Programu, Kampeni hiyo ipewe hadhi ya kuwa programu ndogo na kufanya Awamu hiyo kuwa na jumla ya programu ndogo tano ambazo ni: utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma ya maji vijijini; huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mijini; Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira (inayosimamiwa na Wizara ya

Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto); na kuzijengea uwezo taasisi zinazotekeleza Programu.

248. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu kwa upande wa maji vijijini unalenga kujenga, kukarabati na kupanua miradi ya maji vijijini ambapo vituo **76,334** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia watu **19,080,000** vitajengwa na kufikisha jumla ya vituo **155,934** na kufanikisha lengo la kuwapatia huduma ya maji **asilimia 85** ya wananchi waishio vijijini ifikapo mwaka 2020. Vilevile, kwa upande wa huduma ya maji mijini, Programu imelenga kuongeza hali ya upatikanaji wa majisafi katika Jiji la Dar es Salaam kutoka **asilimia 72** za sasa hadi **asilimia 95**; kwa Miji Mikuu ya Mikoa kutoka **asilimia 86** za sasa hadi **asilimia 95**; na Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa kutoka **asilimia 60** za sasa hadi **asilimia 90**. Aidha, kwa upande wa upotevu wa maji katika maeneo ya mijini, Programu imelenga kupunguza upotevu huo hadi kufikia **asilimia 25** ifikapo mwaka 2020.

249. Mheshimiwa Spika, lengo lingine la Programu ni kuimarisha Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi na jamii kuhusu masuala ya usafi wa mazingira. Vilevile, Kampeni hiyo itahusisha ujenzi wa vyoo bora katika Shule za Msingi na Sekondari. Aidha, awamu ya pili ya Programu imelenga kujenga uwezo wa taasisi zinazotekeleza Programu hiyo kwa kuajiri watumishi wapya, kujenga ofisi, kutoa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau ili kufanikisha utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu hiyo.

5. CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

250. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi katika Sekta za Maji na Umwagiliaji katika mwaka 2015/2016, umekuwa wenye mafaniko makubwa. Mafanikio hayo yametokana na ujenzi wa miradi mipya, ukarabati wa miundombinu iliyochakaa na upanuzi wa miradi ya maji na umwagiliaji kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi. Pamoja na mafanikio hayo, Sekta hizo zimeendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo pamoja na hatua zinazochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

5.1 Madeni Makubwa ya Taasisi na Wakandarasi

251. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malimbikizo makubwa ya madeni ya ankara za matumizi ya maji kutoka baadhi ya Taasisi na Idara za Serikali ambazo hazilipi madeni yao kwa wakati. Hali hiyo imesababisha Mamlaka za Maji Mijini kuwa na mzigo mkubwa wa uendeshaji na matengenezo ya miundombinu. Hadi mwezi Machi 2016, jumla ya madeni hayo yamefikia **Shilingi bilioni 30**. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji inachelewa kukamilika kwa wakati kutokana na malimbikizo ya madai (*Interim Payment Certificates – IPC*) ya Wakandarasi wa miradi. Hali hiyo imesababisha baadhi yao kugoma kuendelea kutekeleza miradi na wengine kujenga miradi hiyo kwa kasi ndogo. Hadi mwezi Machi 2016, Wizara inadaiwa jumla ya **Shilingi bilioni 212.9** ikiwa ni madai ya wakandarasi, watumishi na Taasisi nyingine zinazotoa huduma kwa Wizara.

252. Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo, kwa upande wa madeni ya baadhi ya Taasisi za Serikali na Wakandarasi, Wizara imeanza kulipa madeni ya Wakandarasi wa miradi kuanzia mwezi Januari, 2016. Hadi kufikia mwezi Aprili 2016, jumla ya **shilingi bilioni 107.3** zimelipwa kwa Wakandarasi hao. Vilevile, Mamlaka za Maji zimeagizwa kuanza kutumia huduma ya dira za malipo kadiri unavyotumia (*prepaid*

meters) ili kupunguza tatizo la malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji. Majaribio ya dira za maji za aina hiyo yanaendelea katika baadhi ya maeneo ya Miji ya Dodoma, Dar es Salaam, Moshi na Iringa. Aidha, kwa upande wa madeni ya Wakandarasi, Wizara imeorodhesha madeni yote na kuyawasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uhakiki na malipo.

5.2 Ushiriki Hafifu wa Sekta Binafsi

253. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuongeza ushiriki katika ujenzi, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji na umwagiliaji kupitia Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership – PPP*). Hii ni kutokana na ushiriki wa Sekta hiyo kujikita kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji na umwagiliaji na kuacha suala la uendeshaji na usimamizi kwa Serikali.

Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kuiwezesha Sekta Binafsi kuongeza ushiriki wake katika uendeshaji wa miradi ya maji na umwagiliaji, zikiwemo kutoa elimu kuhusu sheria, kanuni na fursa zilizopo katika Sekta za Maji na Umwagiliaji. Vilevile, Wizara inaendelea kuwajengea uwezo wataalam wake kwa kuwapatia mafunzo yanayohusu Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na kuandaa maandiko ya miradi ya maji na umwagiliaji itakayoendeshwa na Sekta Binafsi.

5.3 Mabadiliko ya Tabianchi

254. Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi yamesababisha vipindi virefu vya ukame na mvua zisizotabirika hali inayochangia kupungua kwa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Hali hiyo inachangia uhaba mkubwa wa maji katika maeneo mengi, hivyo kusababisha wananchi kuvamia maeneo ya vyanzo vya maji kwa ajili ya kuendesha shughuli za kijamii na kiuchumi. Serikali kwa

kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta za Maji na Umwagiliaji, inaendelea kukabiliana na changamoto hizo.

255. Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kujenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya kuhifadhi maji; kutoa mafunzo kwa wataalam na kuelimisha umma ili kuongeza ufahamu kuhusu mabadiliko ya tabianchi; kuhamasisha matumizi ya utalam asilia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kushirikisha wadau mbalimbali katika kutunza vyanzo vya maji kwa kuvitambua na kuviwekea mipaka; kupanda miti kwenye maeneo ya hifadhi za maji; kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na uharibifu wa mazingira kwa kutumia Sheria za Maji na Mazingira na pia kwa kutumia sheria ndogo za Halmashauri; kuandaa na kutekeleza Mipango Shirikishi ya Uendelezaji na Usimamizi wa Rasilimali za Maji (*IWRMD Plans*); kuimarisha Jukwaa la Majadiliano ya Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta ya Maji (*Water Sector Climate Change Coordination Mechanism Dialogue Forum*); na kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi.

5.4 Uendelevu wa Miradi

256. Mheshimiwa Spika, miradi ya maji na umwagiliaji inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa endelevu hivyo kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hali hiyo imesababishwa na mapungufu kwenye uendeshaji na matengenezo ya miradi ikiwa ni pamoja na kutopatikana kwa wakati kwa vipuri vya miradi ya maji; kasi ndogo ya uanzishwaji wa vyombo vya usimamizi wa miradi ya maji na umwagiliaji; na usimamizi hafifu wa makusanyo ya fedha za miradi.

257. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeandaa na inatekeleza Mkakati wa Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini (*National Rural Water Supply Sustainability Strategy*) ambao unasisitiza kuongeza kasi ya uundaji na usajili

wa Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs); kuendelea kuanzisha na kuimarisha Jumuiya za Watumiaji Maji (*Water User Associations – WUAs*); kuimarisha ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu sahihi za vituo vya maji kupitia mfumo wa kompyuta (*Water Point Mapping System-WPMS*); kuanzisha maghala ya kuhifadhi vifaa na vipuri vya maji katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuhakikisha uwepo wa wataalam wa Sekta katika maeneo ya miradi; na kuanzisha daftari la usajili wa vyama vipya vya wamwagiliaji na kuendelea kuviimarisha vilivyopo ili viweze kusimamia na kuendesha miradi ya umwagiliaji nchini.

5.5 Upotevu wa Maji

258. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotevu mkubwa wa maji yanayozalishwa ambao umechangiwa na uchakavu wa miundombinu ya maji, wizi wa maji pamoja na hujuma na uharibifu wa miundombinu ya maji. Hali hiyo imeendelea kuathiri upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Upotevu wa maji katika Mamlaka za Maji kwenye Miji Mikuu ya Mikoa ni wastani wa **asilimia 35** na kwa Jiji la Dar es Salaam pekee ni **asilimia 47**. Viwango hivyo ni vya juu sana ikilinganishwa na kiwango cha **asilimia 20** kinachokubalika kimataifa hivyo kusababisha athari kubwa katika uendeshaji wa miradi ya maji na upotevu wa mapato. Upotevu huo wa mapato umesababisha Mamlaka za Maji Mijini kushindwa kulipia gharama za uendeshaji na matengenezo ya miundombinu na hivyo, Serikali kulazimika kubeba mzigo huo ili kuondoa kero ya uhaba wa maji kwa wananchi.

259. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara inaendelea kurekebisha Sheria za Maji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu wa miundombinu ya maji. Vilevile, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini zinaendelea kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa; kufunga dira za maji kwa wateja wote ili kubaini matumizi yao halisi; kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa

kulinda miundombinu ya maji; na kushirikisha uongozi wa Mkoa, Jeshi la Polisi na wananchi katika kuwabaini na kuwachulia hatua stahiki wanaojihusisha na wizi wa maji na uharibifu wa miundombinu yake. Aidha, katika Jiji la Dar es Salaam Kikosi Maalum cha Wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya Dola, kinaendelea kuwabaini wezi wa maji na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria. Hadi mwezi Aprili 2016, kuna jumla ya kesi **75** zilizopo mahakamani ikilinganishwa na kesi **163** mwezi Aprili 2015. Kupungua kwa kesi hizo kumetokana na baadhi ya watuhumiwa kukubali kulipa malimbikizo ya madeni yao ikijumuishwa na faini.

5.6 Upungufu wa Wataalam

260. Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upungufu wa wataalam katika Sekta za Maji na Umwagiliaji unaosababishwa na Serikali kutokuajiri kwa muda mrefu, kuongezeka kwa idadi ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri, pamoja na kustaafu au kufariki kwa baadhi ya watumishi. Ili kutekeleza miradi ya maji na umwagiliaji kikamilifu, Sekta ya Maji inahitaji jumla ya wataalam **8,721** ikilinganishwa na wataalam **1,876** waliopo kwa sasa. Kwa upande wa Sekta ya Umwagiliaji, jumla ya wataalam **3,399** wanahitajika ikilinganishwa na wataalam **376** waliopo kwa sasa. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara inaendelea na mawasiliano na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kupata vibali vya kuajiri wataalam hao watakaokidhi mahitaji ya wataalam katika Sekta za Maji na Umwagiliaji.

6. SHUKRANI

261. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutambua mchango wa wadau mbalimbali ambao wamechangia mafanikio yaliyofikiwa katika kuendeleza Sekta za Maji na Umwagiliaji. Naamini kuwa mafanikio yaliyopatikana yametokana na ushirikiano na jitihada za pamoja baina ya Serikali na Wadau hao zikiwemo nchi wahisani, mashirika ya misaada ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Vilevile, napenda kuzishukuru nchi rafiki zikiwemo Serikali za Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri.

262. Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wao mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji nchini kwa juhudi zao katika kuchangia utekelezaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi hiyo pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji nchini. Napenda pia, kuwapongeza wananchi kwa uzalendo wao na nawasihii waendeleo kuvilinda vyanzo vya maji na kutunza miundombinu ya maji na umwagiliaji ili kuwa endelevu kwa matumizi ya sasa na vizazi vijavyo.

263. Mheshimiwa Spika, nizishukuru kwa dhati taasisi za fedha za kimataifa na mashirika ya maendeleo ambayo yametoa ushirikiano mkubwa kwa Serikali katika jitihada za kuboresha huduma za maji na umwagiliaji nchini. Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Marekani la

Changamoto za Milenia (MCC), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway (NORAD), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani (UN HABITAT), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden (SIDA), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Canada (CIDA), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

264. Mheshimiwa Spika, nayashukuru pia mashirika na taasisi za kidini ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha malengo ya Sekta za Maji na Umwagiliaji yanafikiwa. Mashirika na taasisi hizo ni pamoja na *World Islamic League*, Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*, *Islamic Foundation*, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Kianglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA)*, *Norwegian Church Aid* na *Livingwater International*.

265. Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuzishukuru taasisi zisizo za kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET)*; Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (WAMMA); *WaterAid*; *World Vision*; *Plan International*; *Concern Worldwide*; *Netherlands Volunteers Services (SNV)*; *Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (IUCN)*; *World Wide Fund for Nature (WWF)*; *African Medical Research Foundation (AMREF)*; *Clinton HIV Aids Initiative*; *Bill and Melinda Gates Foundation*; na wale wote ambao wameendelea kuisaidia Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kufanikisha malengo yake.

Formatted: Font color: Blue

Formatted: Font color: Blue

266. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe (Mb)**, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji; **Mhandisi Mbogo Futakamba**, Katibu Mkuu; **Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelo**, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizochini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa walionipatia kwa kipindi kifupi tangu niteuliwe na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hiyo. Ushirikiano huo umeonesha imani waliyonayo kwangu katika kutekeleza majukumu yaliyopo ili kufikia malengo ya Sekta, Napenda kuwasihi waendeleo na ushirikiano huo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma endelevu za maji na umwagiliaji.

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Indent: Left: 0", First line: 0", Numbered + Level: 1 + Numbering Style: 1, 2, 3, ... + Start at: 1 + Alignment: Left + Aligned at: 0.2" + Indent at: 0.45"

Formatted: Font: Not Bold, Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Font: Not Bold, Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Not Highlight

Formatted: Font: English (U.S.), Not Highlight

Formatted: No bullets or numbering

7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

266-267. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya **Shilingi 979,507,444,199** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2016/2017, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 49

267-268. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 939,631,302,771** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Maji kwa mwaka 2016/2017. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 24,437,365,000** ambapo **Shilingi 7,075,948,000** sawa na **asilimia 28.96** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (**OC**) na **Shilingi 17,361,417,000** sawa na **asilimia 71.04** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (**PE**) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 915,193,937,771** ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 690,155,000,000** sawa na **asilimia 75.41** ni fedha za ndani na **Shilingi 225,038,937,771** sawa na **asilimia 24.59** ni fedha za nje.

(b) Fungu 05

268-269. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 39,876,141,428** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Umwagiliaji kwa mwaka 2016/2017. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 4,506,612,000** ambapo **Shilingi 299,785,000** sawa na **asilimia 6.65** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (**OC**) na **Shilingi 4,206,827,000** sawa na **asilimia 93.35** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (**PE**) ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 35,369,529,428** ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi**

6,000,000,000 sawa na **asilimia 16.96** ni fedha za ndani na **Shilingi 29,369,529,428** sawa na **asilimia 83.04** ni fedha za nje.

269-270. Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani: www.maji.go.tz.

270-271. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Jedwali Na. 1: Visima Vilivyochimbwa na Makampuni Binafsi Pamoja na DDCA kwa Mwaka 2015/2016

Na.	Kampuni	Idadi ya Visima
1.	<i>Aqwe Drilling and Construction Ltd</i>	2
2.	<i>BRA Company</i>	2
3.	<i>Chem Chem Drilling Co. Ltd</i>	38
4.	<i>China Geo-Engineering Corporation</i>	3
5.	<i>CMG Construction Co. Ltd</i>	2
6.	<i>CPPS Mission</i>	76
7.	<i>Gem and Rock Ventures Ltd</i>	1
8.	<i>Global Resources Alliance Tanzania</i>	59
9.	<i>Global Tech Tanzania</i>	11
10.	<i>Honey Well Drilling</i>	1
11.	<i>Kalis Enterprises and Engineering Ltd</i>	3
12.	<i>Konoike Construction co. Ltd</i>	219
13.	<i>Maji Tech Engineering Ltd</i>	57
14.	<i>Master Drilling and Exploration Ltd</i>	1
15.	<i>Maswi Drilling Company</i>	131
16.	<i>Olelo Heju General Traders Co. Ltd</i>	12
17.	<i>Pamoja Drilling Company</i>	1
18.	<i>PNR Services Ltd</i>	72
19.	<i>Serengeti Ltd JV NSPT Ltd</i>	8

20.	<i>Sparr Drilling Co. Ltd</i>	6
21.	<i>Tanzania Water Wells</i>	2
22.	<i>Target Borewells Ltd</i>	7
23.	<i>Thanzania Borehole Co. Ltd</i>	1
24.	<i>Victoria Borehole Drilling Ltd</i>	4
25.	<i>Water Solutions Drilling Company Ltd</i>	99
26.	<i>Willy Enterprises Ltd</i>	1
27.	<i>Drilling and Dam Construction Agency - DDCA</i>	185
Jumla		1,004

Jedwali Na. 2: Makusanyo na Makadirio ya Maduhuli kwa Bodi za Maji za Mabonde kwa Kipindi cha Miaka Mitatu

Na.	Bonde	2014/2015			2015/2016			2016/2017
		Makadirio	Makusanyo Hadi Juni, 2015 (SHS)	%	Makadirio	Makusanyo Hadi Machi, 2016 (SHS)	%	Makadirio ya Makusanyo 2016/2017
1.	Pangani	370,000,000	474,565,720	128	370,000,000	515,350,168.39	139	500,000,000
2.	Wami/Ruvu	320,000,000	110,358,140	34	320,000,000	273,044,039.94	85	300,000,000
3.	Mto Rufiji	580,000,000	664,845,494	115	723,000,000	649,386,983.82	89	916,000,000
4.	Ruvuma	150,000,000	134,842,128	90	170,000,000	161,582,280.00	95	180,000,000
5.	Ziwa Nyasa	275,000,000	85,434,423	31	350,000,000	172,747,014.80	49	670,000,000
6.	Bonde la Kati	200,000,000	118,837,477	59	300,000,000	131,449,288.61	43	350,000,000
7.	Ziwa Rukwa	246,000,000	246,445,961	100	350,000,000	290,183,157.00	82	400,000,000
8.	Ziwa Tanganyika	85,000,000	44,899,765	53	90,000,000	53,380,300.00	59	100,000,000
9.	Ziwa Victoria	350,000,000	212,300,153	61	350,000,000	354,520,800.75	101	390,000,000
Jumla		2,576,000,000	2,092,529,261	81	3,023,000,000	2,601,644,033.31	86	3,806,000,000

Jedwali Na. 3: Vyanzo vya Maji Vilivyokaguliwa katika Mikoa Mbalimbali na Hali ya Ubora wa Vyanzo

Mkoa	Wilaya	Eneo	Vyanzo Vilivyokaguliwa		
			Aina ya Chanzo	Idadi	Vyanzo Visivyo Salama
ARUSHA	Arusha CC	Sinoni	Kisima kirefu	20	6
			Kisima kifupi	3	2
			Kioski (AUWSA)	1	0
		Sombetin	Kisima kifupi	18	17
		Olasiti	Bwawa	1	1
		Muriet	Mito	6	6
		Osunyai	Chemichemi	20	18
		Sokoni 1	Kisima kifupi	90	90
			Kioski (AUWSA)	1	0
			Chemichemi	1	1
		Ngarenaro	Kioski (AUWSA)	11	0
		Matreves-Olmoti	Bwawa	1	1
	Sekei	Chemichemi	1	1	
	Longido	Engikaret	Bwawa	5	5
			Kisima kirefu	1	1
	Meru	Majiya Chai	Chemichemi	4	4
		Kikatiti	Kisima kifupi	8	8
Usa-WSSA		Kioski	6	3	
MANYARA	Hanang	Balagda	Chemichemi	3	3
			Kisima kifupi	21	21
			Bwawa	7	7
			Kisima kirefu	1	1
			Kioski	3	3

Mkoa	Wilaya	Eneo	Vyanzo Vilivyokaguliwa		
			Aina ya Chanzo	Idadi	Vyanzo Visivyo Salama
		Oliurai-Noondoto	Bwawa	1	1
		Himit	Kijito	3	1
		Katesh center	Kijito	3	0
		Jorodom	Kijito	1	0
		Mogitu	Kisima kirefu	1	0
		Gijega	Kisima kirefu	1	0
		Mangarairai	Kijito	1	0
		Lana	Kijito	1	0
	Babati	Mjini Kati-BAWASA	Kisima kirefu	16	0
			Kioski	17	3
KAGERA	Misenyi	Bunazi	Kisima kifupi	1	1
			Kisima kirefu	1	1
		Kyaka	Kisima kirefu	1	1
			Mto	2	2
			Kisima kifupi	1	1
KIGOMA	Kigoma TC	UJJI	Kisima kifupi	10	10
			Kisima kirefu	1	1
			Chemichemi	4	2
MWANZA	Nyamagana	MWAUWAS A	Kioski	14	1
	Ilemela		Kioski	21	8
SINGIDA	Singida TC	Mlinga	Kisima kifupi	2	0
		Unyambwa	Kisima kirefu	2	0
		Mtunduruni	Kioski	1	0
			Kisima kirefu	1	0
		Mandewa	Kisima kirefu	1	0
			Kisima kifupi	1	1
		Unyanga	Kisima kifupi	1	0

Mkoa	Wilaya	Eneo	Vyanzo Vilivyokaguliwa		
			Aina ya Chanzo	Idadi	Vyanzo Visivyo Salama
			Kisima kirefu	1	0
		Kisali	Kisima kifupi	1	1
			Kisima kirefu	1	0
		Misuna	Kisima kifupi	1	0
		Kindai	Kisima kifupi	3	3
		Utemini	Kisima kirefu	1	0
			Kisima kifupi	1	0
		Uhimaka	Kisima kirefu	1	1
			Kisima kifupi	1	1
		Kidaru	Kisima kifupi	4	4
		Tulya	Kisima kifupi	2	2
			Kisima kirefu	1	0
		Ntwike	Kisima kirefu	3	3
		Shelui	Kisima kirefu	1	0
Mtoa	Kisima kirefu	1	1		
MBEYA	Kyela	Matema	Ziwa Nyasa	1	0
			Mto Mwalalo	2	2
MARA	Musoma TC	Rwamlimi	Ziwa Victoria	2	2
			Kisima kifupi	1	1
			Bwawa dogo	1	1
			Chemichemi	1	1
			Kioski	3	0
		Mshikamano	Bwawa dogo	1	1
		Kwangwa	Bwawa dogo	1	1
			Chemichemi	1	0
		Kigera	Bwawa dogo	1	0
		Buhare	Bwawa dogo	1	0

Mkoa	Wilaya	Eneo	Vyanzo Vilivyokaguliwa			
			Aina ya Chanzo	Idadi	Vyanzo Visivyo Salama	
			Kisima kifupi	2	2	
		Kamnyonge	Ziwa Victoria	1	0	
		Makoko	Bwawa dogo	1	1	
			Chemichemi	1	0	
		Mwisenge	Kisima kifupi	1	1	
			Kisima kifupi	2	2	
		Nyakato	Ziwa Victoria	2	2	
		Kitaji				
		Musoma DC	Nyamrandira	Ziwa Victoria	2	2
			Mrangi	Ziwa Victoria	1	1
	Bukima		Kisima kifupi	3	2	
			Ziwa Victoria	2	2	
			Chemichemi	1	1	
			Kisima kirefu	1	1	
	Ifurifu		Kisima kifupi	1	1	
	Bweri		Ziwa Victoria	14	14	
	Makoko					
	Mwisenge					
	Mgobero					
	Kigera		Kioski	1	0	
Makoko	Kioski		1	0		
Mkendo	Kioski	1	0			
Mwisenge	Kioski	1	0			
Serengeti	Nyansurura	Mto Tobora	4	4		
MOROGORO	Morogoro TC	Tungi	Kisima kifupi	12	6	
			Boza	1		
			Kisima kirefu	1	0	
			Mto	1	1	

Mkoa	Wilaya	Eneo	Vyanzo Vilivyokaguliwa			
			Aina ya Chanzo	Idadi	Vyanzo Visivyo Salama	
		Kilakala	Kisima kifupi	1	0	
		Mlimani	Mito	1	1	
		Mafisa	Kisima kirefu	1	0	
			Kisima kifupi	1	1	
		Lukobe	Kisima kifupi	8	4	
		MORUWASA	Kioski	50	17	
		Mwembesongo	Kisima kirefu	3	0	
			Kisima kifupi	3	3	
		Kitosa	Mikumi	Kisima kirefu	2	0
			Kidodi	Kisima kifupi	3	3
	Ruaha		Mito	1	1	
			Kioski	4	4	
			Kisima kifupi	1	1	
		Kioski	2	2		
	Mvumero	Mlali	Mto	3	3	
	Morogoro DC	Bwakila	Kisima kifupi	3	3	
			Mto	2	2	
		Mvuha	Kisima kifupi	4	4	
			Mto	1	1	
			Kisima kifupi	4	4	
Dodoma	Dodoma TC	Mnadani	Kisima kifupi	4	4	
			Bwawa	1	1	
		Kioski (DUWASA)	37	1		
	Chigongwe	Kisima kifupi	5	5		
	Chamwino	Lonje	Kisima kifupi	2	2	
	Mpwapwa-WSSA	Chipokolo	Kisima kirefu	2	0	
Iringa	Iringa DC	Pawaga	Mto	4	3	

Mkoa	Wilaya	Eneo	Vyanzo Vilivyokaguliwa		
			Aina ya Chanzo	Idadi	Vyanzo Visivyo Salama
	Mufindi	Mafinga WSSA	Mto	2	0
			Kioski	5	0
JUMLA				600	371

Jedwali Na. 4 (a): Orodha ya Halmashauri Zilizotengewa Fedha za Maendeleo Kutekeleza Miradi ya Maji Vijijini katika Mwaka 2016/2017

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
Arusha	1	Arusha	MC	1,339,587,000	125,000,000	1,464,587,000
	2	Arusha	DC	4,053,854,000	157,768,000	4,211,622,000
	3	Karatu	DC	958,998,000	182,057,000	1,141,055,000
	4	Longido	DC	4,474,189,000	134,077,000	4,608,266,000
	5	Meru	DC	2,700,121,000	220,784,000	2,920,905,000
	6	Monduli	DC	2,470,643,000	180,145,000	2,650,789,000
	7	Ngorongoro	DC	1,932,000,000	226,557,000	2,158,557,000
Jumla ndogo				17,929,391,000	1,226,389,000	19,155,780,000
Dar es Salaam	8	Ilala	MC	1,656,109,000	93,179,000	1,749,289,000
	9	Kinondoni	MC	718,741,000	155,280,000	874,021,000
	10	Temeke	MC	420,000,000	155,285,000	575,285,000
Jumla ndogo				2,794,850,000	403,744,000	3,198,594,000
Dodoma	11	Bahi	DC	1,084,452,000	113,348,000	1,197,800,000
	12	Chamwino	DC	783,515,000	197,767,000	981,282,000
	13	Chemba	DC	1,432,869,000	221,644,000	1,654,514,000
	14	Dodoma	MC	1,134,701,000	89,998,000	1,224,699,000
	15	Kondoa	DC	1,577,274,000	138,592,000	1,715,866,000
	16	Kondoa	TC	190,000,000	50,000,000	240,000,000
	17	Kongwa	DC	732,006,000	254,305,000	986,311,000
	18	Mpwapwa	DC	1,426,298,000	156,324,000	1,582,622,000
Jumla ndogo				8,361,115,000	1,221,978,000	9,583,093,000
Geita	19	Bukombe	DC	1,432,000,000	272,618,000	1,704,618,000
	20	Chato	DC	5,802,515,000	299,390,000	6,101,906,000
	21	Geita	DC	3,021,443,000	260,414,000	3,281,857,000
	22	Geita	TC	420,000,000	194,751,000	614,751,000
	23	Mbogwe	DC	1,432,000,000	326,293,000	1,758,293,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
	24	Nyanghwale	DC	6,111,411,000	299,415,000	6,410,827,000
Jumla ndogo				18,219,370,000	1,652,881,000	19,872,251,000
Iringa	25	Iringa	DC	2,449,131,000	233,686,000	2,682,816,000
	26	Iringa	MC	1,704,917,000	171,689,000	1,876,606,000
	27	Kilolo	DC	932,183,000	270,271,000	1,202,455,000
	28	Mafinga	TC	420,000,000	125,000,000	545,000,000
	29	Mufindi	DC	2,449,787,000	227,190,000	2,676,977,000
Jumla ndogo				7,956,018,000	1,027,836,000	8,983,854,000
Kagera	30	Biharamulo	DC	2,044,910,000	222,109,000	2,267,018,000
	31	Bukoba	DC	1,758,965,000	346,495,000	2,105,459,000
	32	Bukoba	MC	448,250,000	75,052,000	523,303,000
	33	Karagwe	DC	4,297,029,000	338,070,000	4,635,099,000
	34	Kyerwa	DC	2,432,000,000	318,131,000	2,750,131,000
	35	Misenyi	DC	2,010,431,000	243,426,000	2,253,857,000
	36	Muleba	DC	1,331,989,000	315,084,000	1,647,074,000
	37	Ngara	DC	1,921,893,000	123,616,000	2,045,509,000
Jumla ndogo				16,245,467,000	1,981,983,000	18,227,450,000
Katavi	38	Mlele	DC	633,889,000	179,995,000	813,884,000
	39	Mpanda	DC	432,000,000	347,726,000	779,726,000
	40	Mpanda	MC	420,000,000	156,972,000	576,972,000
	41	Mpimbwe	DC	633,889,000	179,995,000	813,884,000
	42	Nsimbo	DC	481,150,000	276,272,000	757,422,000
Jumla ndogo				2,600,928,000	1,140,961,000	3,741,889,000
Kigoma	43	Buhigwe	DC	932,000,000	351,723,000	1,283,723,000
	44	Kakonko	DC	932,000,000	261,621,000	1,193,621,000
	45	Kasulu	DC	3,104,577,000	268,884,000	3,373,461,000
	46	Kasulu	TC	720,000,000	125,000,000	845,000,000
	47	Kibondo	DC	848,994,000	274,982,000	1,123,975,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
	48	Kigoma	DC	1,752,066,000	286,396,000	2,038,462,000
	49	Kigoma/Ujiji	MC	1,679,724,000	69,860,000	1,749,584,000
	50	Uvinza	DC	3,252,035,000	309,759,000	3,561,794,000
Jumla ndogo				13,221,396,000	1,948,225,000	15,169,621,000
Kilimanjaro	51	Hai	DC	725,786,000	178,862,000	904,648,000
	52	Moshi	DC	524,183,000	235,202,000	759,385,000
	53	Moshi	MC	607,864,000	152,892,000	760,755,000
	54	Mwanga	DC	780,249,000	321,765,000	1,102,014,000
	55	Rombo	DC	2,657,986,000	320,888,000	2,978,873,000
	56	Same	DC	438,226,000	225,620,000	663,847,000
	57	Siha	DC	2,032,133,000	124,663,000	2,156,796,000
Jumla ndogo				7,766,427,000	1,559,891,000	9,326,319,000
Lindi	58	Kilwa	DC	440,780,000	345,144,000	785,924,000
	59	Lindi	DC	1,440,262,000	326,088,000	1,766,351,000
	60	Lindi	MC	462,397,000	98,366,000	560,763,000
	61	Liwale	DC	447,913,000	284,005,000	731,919,000
	62	Nachingwea	DC	438,282,000	341,585,000	779,867,000
	63	Ruangwa	DC	1,290,800,000	395,952,000	1,686,752,000
Jumla ndogo				4,520,435,000	1,791,139,000	6,311,575,000
Manyara	64	Babati	DC	962,936,000	208,065,000	1,171,001,000
	65	Babati	TC	817,589,000	79,533,000	897,121,000
	66	Hanang	DC	1,198,653,000	370,812,000	1,569,466,000
	67	Kiteto	DC	972,879,000	331,715,000	1,304,595,000
	68	Mbulu	DC	2,181,221,000	270,813,000	2,452,035,000
	69	Mbulu	TC	190,000,000	50,000,000	240,000,000
	70	Simanjiro	DC	1,374,341,000	397,714,000	1,772,056,000
Jumla ndogo				7,697,620,000	1,708,653,000	9,406,273,000
Mara	71	Bunda	DC	1,703,570,000	356,014,000	2,059,584,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
	72	Bunda	TC	190,000,000	50,000,000	240,000,000
	73	Butiama	DC	945,785,000	234,412,000	1,180,197,000
	74	Musoma	DC	2,887,450,000	316,679,000	3,204,129,000
	75	Musoma	MC	0	0	0
	76	Rorya	DC	3,066,735,000	166,078,000	3,232,813,000
	77	Serengeti	DC	1,357,743,000	138,766,000	1,496,509,000
	78	Tarime	DC	480,140,000	219,881,000	700,021,000
	79	Tarime	TC	420,000,000	177,902,000	597,902,000
Jumla ndogo				11,051,422,000	1,659,734,000	12,711,156,000
Mbeya	80	Busokelo	DC	445,314,000	175,599,000	620,913,000
	81	Chunya	DC	393,299,000	168,270,000	561,569,000
	82	Kyela	DC	2,280,274,000	80,626,000	2,360,900,000
	83	Mbarali	DC	3,440,782,000	221,228,000	3,662,010,000
	84	Mbeya	CC	475,621,000	154,985,000	630,606,000
	85	Mbeya	DC	2,537,310,000	249,706,000	2,787,016,000
	86	Rungwe	DC	5,094,112,000	227,364,000	5,321,476,000
Jumla ndogo				14,666,712,000	1,277,777,000	15,944,490,000
Morogoro	87	Gairo	DC	452,927,000	199,307,000	652,234,000
	88	Kilombero	DC	1,673,251,000	182,749,000	1,856,000,000
	89	Ifakara	TC	190,000,000	50,000,000	240,000,000
	90	Kilosa	DC	897,377,000	245,436,000	1,142,813,000
	91	Malinyi	DC	702,000,000	50,000,000	752,000,000
	92	Morogoro	MC	372,814,000	105,494,000	478,308,000
	93	Morogoro	DC	4,454,547,000	331,026,000	4,785,573,000
	94	Mvomero	DC	775,271,000	339,895,000	1,115,165,000
	95	Ulanga	DC	2,932,298,000	253,347,000	3,185,645,000
Jumla ndogo				12,450,484,000	1,757,255,000	14,207,739,000
Mtwara	96	Masasi	DC	6,704,016,000	177,902,000	6,881,918,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
	97	Masasi	TC	420,000,000	179,513,000	599,513,000
	98	Mtwara	DC	1,782,468,000	165,650,000	1,948,119,000
	99	Mtwara	MC	451,960,000	324,400,000	776,360,000
	100	Nanyumbu	DC	520,631,000	93,630,000	614,261,000
	101	Nanyamba	TC	420,000,000	125,000,000	545,000,000
	102	Newala	DC	6,712,587,000	176,975,000	6,889,561,000
	103	Newala	TC	190,000,000	50,000,000	240,000,000
	104	Tandahimba	DC	665,574,000	299,440,000	965,013,000
Jumla ndogo				17,867,235,000	1,592,510,000	19,459,745,000
Mwanza	105	Buchosa	DC	1,202,000,000	50,000,000	1,252,000,000
	106	Ilemela	MC	3,629,972,000	335,168,000	3,965,140,000
	107	Kwimba	DC	3,582,724,000	110,081,000	3,692,806,000
	108	Magu	DC	3,607,700,000	273,009,000	3,880,709,000
	109	Misungwi	DC	2,392,687,000	159,170,000	2,551,858,000
	110	Mwanza	CC	218,526,000	311,247,000	529,773,000
	111	Sengerema	DC	1,650,846,000	153,512,000	1,804,358,000
	112	Ukerewe	DC	3,046,539,000	119,283,000	3,165,822,000
Jumla ndogo				19,330,995,000	1,511,470,000	20,842,465,000
Njombe	113	Ludewa	DC	339,678,000	221,644,000	561,322,000
	114	Makambako	TC	920,000,000	72,836,000	992,836,000
	115	Makete	DC	640,621,000	181,903,000	822,524,000
	116	Njombe	DC	251,268,000	333,646,000	584,914,000
	117	Njombe	TC	2,433,273,000	196,633,000	2,629,907,000
	118	Wangingombe	DC	832,000,000	260,817,000	1,092,817,000
Jumla ndogo				5,416,840,000	1,267,480,000	6,684,319,000
Pwani	119	Bagamoyo	DC	547,071,000	215,407,000	762,478,000
	120	Chalinze	DC	650,000,000	100,000,000	750,000,000
	121	Kibaha	DC	738,223,000	153,952,000	892,175,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
	122	Kibaha	TC	1,026,571,000	133,273,000	1,159,844,000
	123	Kibiti	TC	690,000,000	50,000,000	740,000,000
	124	Kisarawe	DC	1,112,440,000	283,025,000	1,395,465,000
	125	Mafia	DC	885,246,000	255,300,000	1,140,546,000
	126	Mkuranga	DC	959,468,000	166,366,000	1,125,835,000
	127	Rufiji	DC	319,612,000	141,191,000	460,804,000
Jumla ndogo				6,928,631,000	1,498,515,000	8,427,146,000
Rukwa	128	Kalambo	DC	849,730,000	104,666,000	954,396,000
	129	Nkasi	DC	5,224,162,000	141,560,000	5,365,722,000
	130	Sumbawanga	DC	812,228,000	163,356,000	975,585,000
	131	Sumbawanga	MC	662,179,000	155,184,000	817,363,000
Jumla ndogo				7,548,299,000	564,766,000	8,113,065,000
Ruvuma	132	Madaba	DC	777,115,000	50,000,000	827,115,000
	133	Namlumbo	DC	1,014,057,000	221,644,000	1,235,702,000
	134	Nyasa	DC	1,454,764,000	238,868,000	1,693,632,000
	135	Songea	DC	4,613,040,000	118,195,000	4,731,235,000
	136	Mbinga	DC	1,522,423,000	196,769,000	1,719,192,000
	137	Songea	MC	1,159,859,000	163,284,000	1,323,143,000
	138	Tunduru	DC	1,450,134,000	198,318,000	1,648,452,000
Jumla ndogo				11,991,393,000	1,187,077,000	13,178,470,000
Shinyanga	139	Kahama	TC	434,581,000	159,570,000	594,151,000
	140	Kishapu	DC	774,678,000	244,562,000	1,019,240,000
	141	Msalala	DC	432,000,000	194,435,000	626,435,000
	142	Ushetu	DC	453,441,000	258,289,000	711,731,000
	143	Shinyanga	DC	2,189,091,000	166,496,000	2,355,587,000
	144	Shinyanga	MC	458,943,000	221,280,000	680,223,000
Jumla ndogo				4,742,734,000	1,244,632,000	5,987,366,000
Simiyu	145	Bariadi	TC	420,000,000	106,881,000	526,881,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
	146	Bariadi	DC	1,029,901,000	154,669,000	1,184,570,000
	147	Busega	DC	747,592,000	155,113,000	902,705,000
	148	Itilima	DC	1,682,074,000	106,261,000	1,788,334,000
	149	Maswa	DC	1,305,810,000	180,181,000	1,485,991,000
	150	Meatu	DC	3,252,645,000	197,398,000	3,450,043,000
Jumla ndogo				8,438,022,000	900,503,000	9,338,524,000
Singida	151	Ikungi	DC	542,415,000	166,758,000	709,173,000
	152	Iramba	DC	1,062,141,000	168,890,000	1,231,031,000
	153	Itigi	DC	542,000,000	67,784,000	609,784,000
	154	Manyoni	DC	432,000,000	67,784,000	499,784,000
	155	Mkalama	DC	572,751,000	115,600,000	688,351,000
	156	Singida	DC	543,909,000	66,975,000	610,884,000
	157	Singida	MC	2,180,966,000	221,442,000	2,402,408,000
Jumla ndogo				5,876,183,000	875,232,000	6,751,416,000
Songwe	158	Ileje	DC	663,164,000	278,363,000	941,527,000
	159	Mbozi	DC	686,536,000	136,625,000	823,161,000
	160	Momba	DC	663,125,000	221,644,000	884,770,000
	161	Songwe	DC	702,000,000	50,000,000	752,000,000
	162	Tunduma	TC	620,000,000	133,369,000	753,369,000
Jumla ndogo				3,334,826,000	820,002,000	4,154,828,000
Tabora	163	Igunga	DC	432,000,000	110,612,000	542,612,000
	164	Kaliua	DC	481,428,000	96,856,000	578,283,000
	165	Nzega	DC	432,000,000	246,501,000	678,501,000
	166	Nzega	TC	420,000,000	125,000,000	545,000,000
	167	Sikonge	DC	433,035,000	255,552,000	688,587,000
	168	Tabora	MC	1,367,335,000	137,795,000	1,505,130,000
	169	Urambo	DC	434,749,000	157,317,000	592,066,000
	170	Uyui/Tabora	DC	486,508,000	267,910,000	754,418,000

Mkoa	Na.	Halmashauri	Aina	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
Jumla ndogo				4,487,055,000	1,397,543,000	5,884,598,000
Tanga	171	Bumbuli	DC	938,455,000	221,974,000	1,160,429,000
	172	Handeni	DC	897,206,000	267,615,000	1,164,821,000
	173	Handeni	TC	920,000,000	209,939,000	1,129,939,000
	174	Kilindi	DC	3,705,996,000	173,915,000	3,879,911,000
	175	Korogwe	DC	1,631,609,000	260,284,000	1,891,893,000
	176	Korogwe	TC	343,810,000	235,388,000	579,198,000
	177	Lushoto	DC	3,193,519,000	211,682,000	3,405,202,000
	178	Mkinga	DC	4,195,472,000	180,664,000	4,376,136,000
	179	Muheza	DC	991,210,000	162,268,000	1,153,478,000
	180	Pangani	DC	439,959,000	248,890,000	688,848,000
	181	Tanga	CC	2,298,915,000	249,203,000	2,548,119,000
Jumla ndogo				19,556,152,000	2,421,823,000	21,977,975,000
JUMLA NDOGO – 4(a)				261,000,000,000	35,640,000,000	296,640,000,000

Jedwali Na. 4 (b): Fedha za Maendeleo Zilizotengwa kwa ajili ya Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini katika Sekretarieti za Mkoa kwa Mwaka 2016/2017

Na.	Mkoa	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
1.	Arusha	40,758,000	40,758,000	81,516,000
2.	Dar es Salaam	31,778,000	31,778,000	63,555,000
3.	Dodoma	39,129,000	39,129,000	78,257,000
4.	Geita	39,975,000	39,975,000	79,950,000
5.	Iringa	37,409,000	37,409,000	74,818,000
6.	Kagera	41,409,000	41,409,000	82,818,000

Na.	Mkoa	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
7.	Katavi	37,575,000	37,575,000	75,150,000
8.	Kigoma	37,575,000	37,575,000	75,150,000
9.	Kilimanjaro	37,575,000	37,575,000	75,150,000
10.	Lindi	37,575,000	37,575,000	75,150,000
11.	Manyara	39,575,000	39,575,000	79,150,000
12.	Mara	37,371,000	37,371,000	74,742,000
13.	Mbeya	29,516,000	29,516,000	59,032,000
14.	Morogoro	45,287,000	45,287,000	90,573,000
15.	Mtwara	43,575,000	43,575,000	87,150,000
16.	Mwanza	41,409,000	41,409,000	82,818,000
17.	Njombe	37,575,000	37,575,000	75,150,000
18.	Pwani	41,409,000	41,409,000	82,818,000
19.	Rukwa	37,575,000	37,575,000	75,150,000
20.	Ruvuma	37,575,000	37,575,000	75,150,000
21.	Shinyanga	45,409,000	45,409,000	90,818,000
22.	Simiyu	37,575,000	37,575,000	75,150,000
23.	Singida	37,575,000	37,575,000	75,150,000
24.	Songwe	15,893,000	15,893,000	31,786,000
25.	Tabora	46,000,000	46,000,000	92,000,000
26.	Tanga	45,927,000	45,927,000	91,854,000
JUMLA NDOGO – 4(b)		1,000,000,000	1,000,000,000	2,000,000,000

Jedwali Na. 4 (c): Fedha za Maendeleo Zilizotengwa kwa ajili ya Miradi Mingine ya Maji Vijijini Inayoendelea Kujengwa katika Mwaka 2016/2017

Na.	Kazi Itakayotekelezwa	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla
1.	Miradi ya Matokea ya Haraka (wins)	48,700,000,000	0	48,700,000,000
2.	Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye Mabwawa	17,323,312,000	0	17,323,312,000
3.	Mradi wa kuweka miundombinu ya maji vijijini kutoka katika visima	4,000,000,000	0	4,000,000,000
4.	Miradi ya Kimkakali (Strategic/Earmarked Projects)	8,000,000,000	0	8,000,000,000
5.	Mradi wa upanuzi na ukarabati wa miundombinu Chiwambo, Makonde, vijiji 40 KASHWASA, Wanging'ombe, HTM na Ntomoko	3,000,000,000	0	3,000,000,000
6.	Miradi wa Maji wa Tabora	137,044,000	1,000,000,000	1,137,044,000
7.	Mradi wa Maji Kigoma	0	5,280,000,000	5,280,000,000
8.	Mradi wa maji Njombe, Urambo, Mbulu, Babati, Iramba, Singida Rural, Kilosa chini ya ufadhili wa WaterAID.	0	3,800,000,000	3,800,000,000
9.	Kujenga miradi ya maji Morogoro kwa ufadhili wa JICA	0	270,000,000	270,000,000
10.	Mradi wa Same-Mwanga	19,224,000,000	34,170,000,000	53,394,000,000
11.	Usimamizi, ufuatiliaji, tathmini na uendeshaaji na Matengenezo Miradi ya Maji Vijijini	10,956,144,000	3,700,000,000	14,656,144,000
12.	Usimamizi na usafi wa mazingira - TAMISEMI	0	300,000,000	300,000,000
13.	Usimamizi na usafi wa mazingira-Wizara ya Afya	0	3,700,000,000	3,700,000,000
14.	Usimamizi na usafi wa mazingira-Wizara ya Elimu	0	1,100,000,000	1,100,000,000
JUMLA NDOGO - 4(c)		111,340,500,000	53,320,000,000	164,660,500,000
JUMLA KUU MAJI VIJIJINI [4(a) + 4(b) + 4(c)]		373,340,500,000	89,960,000,000	463,300,500,000

Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Fedha Zinzohitajika katika Utekezaji wa Miradi ya Maji ya Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
1.	Mtwara	Mradi wa Maji Makonde	Ujenzi wa chanzo, Ujenzi wa mitambo ya kutibu majisafi, Ujenzi wa matanki, Ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji	EURO milioni 89	- Majadiliano na Kampuni ya CSC kutoka Afrika Kusini yanaendelea - Usanifu umekamilika
2.	Katavi	Mradi wa Maji Mpanda	Ujenzi wa vyanzo, mtambo wa kutibu na kusafisha maji, matanki ya kuhifadhi maji, vituo vya kuchotea maji, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji.	Shilingi bilioni 55.81	- Majadiliano na Serikali ya Austria kupitia Kampuni ya OSTAP kwa ajili ya ufadhili wa mradi yanaendelea - Usanifu umekamilika.
		Mradi wa maji mji wa Inyonga	Uchimbaji visima, ufungaji wa pampu, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya usambazaji, ujenzi wa matanki na miundombinu ya uondoshaji majitaka	Shilingi bilioni 10.08	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
3.	Mbeya	Mradi wa Maji wa Mji wa Tunduma	Ujenzi wa chanzo, mtambo wa kusafisha na kutibu maji, matanki ya kuhifadhi maji, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji	EURO milioni 100	- Majadiliano na Serikali ya Ubelgiji kupitia Kampuni ya ASPAC International yanaendelea - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji	Kuchimba visima vitatu, kununua na	USD milioni 4.43	- Andiko la mradi limewasilishwa

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
		Chunya	kufunga pampu, ujenzi wa majengo matatu ya kuendesha pampu, tanki la mita za ujazo 500, jengo la kuhifadhi dawa, ulazaji wa bomba kuu kilomita 7, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 10.5 na ununuzi wa dira za maji		Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji Kasumulu	Kuchimba visima vitatu, kununua na kufunga pampu, ujenzi wa majengo matatu ya mitambo ya kusukuma maji, ujenzi wa tanki la mita za ujazo 500, jengo la kuhifadhi dawa, ulazaji wa bomba kuu kilomita 3.8, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 22.50 na ununuzi wa dira za maji	USD milioni 5.80	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji Kyela	Kuchimba visima vitatu, kununua na kufunga pampu, ujenzi wa majengo matatu ya mitambo ya kusukuma maji, ujenzi wa tanki la mita za ujazo 500,	USD milioni 6.90	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
			jengo la kuhifadhi dawa, ulazaji wa bomba kuu kilomita 4.50, ulazaji wa mabomba ya usambazaji kilomita 36.0 na ununuzi wa dira za maji		
		Mradi wa Mji Mbalizi	Ujenzi wa Chanzo, mitambo ya kutibu na kusafisha maji, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, ukarabati na upanuzi wa mabomba ya kusambaza maji	USD milioni 10.80	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Mji Mlowo	Kuchimba visima vitatu, kununua na kufunga pampu, ujenzi wa majengo matatu ya mitambo ya kusukuma maji, ujenzi wa tanki la mita za ujazo 500, jengo la kuhifadhi dawa, ulazaji wa bomba kuu umbali wa kilomita 4.8, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 20 na ununuzi wa dira za maji	USD milioni 5.13	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Mji Rujewa	Kuchimba visima vitatu, kununua na kufunga pampu, ujenzi wa majengo matatu ya mitambo	USD milioni 5.10	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
			ya kusukuma maji, ujenzi wa tanki la mita za ujazo 500, jengo la kuhifadhi dawa, ulazaji wa bomba kuu kilomita 0.5, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 11.68 na ununuzi wa dira za maji		ufadhili kutoka Serikali ya India - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Mji Tukuyu	Ujenzi wa chanzo, mtambo wa kutibu na kusafisha maji, matanki ya kuhifadhi maji, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji na ununuzi wa dira za maji	USD milioni 8.45	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Mji Vwawa	Ujenzi wa chanzo, mtambo wa kutibu na kusafisha maji, matanki ya kuhifadhi maji, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji na ununuzi wa dira za maji. Ukarabati wa chanzo, matanki ya kuhifadhi maji, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji	USD milioni 8.61	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
		Mradi wa Maji Itumba	Ulazaji bomba kuu kilomita 4.55 na 0.99, mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 8.30, ujenzi wa <i>sedimentation tank</i> lenye mita za ujazo 1,296, jengo la madawa, ukarabati wa matanki na ununuzi wa dira za maji	USD milioni 3.13	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
4.	Lindi	Mradi wa Maji katika mji wa Kilwa Masoko	Ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafisha na kutibu maji, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, ukarabati na upanuzi wa mabomba ya kusambaza maji	EURO milioni 61.67	- Majadiliano na Serikali ya Ubelgiji kupitia Kampuni ya ASPAC International yanaendelea - Usanifu umekamilika
5.	Tanga	Mradi wa Maji Korogwe	Ujenzi wa chanzo, ujenzi wa matanki, ukarabati na upanuzi wa mabomba ya kusambaza maji	EURO milioni 5.8	- Majadiliano na Serikali ya Austria kupitia Kampuni ya STRABAG kwa ajili ya ufadhili wa mradi yanaendelea - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji Muheza	Ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafisha na kutibu maji, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, ukarabati na upanuzi	USD milioni 13.4	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
			wa mabomba ya kusambaza maji na ujenzi wa jengo la ofisi.		- Usanifu umekamilika
		Mradi Maji wa mji wa Pangani	Uchimbaji wa visima vitatu, ununuzi wa pampu na kuzifunga, ununuzi wa jenereta, kulaza bomba na kuweka mfumo wa kutibu maji	USD milioni 1.2	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji HTM	Ukarabati na upanuzi wa chanzo cha Mto Pangani, kujenga mitambo ya kusafisha maji, kukarabati bomba kuu, kukarabati matanki na kujenga mengine mapya na kukarabati na kupanua mtandao wa majisafi	USD milioni 84.4	- Majadiliano na Serikali ya Uholanzi kupitia Kampuni ya BAM International ambapo fedha kiasi cha EURO milioni 60 zinategemewa kupatikana - Usanifu umekamilika
6.	Mara	Mradi wa Maji Mugumu	Ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafisha na kutibu maji, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji	USD milioni 8.64	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji wa Tarime	Kuboresha kiteo cha maji na chujio, bomba la kusafisha na kusambaza maji pamoja na kuunganishia wateja	USD milioni 11.64	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
7.	Njombe	Mradi wa Maji Wanging'o mbe	Ukarabati wa chanzo cha Mbukwa na Mtitafu, Ulazaji wa bomba kuu kutoka chanzo cha Mbukwa, Ukarabati wa matanki, Ulazaji wa bomba kuu kutoka chanzo cha Mtitafu, Ujenzi wa tanki la Igwachanya na ulazaji wa mtandao wa usambazaji maji	USD milioni 48.99	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India. - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji wa Mji wa Njombe	Ukarabati wa chanzo cha Magoda, ujenzi wa chanzo cha Mto Hagafilo, ulazaji wa bomba kuu, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji, ujenzi wa matanki na ununuzi wa dira za maji.	USD milioni 11.99	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji wa Mji wa Makele	Ujenzi wa chanzo, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, ukarabati na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji	USD milioni 19.15	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji wa Mji wa Ludewa	Ujenzi wa chanzo, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, ukarabati na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji	USD milioni 8.61	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
		Mradi wa Maji wa Mji	Ujenzi wa chanzo, mitambo ya kutibu na	USD milioni 32.40	- Andiko la mradi limepelekwa

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
		wa Makambako	kusafisha maji, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji		Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India. - Usanifu umekamilika
8.	Geita	Mradi wa Maji wa Mji wa Geita	Ujenzi wa chanzo, mitambo ya kutibu na kusafisha maji, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa matanki, na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji	USD milioni 45.84	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India. - Usanifu umekamilika
9.	Manyara	Mradi wa maji wa Mji wa Katesh	Uchimbaji wa visima vitano, ujenzi wa matanki mawili pamoja na chujio kwenye chanzo kilichopo Hamit	USD milioni 3.65	- Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kutekeleza mradi - Usanifu umekamilika
10.	Kigoma	Mradi maji wa Mji wa Kasulu	Ukarabati wa vyanzo vya maji vya Miseno, Nyakatoke na Nyanka pamoja wa chanzo cha Benga. Ukarabati wa matanki ya maji maeneo ya Magereza na <i>R.C. Mission</i>	USD milioni 9.89	- Andiko la mradi limepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuomba ufadhili kutoka Serikali ya India - Usanifu umekamilika
11.	Pwani	Mradi maji wa Mji wa Kisarawe	Ujenzi wa nyumba mbili za mitambo, ununuzi wa pampu mbili, ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 22, ujenzi wa	USD milioni 2.31	- Majadiliano na Serikali ya Austria kupitia Kampuni ya STRABAG kwa ajili ya ufadhili wa mradi

Na.	MKOA	MRADI	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	MAHITAJI YA FEDHA	MAELEZO
			matanki mawili ya mita za ujazo 1,000 na ukarabati wa tanki la mita za ujazo 90 na ujenzi wa <i>sump well</i>		yanaendelea - Usanifu umekamilika
		Mradi Maji wa Mji wa Kilindoni	Ujenzi wa nyumba moja ya mitambo, ununuzi wa pampu mbili, ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 21, ujenzi wa matanki matatu na ujenzi wa <i>sump wells</i> tatu	USD milioni 2.70	- Majadiliano na Serikali ya Austria kupitia Kampuni ya STRABAG kwa ajili ya ufadhili wa mradi yanaendelea - Usanifu umekamilika
